**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Kumi na Tano - Tarehe 04 Juni, 2015**

*(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawakena Watoto:** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake Watoto kwa mwaka 2015/2016 Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, naomba kuweka mezani maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2015/2016 naomba kuwasilisha.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 5**

**Matengenezo ya Barabara ya Bwagamoyo-Matuuni-Uondwe**

**Mhe. Salim Abdalla Hamad -** Aliuliza:

Katika ujenzi wa barabara mpya zilioko katika Mkoa wa Kaskazini Pemba ambazo zimefadhiliwa na Mfuko wa Changamoto wa Maendeleo ya *Millenium (Millenium Challenge Account)* wa Marekeani, Kampuni ya *H. Young* ambayo ndiyo wajenzi wa barabara hizo, ilichimba kifusi katika eneo la Mto Mkuu na kusababisha barabara ya Bwagamoyo - Matuuni – Uondwe ambayo ikitumika kubebea kifusi hicho kuharibika sana kiasi ambacho katika kipindi cha mvua huwa haipitiki na haitumiki kabisa.

Je, ni lini Kampuni hii itaifanyia matengenezo alau ya kuipa na kuiwekea kifusi barabara hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - ** Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Salim Abdalla Hamad Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Mtambwe swali lake Nam. 5 kama ifuatavyo:-
Mhe. Spika, barabara ya Mtambwe Bwagamoyo ina urefu wa kilomita 3.7 iliyo katika hali au hatua ya kifusi, barabara hii katika eneo la Kela hadi Bwagamoyo ilikuwa ina milima miwili ambayo ilikuwa haipitiki kabisa maeneo ya Mto Mkuu kupandishia kuelekea Matuuni.

Makubaliano ya kukodishwa eneo hilo kwa ajili ya wajenzi wa barabara za mradi MCC ilikuwa ni kwamba Mkandarasiachukue kifusi baadae hali ya barabara izingatiwe kwa kurejeshwa kama ilivyokuwa awali. Wizara yangu baada ya kupata taarifa hiyo ilifatilia na kusimamia kwa msingi pamoja na kulinda mazingira husika. Tayari maeneo ambayo yalichimbwa kifusi yamefukiwa kwa madhumuni ya kutumika kwa matumizi baada ya kukamilika kwa ujenzi husika.

Napenda kumthibitishia Mhe. Mjumbe kwamba wizara yetu kwa kukushirikiana na Wizara ya Kilimo kwa kupitia mradi wa MIVAP barabara hii itazingatiwa na itasimamiwa ili kuona inarudi katika hali yake pamoja na Mkandarasi kukamilisha ahadi yake.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, barabara hii tunayoizungumza kwanza ni barabara muhimu sana na kutokana na umuhimu ni wananchi wenyewe kwa gharama zao walioifanya mpaka ikawa inapita gari. Ninashukuru Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa wakati ule ikajenga daraja iliyo nzuri. Baada ya hapo kwa sababu ya umuhimu wake *TASAF* ilisaidia mara mbili kutoa fedha zake, milioni thalathini kwa mara ya mwanzo na milioni 40 kwa mara ya pili na zikatumika kwa kutia kifusi barabara hiyo.

Katika matengenezo ya hizi barabara kwa Kampuni hii ya *H. Young* ilibidi barabara ile waifanye pana zaidi ili magari yao yaweze kupita na kuchimba kifusi lakini katika kufanya hivyo ilibidi barabara ile ichafuke yote. Kwanza ilifanywa grading kifusi kikaondoka na ikafanywa pana na walipoitumia kwa magari yao kwa ile sehemu nyengine ikabidi barabara yote ichafuke. Hivi sasa ikinyesha mvua siku moja haipitiki tena na imeachwa kabisa.

Ningelipenda kujua Mhe. Naibu Waziri anieleze ni lini hasa barabara hii itashughulikiwa wakati Kampuni ya H. Young sasa hivi inashughulikia barabara nyengine ya vijijini.

Ikiwa ni mfuko wa kilimo naona kwa Mtambwe tayari umeshatumika kwa barabara mbili kuanzia Makongeni mpaka Kinazini na barabara ya Kivumoni. Je, ana uhakika na barabara hii ilikuwa imo haijatengenezwa itatengenezwa kweli.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano**: Mhe. Spika, ni kweli kwamba barabara hii imetumika wakati wa ujenzi wa mradi mkubwa wa *MCC*, kifusi kimechukuliwa kule na matumizi ya barabara hii yalikuwa zaidi ya uwezo wake kwa maana kwamba kama barabara ilikuwa ina uwezo wa kuchukua tani tano, mzigo uliopakiwa ndani ya *lorry* lile la kubeba kifusi ilikuwa zaidi ya tani 5 tabaan barabara ikavurugika. Tulichokisema kwamba sisi tumemsimamia na tutaendelea kumsimamia Mkandarasi kuona kwamba anatimiza makubaliano waliokubaliana na wananchi. Lakini kwa kuwa Mkandarasi huyu amepewa kazi na *MIVAP*, kazi ya kusimamia mradi wa *MIVAP* tayari sisi tumekubaliana kwamba kabla ya kukamilisha mradi wake wa *MIVAP* barabara hii ataitengeneza.

Kwa hivyo nimuombe tu Mhe. Mwakilishi kwamba siwezi kukwambia kama kesho au keshokutwa, lakini makubaliano yetu na ahadi yake kwamba kabla kukamilisha mradi wa *MIVAP* kazi ambayo amepewa atahakikisha kuwa barabara hii anairejesha kama awali kama ambavyo amekubaliana na sisi. Jukumu letu kama wizara ni kusimamia kwamba makubaliano hayo yatimie kwa vitendo.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize Serikali swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa barabara hii hutumiwa sana na wakulima katika vijiji vya Chekea, Kidundo, Mpakanjia, Uondwe, Kiapaka pamoja na Nyali katika kusafirisha karafuu zao na kwa kuwa ili kwenda kuuza Wete na kwa kuwa barabara hii kwa sasa haipitiki. Je, Mhe. Waziri anaweza kuishauri mamlaka husika wakulima wa vijiji vilivyovitaja wakasafirisha karafuu zao kupitia baharini na hatimaye kwenda Wete pale bila kukamatwa wakaambiwa wanataka kusafirisha magendo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, kwanza sikubaliani na kauli ya Mhe. Mjumbe kwa kusema kwamba njia hii haipitiki, nina uthibitisho kuwa njia hii haiko hali nzuri kama vile ilivyokuwa awali. Lakini njia hii inapitika na njia hii imeongezwa upana kutoka mita 2.5 mpaka mita 3.2 baadhi ya maeneo kwa hivyo barabara hii inapitika vizuri. Suala la wananchi kuweza kupatiwa nafasi nzuri ya kupita mimi nadhani katika maeneo ya Mtambwe sasa hivi kuna barabara nzuri zaidi kulikoni hapo awali. Tuna mtandao mpana na mzuri wa barabara ya lami, kwa hivyo kama kuna watu wanahitaji kusafirisha karafuu wazunguke tu wende Nyali watapata barabara ya Lami watakwenda Wete kwenye kuuza katika masoko yanayostahiki.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, je, ni lini atafanya ziara kati ya yeye na Mwakilishi kwenda kuangalia ukweli wa suala hilo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, nadhani alikuwa aseme Mwakilishi mwenyewe kwamba kama yeye anahitaji hiyo ziara, mimi wajibu wangu kutembelea maeneo yote niliyopangiwa kazi. Sina siku, sina wakati, nipo tayari muda wowote. Kwa hivyo kama anahitaji ziara yeye Mwakilishi aseme, mimi niko tayari kwenda kuyakagua maeneo hayo.

**Nam. 73**

**Upekuzi wa Abiria kwa Kutumia Mikono Bandarini**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub -** Aliuliza **:-**

Machi, mwaka huu tumeshuhudia upekuzi mkubwa katika Bandari ya Malindi kwa abiria wanaoingia kutoka Tanzania Bara. Bahati mbaya Maofisa wanaofanya kazi hiyo wanatumia mikono kupapasa watu hadi katika sehemu za siri za viungo. Kitendo hicho ni kwenda kinyume na misingi ya Haki za Binaadamu na mila na silka zetu.

(a) Kwa nini Serikali imeshindwa kwueka vifaa vya ukaguzi kama ilivyo kwa Bandari ya Tanzania Bara, ili kuepusha vitendo vya uvunjaji wa Haki za Binaadamu ikiwemo kumpapasa mtu katika sehemu zake za siri.

(b) Kama Serikali haina uwezo wa kununua vifaa kwa nini juhudi zisichukuliwe kuwaomba wahisani kusaidia eneo hilo kama wanavyosaidia maeneo mengine ya Bandari hiyo.

(c) Kwa kuwa suala la upekuzi wa mizigo ni nyeti kwa nini mizigo ya abiria wanawake ipekuliwe na Askari wanaume na wakati mwengine wanawake kupekua wanaume.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano –** Alijibu :-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake namba 73 lenye vifungu a, b, na c kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Shirika la Bandari imeweka utaratibu kwa wasafiri wanawake kupekuliwa na Maofisa Wanawake na wanaume kupekuliwa na Maofisa Wanaume pale inapobidi msafiri kupekuliwa mwilini.

Kwa upande wa mizigo Shirika hatuna utaratibu maalum wa kudadisi kwamba mzigo huu wa mwanamke au mwanamume, kwa hivyo upekuzi unafanywa na Afisa aliyepo katika kitengo kila au ama wakati ule aliye katika zamu. Pamoja na Utaratibu huo wizara tayari tumeona upo umuhimu katika bajeti ya mwaka tayari Shirika la Bandari wamezingatia ununuzi wa mashine za kukagulia mizigo yaani *X-Ray*.

Majibu, Mhe. Spika, Serikali haijashindwa kuweka mashine hizo za ukaguzi, tulikuwa na vipaumbele vyengine vya vifaa vya utendaji kazi katika maeneo ya bandari. Napenda kumthibitishia Mhe. Mjumbe na Baraza lako tukufu kwamba katika bajeti ya 2015/2016 ya Shirika la Bandari mashine husika zitanunuliwa.

(b) Mhe. Spika Serikali ina uwezo na tayari tumeshadhamiria tutalikamilisha kwa vitendo jambo hilo la kuweka mashine husika za ukaguzi.

(c) Utaratibu wa upekuzi wa mizigo hauzingatii nani mmiliki husika, aidha suala la jinsia tutalizingatia ikibidi, lakini mtazamo muhimu kwa Serikali ni kuweka upekuzi wa mizigo kwa madhumuni ya kulinda usalama wa bandari zetu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, rafiki yangu na nimpongeze kwa kutimia miaka 28 hivi juzi wala sio 38 ilikuwa tunadhamira ya kutafuta cheo cha ukoplo lakini ninafikiri kinakaribia. Lakini kwanza rafiki yangu Mhe. Naibu Waziri haya mambo mimi mwenyewe yamenikuta na sio bandarini tu mpaka *airport*; mimi nafsi yangu kama ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, mwanamume kupekuliwa na mwanamke nikampigia waziri. *X-Ray* nikuombe, kama unavyofanya ziara nyengine ukapata kwenda kuhakikisha bandarini haya mambo yapo na hayaleti sura nzuri hasa kwa wageni wote wanaoingia nchini, fanya ziara ukahakikishe. Mimi siwezi kurupuka tu nikaletwa swali ambalo halina ukweli ndani yake. Mimi ni mwakilishi na ninachukua wajibu wangu nini cha kufanya, hilo la mwanzo.

La pili utakuwa tayari au unataka ushahidi wa Kinyamwezi kushuhudia haya mambo yapo na unatoa kauli gani kwa kitendo kama hicho.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, Mhe. Spika, tunachokisema kwamba bandarini hatuna *X-Ray* hivi sasa, unapokuja na mzigo hatuzingatii mzigo huu wa jinsia gani, madhumuni ya Serikali ni kulinda usalama, mzigo wako utapekuliwa na Afisa aliyepo katika zamu, akiwa

mwanamke aikiwa mwanaume. Suala la kupekuliwa wwewe binafsi litazingatia jinsia yako. Kama mwanamke utapekuliwa na mwanamke, kama mwanaume utapekuliwa na mwanamme mwenzako, kama kuna kosa limetendeka sisi ni wajibu wetu kurekebisha na tutawaelekeza watendaji wetu kwamba hivyo si sahihi. Sasa ukinambia tusubiri ushahiidi wa kinyamwezi sijui unamaanisha nini.

Mimi wajibu wangu ni kusema kwamba ninajua utaratibu kwamba hatuna *X-Ray* machine katika eneo la Bandarini, madhumuni ya Serikali ni kutenga fedha kwa ajili ya kununua mashine husika kipindi hiki ambacho hatuna mashine mizigo yote bila ya kujali huu wa nani tutachukua kupata usalama. Lakini upekuzi wa mtu binafsi tutazingatia jinsia mwanamme atapekuliwa na mwanamume mwenzake na mwanamke atapekuliwa na mwanamke mwenzake.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana yaliyojibiwa na Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, naomba kutoa maelezo ya ziada kuhusu suala la vifaa vya ulinzi katika bandari ya Malindi. Kupitia Baraza hili Tukufu naomba nimueleze Mhe. Mwakilishi kwamba katika mradi wetu wa *CCTV* Mkoa wa Mjini Magharibi pia umezingatia kuwa na *X Ray machine* katika bandari ya Malindi na katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Abeid Amani Karume. Ahsante sana.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Ahsante Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu ya nyongeza ya Mhe. Waziri kuhusiana na suala zima la mashine hizi za upekuzi. Katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba Serikali tayari imeshatenga fedha kwa ajili ya bajeti hii inayokuja. Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho kitatumika kununua mashine hizi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, hatuwezi kutaja kiwango cha fedha ambazo tumekitenga na hatuwezi kutaja kwa sababu ya utaratibu wa zabuni, tukisema kwamba kwa mfano tumetenga milioni kumi maana yake tunawaambia hawa ambao tutawatangazia zabuni kwamba na wao wanatakiwa kuleta zabuni yao kwa kulenga ile milioni kumi. Utaratibu wa Serikali kwamba tumetenga fedha, tutakwenda katika mchakato wa zabuni atakayeshinda zabuni tutampa kazi atatuletea vifaa, tutafanya kazi za wananchi kama tulivyokusudia.

**Nam. 4**

**Upatikanaji wa Umeme kwa Wananchi wa Zanzibar**

**Mhe. Salim Abdalla Hamad –** Aliuliza:-

*ZECO* ni Shirika ambalo ndilo linalohusika kikamilifu na kazi ya kuendesha na kutoa huduma ya umeme kwa wateja walioko Zanzibar, kwa sababu umeme huu ambao unatoka Tanzania Bara ni ghali kwa kiasi ambacho Wazanzibari walio wengi hawawezi kumudu gharama ambazo *ZECO* inanunua umeme huo kutoka *TANESCO*.

(a) Ni kiasi gani cha fedha ambacho *ZECO* inafaidika kwa wananchi kutokana na bei ambayo *ZECO* inailipia *TANESCO* ukilinganisha na mauzo ya umeme huo kwa wananchi.

(b) Hivi sasa *ZECO* inadaiwa kiasi gani na *TANESCO*.

(c) *ZECO* inadai kiasi gani kwa wananchi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kutokana na gharama za uendeshaji bei inayouziwa umeme kutoka *TANESCO* na bei inayouziwa umeme kwa wateja wa Zanzibar Shirika limekuwa likipata hasara. Hasara hii inaonekana katika mahesabu za Shirika ya mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2014. Hata hivyo, mbali ya hasara inayopatikana bado Shirika limeweza kumudu utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo kupeleka umeme vijijini. *ZECO* imeweza kujiendesha japokuwa inapata hasara kwa sababu ya kulipa robo tatu ya ankara yake kwa *TANESCO* na robo moja ndio inayotumika kwa shughuli zake.

(b) Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2015 Shirika la Umeme linadaiwa na *TANESCO* jumla ya shilingi bilioni 50.8. Katika kupunguza deni hilo *ZECO* imewekeana utaratibu wa kulilipa na *TANESCO* kama hivi ifuatavyo:-

- Kulipa ankara ya mwezi kwa ukamilifu na kulipa shilingi bilioni moja kila mwezi kwa ajili ya kupunguza deni hilo. Hata hivyo, *ZECO* imeweza kutekeleza ulipaji wa ankara kwa miezi minne tu na miezi miwili tu *ZECO* iliweza kulipa ziada ya milioni 500.

(c) Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2015 *ZECO* inawadai wateja wake jumla ya shilingi bilioni 33.02 kwa mchanganuo ufuatao:-

- Wateja binafsi ni shilingi bilioni 9.01
- Taasisi ya SMZ ni shilingi bilioni 22.52
- Na Taasisi za SMT ni shilingi bilioni 1,475,838,593

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake yakuridhisha kabisa, lakini pamoja na hayo naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa sababu *ZAWA* ni taasisi iliyomo katika wizara yake na kwa sababu *ZAWA* imeshindwa kufanya majaribio na badala yake yakatumika miradi mikubwa ya maji iliyofanywa na Wachina kwa sababu tu wanaida fedha nyingi sana na *ZECO* kiasi ambacho *ZAWA* waliona ni afadhali hata wangelifunga mita za TUKUZA lakini haikuwezekana.

a) Suala langu la kwanza hili je, hii *ZECO* inaidai kiasi gani *ZAWA* na kwa sababu ni fedha nyingi na *ZAWA* haina uwezo wa kulipa fedha hizo malipo yako yakoje ili *ZECO* iweze kufanya kazi zake ipasavyo.
b) Kutokana na maelezo ya Mhe. Waziri ni kwamba *ZECO* inanunua umeme ghali na inatoa fidia kwa wananchi, nataka kujua katika kila *unit ZECO* inatoa fidia kiasi gani kwa wananchi ili wananchi waweze kuutumia umeme huo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, suala hili la mwanzo hata juzi tu nimelijibu kwamba Mamlaka ya Maji *ZAWA* pamoja na Shirika la Umeme hakuna matatizo yoyote. Ni kweli lilikuwepo deni ambalo walikuwa wanadaiwa *ZAWA*, lakini deni hilo limechukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Fedha na tayari linalipwa na Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, hakuna matatizo kati ya Shirika la Umeme na *ZAWA* na tayari Shirika la Umeme visima vyote ambavyo vilikuwa vimefungwa mita za TUKUZA, mita hizo zimefunguliwa na zimefungwa mita za kawaida ili tu *ZAWA* ifanye kazi zake vizuri ya kuwahudumia wananchi katika huduma hii ya kuwapatia maji safi na salama. Naomba suala la pili Mhe. Mwakilishi alirejee sikulifahamu vizuri.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, kwa sababu Mhe. Waziri amekiri kwamba kwa bei ya umeme *ZECO* inayonunua kutoka *TANESCO* na umeme ule

kuupeleka kwa wananchi, wananchi itakuwa hawana uwezo wa kulipia gharama kama wanavyonunua wao na hivyo *ZECO* inatoa fidia. Suala ni kiasi gani cha fidia kinachotolewa kwa kila *unit* moja ili mwananchi aweze kutumia umeme huo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwanza nikubaliane na Mhe. Mwakilishi au nirejee suala langu kama nilivyoeleza hapo awali kwamba bei tunayonunua umeme kwa wenzetu wa *TANESCO,* ni bei kubwa sana na katika uendeshaji wa Shirika kulingana na bei ambayo tunayonunua umeme kutoka *TANESCO* basi Shirika linakula hasara, lakini bado Serika ya Mapinduzi ya Zanzibar iko tayari kuwahudumia wananchi wake hususan kupitia suala hili la kuwasambazia umeme.

Bei ya *unit* ziko katika hali tofauti, kuna *unit* za mteja wa kawaida ambayo ni shilingi 90 mteja wa chini na kuna *unit* ambayo tunauza 220. Kwa hiyo, hakuna fidia yoyote ambayo inayotoka kwa mteja, kwa sababu kama nilivyoeleza hapo awali wizara yangu kupitia Shirika la Umeme kwamba inanunua umeme kutoka *TANESCO* kwa bei kubwa mno.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, na mimi nashukuru sana kwa kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri sana Mhe. Naibu Waziri ama leo ametulia sana. Mheshimiwa kauli yako ya mwanzo na ya pili ulieleza kuwa ni kweli *ZECO* inanunua bei kubwa sana kwa *TANESCO*. Mhe. Spika, *ZECO* tunaijua kama ni sehemu ambayo inayoendesha hapa Zanzibar na wanachama wake wanaonunua umeme ni watu duni sana. Mheshimiwa huoni kama sasa hivi Shirika lako linakwenda na hatua ya kufa.

La pili Mheshimiwa kwa kuwa hali kama hiyo serikali imeona je, wizara yako ina mpango gani wa kutafuta umeme mbadala wenye bei rahisi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, bado niseme Serikali ya Mapinduzi Zanzibar lengo langu kuu ni kuwasambazia wananchi wote huduma ya umeme katika miji na vijiji. Na pia katika suala zima la kutafuta umeme mbadala Zanzibar, basi serikali iko katika jitihada hizo na tayari serikali imeunda kamati maalum ambayo inafuatilia masuala hayo. Kwa hiyo, pindi yatakapokamilika basi Zanzibar itapata umeme ambao unajitegemea kutoka Zanzibar wenyewe.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 – Wizara ya Afya

(*Majadiliano yanaendelea*)

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea na majadiliano leo tunao wageni vile vile ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Zanzibar wamekuja hapa kwa ajili ya kujifunza shughuli zetu za Baraza, na wanafunzi hao jumla yao ni 70 wanaongozwa na baadhi ya viongozi wao wakiwemo Waziri Mkuu, ndugu Mussa Hashim Khamis pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria ndugu Mkasi Hassan Thabit, pamoja na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria ndugu Ali Ahmed. Niwaombe basi wanafunzi hao 70 pamoja na viongozi wao wanyanyuke ili wasailimiane na Waheshimiwa Wajumbe. Karibuni, wale pale, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, jana tulishindwa kuendelea na shughuli yetu kama mara kwa mara nilivyokuwa naonya kama *quorum* inakuwa haitimii. Nimeshauriwa kwamba tutengue Kanuni, lakini suala la kutengua Kanuni mimi naliona ni tatizo kidogo, kwa sababu chombo hiki ni chombo cha demokrasia na suala la demokrasia limo ndani ya Katiba kuamua mambo ni sehemu ya demokrasia ile kufanya maamuzi ni sehemu ya demokrasia. Tukiamua tukiwa hatuna *quorum* ambayo inatambulikana kwa mujibu wa Kanuni zetu maana yake hata ule utaratibu wa demokarasia itakuwa hautimii sawa sawa.

Demokrasia ni jambo la Kikatiba ambalo kimsingi ni lazima tuitimize kama ilivyo. Kwa hiyo, mimi niendelee tu kuwaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kwamba tujitahidi sana tuwemo humu ndani na kabla ya kuendelea tutahesabu wajumbe waliomo sasa, kama itakuwa wametimia basi tutapitisha hoja hii, lakini kama itakuwa hawajatimia tutaendelea na hoja iliyopo, Waswahili wanasema “ng’ombe anavyoanguka ndivyo anavyochinjwa hivyo hivyo”. Kwa hiyo, wacha niwaambie Makatibu hapa waweze kuhesabu ili tuone ni wajumbe wangapi. Hivi tuna wajumbe wangapi Katibu?

43 oh! Naambiwa leo haijambo kidogo basi tuitumia nafasi hii kwa kumuomba Mhe. Waziri wa Afya sasa atoe hoja baada ya kuwa amefanya majumuisho jana. (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya wizara sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu. Naomba kutoa…

**Mhe. Spika:** Hapana, jana hoja haikuungwa mkono kwa *quorum* inayotimia, kwa hiyo kwanza tuwahoji wajumbe hawa wakubali ili baadae tutakwita tena ili useme hayo maneno uliyosema sasa, omba kutoa hoja baada ya yale majumuisho yako uliyofanya Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, baada ya maelezo ambayo niliyatoa kwa wajumbe na nawaomba sana wajumbe waipitishe bajeti yetu ili tuweze kuwatumikia wananchi mbali mbali wanaokuja hospitali na wale wanaotaka huduma ya afya kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri rudi kwenye nafasi yako kidogo. Naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Afya kwa mwaka 2015/2016 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lako limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afya sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu. Naomba kutoa hoja.

## KAMATI YA MATUMIZI

### FUNGU H01 - WIZARA YA AFYA

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 01 | Afisi Kuu Pemba | Sh. 96,000,000/= |
| Kifungu 04 | Idara ya Kinga Unguja | Sh. 47,338,000/= |
| Kifungu 05 | Idara ya Tiba | Sh. 25,400,000/= |
| | **JUMLA KUU** | Sh.**168,738,000/=** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU H01 - WIZARA YA AFYA**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu kidogo S01 | Programu ndogo ya Kinga na Elimu ya Afya | Sh.32,963,434,000/= |
| **Jumla ya Kifungu P01** | | **Sh.32,963,434,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KIFUNGU P02 PROGRAMU YA HUDUMA ZA TIBA**

**Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilimuomba Mhe. Waziri katika programu hii ya P02 Huduma za Tiba aweze kunitengea shilingi milioni mia moja kwa ajili ya ununuzi wa *lift*. Pamoja na majibu mazuri ambayo Mhe. Waziri amejibu akisaidiana na Naibu Waziri wake, bado sijaridhika na majibu yake, naomba bado kuendelea kutetea hoja katika fedha ambazo zipo hapa hususan katika hili fungu la H04, Mradi wa Huduma ya kupandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja kwenye shilingi bilioni kumi na sita, milioni mia mbili na tisini na saba, mia sita na ishirini na saba elfu tupunguze shilingi milioni mia moja kwa ajili ya ununuzi wa *lift*.

Nimeangalia vizuri sana na nimeona kwamba katika hiki kitabu tulichonacho ambacho kuna ufafanuzi mbele ukurasa wa 475 hapa chini pameelezewa kwa vizuri sana matumizi ya fedha hizi. Moja kati ya matumizi haya ni kufanya matengenezo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Naomba maelezo ya ziada Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kwa kifupi anachoomba Mhe. Mjumbe ni kwamba tufanye *reallocation* ili tutoe fedha kwenye kifungu hicho tulete katika kifungu cha kuimarisha huduma za pale ili *lift* iweze kununuliwa, nadhani kwa ufupi ndio hayo.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, katika majibu yetu tuliyosema jana tulikubaliana na hoja yake, lakini tulimwambia kwamba kila kitu kina *priority* yake. Sisi hatuwezi kutenga shilingi milioni mia moja ikiwa hatujaijua ile bei ya *lift* kwa sababu sasa hivi hatuwezi kutengeneza *lift*. Mnazi Mmoja zipo *lift* mbili, moja imetiwa mpya tutakapotenga fedha tutatenga fedha kwa ajili ya *lift* mpya na sio kutengeneza *lift*. Kwa hivyo, kutenga shilingi milioni mia moja wakati hatujaijua bei yake itakuwa haisaidii. Sisi tuko tayari kutia *lift* mpya lakini bei yake haijajulikana na sio kutengeneza *lift* iliyokuwepo, kwa sababu *lift* iliyokuwepo imepitwa na muda sana halafu tunajua *technology* za sasa zimekua sana kiasi cha kwamba ukienda katika baadhi ya hoteli Mhe. Mwenyekiti *lift* inakwenda kwa

*security card*, ambayo ndio tunayoitaka kwa pale ili iweze kubeba wagonjwa tu na sio kutumia kwa watu wengine. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mheshimiwa nilimwambia toka jana kwamba hili tuchukulie kwa sababu hii ni kitu ambacho *particular* na kila daktari, kila mfanyakazi, kila afisa ana hakika kwamba *lift* ni muhimu kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio maana ikatiwa mpya ile moja sasa bado nyengine moja. Hatukulidharau, kwa hivyo tunamuomba Mhe. Mjumbe atuchukulie na kwa sababu mambo haya yanapata ufadhili haina haja ya kumegua pesa hizi za wagonjwa tunaweza tukapata njia nyengine, tukapata *lift* ya kisasa yenye kulingana na huduma inayotakiwa. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Mjumbe atuchukulie kwa hilo.

**Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba Mhe. Waziri anifahamu ninachokisema, ninachokizungumza ukienda katika ukurasa wa 475 fungu ambalo mimi nalizungumzia kitabu hicho hicho alichonacho, hapa katika programu hii imeelekezwa kwamba ni mradi wa huduma ya kupandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kifungu kidogo cha 1 kinasema kwamba, kufanya matengenezo ya jengo la madawa ya macho na watoto, lakini programu ya pili yake inasema kwamba ni kufanya matengenezo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, *lift* ni sehemu ya matengenezo katika hospitali hii na ndio maana nikaomba kwamba, kutokana na usumbufu ambao wananchi wanaupata naomba sana suala hili lizingatiwe ili katika kasma ya shilingi bilioni nne zitoke shilingi milioni mia moja. Nimezungumza hivi kwa sababu naelewa kwamba dola 40 mpaka 60,000 zina uwezo wa kuweza kupata hiyo *lift*, *maximum* kabisa. Kwa hiyo, ndio maana nikamuomba Mhe. Waziri kwamba tufanye utaratibu kupanga matumizi ni kuamua tu Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hiyo tufanye utaratibu nipewe maelekezo kwamba *lift* itanunuliwa na sio kutegemea wahisani kama ambavyo tumepitisha bajeti yetu kubwa kwa kusema kuwa bajeti yetu itakuwa ni tegemezi. Naomba wizara ichukue dhamana kuhakikisha kwamba katika kipindi hiki kidogo *lift* inanunuliwa na wananchi hawapati tena usumbufu wa kuweza kupandisha wagonjwa kwa kutumia mikono. Naomba maelezo ya ziada Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, sijui Mhe. Mwakilishi anataka tumueleze vipi, nasema kuanzia sisi wizara na Hospitali ya Mnazi Mmoja *management* yake na madaktari wote wanaamini hilo analoamini yeye, kwamba *lift* ni muhimu kwa ajili ya kupandisha wagonjwa na kuteremsha pamoja na *staff* wake. Lakini ndio tukamwambia kwamba sisi hii shilingi milioni mia moja yeye kaipata wapi, sisi hatuwezi kuji-*commit* katika shilingi milioni mia moja tutaji-*commit* kwa zaidi ya hapo, lakini lazima tupate ile *net price* yake. Sasa tukisema

shilingi milioni mia moja tunazitenga ikiwa hazitendi chochote sasa tutakuwa tumefanya nini?

Kwa hivyo, sisi tushamwambia tutaji-*commit* katika hayo matengenezo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja moja wapo ni hiyo *lift,* lakini hatuwezi kuji-*commit* kwa shilingi hizo milioni mia moja. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Sijui kama nimefahamu sawa sawa, wizara au waziri kwa niaba ya wizara anasema kwamba hilo jambo wanakubali lakini hawawezi wakasema kwamba, wafanye *reallocation actually* hiyo kazi ya *reallocation* sio kazi ya Baraza hili, kwa sababu ina taratibu zake na inabidi lazima upate idhini fulani na idhini hiyo haipo hapa, lakini wanakubali *commitment* ya kutafuta *lift.* Lakini wakisema kwamba wahamishe shilingi milioni mia moja kwa ajili ya kununua *lift* na ikaja ikatokezea kwamba *lift* hiyo pengine ni shilingi milioni mia moja na hamsini maana yake maagizo ya Baraza hili itakuwa hayawezi kufua dafu. Lakini anakubali kwamba *lift* litanunuliwa tena jipya anasema na wanataka *lift* aina ambayo itawezesha kwa kutumia *security card* waingie wagonjwa tu, mana sote sasa hivi tutakuwa tumepata kama kitu cha urahisi tutaingia tu mle na kitu kikitumika sana kuharibika kwake ni kwepesi ndio hilo analosema waziri. *(Makofi)*

Makofi haya nadhani wamekubali na Mhe. Mjumbe nadhani atakuwa amekubali.

**Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, nimefarajika kuona kwamba Mhe. Waziri amekubali lakini na mwenyekiti wangu mweza msaidizi wake kanisisitiza kwamba nikubali yeye atalishughulikia. Kwa hiyo, kazi hii nawaachia kamati inayohusika, ili wahakikishe kwamba suala hili linafanyika ndani ya kipindi kifupi na *lift* inapatikana na watu wanaendelea na kupata huduma hiyo. Naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

**KIFUNGU P02 PROGRAMU YA HUDUMA ZA TIBA**

| | |
|---|---|
| Kifungu S01 Huduma za Hospitali | Sh.37,860,771,000/= |
| **Jumla ya Kifungu** | **Sh.37,860,771,000/=** |

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KIFUNGU P03 PROGRAMU YA USIMAMIZI WA SERA ZA AFYA NA UTAWALA**

| | |
|---|---|
| Kifungu S01 Programu ndogo ya Uongozi na Utawala | Sh.3,106,943,000/= |
| Kifungu S02 Programu ndogo Sera, Mipango na Utafiti | Sh.3,417,952,000/= |
| Kifungu S03 Programu ndogo ya Kuratibu Shughuli za Afya Pemba | Sh.7,631,000,000/= |
| **Jumla ya Kifungu:** | **Sh.14,155,895,000/=** |
| **JUMLA KUU:** | Sh.**84,980,100,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU H02 HOSPITALI YA MNAZI MMOJA**

| | |
|---|---|
| Kifungu 01 Idara ya Utawala na Huduma | Sh.902,973,000/= |
| **JUMLA KUU:** | **Sh.902,973,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU H02 HOSPITALI YA MNAZI MMOJA**

**Mhe. Jaku Hashi Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, huu ni mwaka wangu wa tatu au wa nne kwa masuala ya Wizara ya Afya. Kwa masikitiko makubwa na uchungu, huruma kubwa na huzuni karibu siku zote nilikuwa nikichangia suala hili kuhusu banda la wagonjwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na suala la Dkt. Hamza Hospitali ya Jambiani. Suala hili nimelipigia kelele kwa muda mrefu na hizi dakika zangu za mwisho na bajeti yenyewe ni ya mwisho sitokubali. Kuna wimbo unasema, kuna aliyeanza leo na atakaekuja kesho, nililipigia kelele sana suala la banda lile hakuna kauli. Mhe. Naibu Waziri aliji-*commit* katika chombo hiki cha wananchi akanambia miezi sita huu ni mwaka mmoja na nusu na *hansard* zipo.

Sasa nataka maelezo ya kina kabisa na ufasaha kuhusu banda lile la wagonjwa. Nimshukuru tena Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kutoa kibali eneo lile kujengwa, ilikuwa si kazi rahisi na mmoja wa wahangaikaji ni mimi. Mhe. Waziri yeye anategemea kuaga penye majaaliwa huku wananchi wanaendelea kuteseka, nataka maelezo ya kina na ya ufasaha kabisa vyenginevyo Wajumbe kwa hili nilikuombeni tokea jana. Sijawahi kuomba katika Baraza hili, watu pale wanateseka wanapigwa na mvua maradhi yanazidi wanaoumia ni

wananchi na hii ni dhamana ya wananchi tutakwenda kuulizwa tumetumia vipi dhamana yetu. Pale hapapikwi pilau wala biriani wanakwenda kwa shida.

Mhe. Waziri naomba sana kwa heshima na taadhima tusikilize jawabu ambazo zitaleta muwafaka na yeye vile vile kuwa imamu wetu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Hoja yenyewe ni vipi? Ile hoja yenyewe hasa.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, hoja ni kujengwa kwa banda la wagonjwa mwaka wa nne hakujapatikana jawabu na hii ni lala salama. Nataka kauli ya serikali ambayo itaniridhisha, vyenginevyo nafikiri kuna Wajumbe humu watani-*support* kwa suala hili.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza naomba nisahihishe kidogo maelezo aliyotoa yeye sio banda la wagonjwa ni banda la wananchi kwa ajili ya kusubiri wakati wa kuangalia wagonjwa wao. Wagonjwa wanapofika wana sehemu zao za kwenda kukaa na kungojea matibabu. Hili ni banda ambalo lingetarajiwa kujengwa kwa ajili ya wale wananchi ambao wanakwenda kabla ya wakati kwa kutizama wagonjwa, ili wapate kupumzika badala ya kwenda kwenye hospitali na kufanya msongamano mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa majibu yake ni kwamba, ni kweli wizara tayari imeshatayarisha mchoro na ilichukua muda mrefu kutayarisha michoro ile kutokana na masharti ya Hifadhi ya Mji Mkongwe na gharama inakadiriwa kuwa ni shilingi 200,000,000 kulijenga. Sasa kwa wakati huu kwa Wizara ya Afya na fedha inazopata haina uwezo wa kujenga hilo, kwa hivyo wizara iliamua kwamba itoe matangazo kwa ajili ya kukaribisha wawekezaji au mradi wa pamoja na watu binafsi.

Matangazo hayo Mhe. Naibu Waziri amejibu jana katika majibu yake kwamba yameshatolewa katika mitandao na jana alitangaza rasmi, vile vile hapa kwamba mtu yeyote anayetaka kujenga alete maombi yake ili tuweze kukaa pamoja na wizara kujenga. Lakini katika kipindi hiki ambacho sisi, mimi na naibu waziri tuliingia Mhe. Mwenyekiti. Sasa hivi tumeshasahau lakini kulikuwa na mripuko wa maradhi ya Ebola ambayo ni jambo la kimataifa na tulitarajiwa tuchukue hatua zote sisi. Kwa hivyo, kwa mujibu wa kinga ilikuwa lazima tuchukue hatua za dharura za kujitayarisha na maradhi ya Ebola na hilo liko wazi na hatua tumezieleza jana katika *budget speech,* hatua gani zilichukuliwa. Kwa hivyo, hili suala halikudharauliwa.

La mwisho serikali haina lala salama, serikali inaendelea. Hii ni lala salama kwa sisi kuna wengine tutarudi na wengine hatutarudi, lakini serikali haina lala salama itaendelea. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.*(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Kwanza hiki kifungu sicho, kwa kuwa suala lilikwishaulizwa tu, lakini kifungu hasa ni uongozi na utawala. Sasa kwa kuwa majibu yashatoka nikaona basi huko kwenye uongozi na utawala tusije tukasema tena lakini ndio kifungu chake. Lakini huduma za wagonjwa si huduma za watu wanaokuja kuangalia wagonjwa ni vitu viwili tofauti. Ehee Mhe. Jaku.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Hii ni harakati unajua jambo ukilifukuzia Mheshimiwa lina harakati zake na hili suala ni la muda mrefu basi kila linapofika Waswahili wanasema: "Unapokuta maji yakoge mwanzo hujui kama mbele utayakuta tena huko".

Mhe. Mwenyekiti, naomba hapa unistahamilie sana tena kwa heshima kabisa, sijawahi kukuomba katika maisha yangu mara yangu ya mwanzo leo Mhe. Mwenyekiti. Wizara inataka kupitisha bajeti yake majibu haya mimi nishayazowea Mhe. Mwenyekiti, leo mwaka wa nne Naibu Waziri *hansard* ipo katoa miezi sita tu, wanaoteseka pale ni watu wanaosubiri wanatoka Muyuni, Makunduchi, Kengeja, Mtambile wanakuja pale, hilo banda miaka minne waziri nilichozungumza mimi ni Kiswahili kiko wazi. Leo kweli serikali inashindwa kwenda kujenga pale? Haiwezekani Mheshimiwa ni muda mrefu hivi kutangaza *tender* huu ni uongo dhahiri tena umekuwa, sasa hivi siwezi kusema lugha hiyo, miaka minne haiwezekani.

Mhe. Mwenyekiti, siwezi kufuta kauli nakijua ninachokizungumza nasemea hoja ninayoijua. Hapa panataka kupitishwa bajeti haiwezekani mimi nitaisimamia hoja hii kwa kwa banda lile linalotaka kwenda kujengwa kuwa linatangaziwa tenda sasa hivi, hiyo miaka minne walikuwepo wapi hawajui kwamba kuna tenda...

**Mhe. Mwenyekiti:** Ngoja nikusaidie Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Labda Mhe. Waziri Mhe. Jaku Hashima Ayoub anataka uoneshe *commitment* kama ile ya kwenye *lift* hebu twambie unategemea kufanya vipi.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, *commitment* sie tumeshatoa kwa sababu tumeshakiri kwamba kwa sasa kwa bajeti yetu ilivyo hatuwezi kulitekeleza. Tunakaribisha *PPP* ambayo ni sera iliyokubalika na serikali. Sasa hatuwezi kumchukuwa Mhe. Jaku Hashim peke yake kwa sababu tunatizama *conditions* zake ndio maana tukataka na wengine wajitokeze. Tunajua yeye ana *interest* ya kuja kujenga lakini hatuwezi kumchukuwa peke yake. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim Ayoub sijakuruhusu bado. Anachosema Mhe. Waziri kwamba jambo hili wanalizingatia na katika mazingatio ni kwamba tena mimi sitaki tuite banda tukiita banda tunalidogesha.

Hapa ni pahala maalum, ni ujenzi maalum kwa ajili ya wale wanaokuja kuangalia wagonjwa wapate kusubiri. Ukiita banda inakuwa ni kama kitu kidogo kidogo tu hivi cha ovyo ovyo na hatutaki kufanya kitu cha aina hiyo na ndio maana, sasa akawa anasema kwamba *commitment* yao baada ya kuwa kulikuwa na shughuli kubwa sana ya maradhi ya Ebola na wakatakiwa wachukuwe hatua muafaka wanachofanya.Ssasa ni kuomba mashirikiano na wengine ili kitu hichi kiweze kuja kujengwa ndicho anachosema. Kwa hiyo, kazi hiyo ndio anayowaahidi hapa wizara wataifanya. Inaweza wakati huo anaweza kuwa yeye au mwengine. Hebu twambie hapo unasemaje, sasa na makofi uliyasikia.

**Mhe. Jaku Hashim  Ayoub:** Naendelea kuheshimu na nitaendelea kuheshimu mpaka dakika ya mwisho. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hili suala la muda mrefu hawajawa tayari kutangaza hizi tenda haya ni maneno tu. Serikali haijawa tayari na mimi wala sipataki pale Mheshimiwa wala sina *interest* ya kufanya biashara sijui biashara gani nikaifanye pale, ninawowalilia ni wananchi sina *interest* yoyote Mhe. Waziri ukafikiri kama nataka kujenga pale.

Ninacholilia wananchi wanateseka ile hospitali toka asili yake imejengwa sehemu ya kukalia wananchi, leo imeenda kuwekwa ma- *files*. Kwa hapa kama hawezi mimi la mwisho anikabidhi ramani nitatafuta njia za kwenda kuweza kujenga banda lile ndilo la mwisho hili ili suluhu ipatikane. Anikabidhi ramani nitaenda kutafuta njia mimi za kwenda kujenga ndio la mwisho, vyengine kikatafutwe cha kufanya. Haiwezekani kustahamili mambo kama haya anikabidhi ramani. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri una majibu za ziada.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ**: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani Mhe. Jaku Hashim Ayoub aelewe kwanza taratibu za utendaji wa kazi za kiserikali, kama ulivyokwisha kumuelekeza Mhe. Mwenyekiti. Jambo hili yeye anasema miaka minne iliyopita. Lakini mimi nadhani Mhe. Jaku Hashim na yeye anaweza akawa ni binaadamu akawa amesahau namna ya hili jambo lilipoanza kushughulikiwa na serikali sio miaka minne iliyopita.

Ni miaka ambayo mimi nimeshahamishiwa Wizara ya Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ na Waziri Mhe. Juma Duni akiwa Waziri wa Afya kwa mara ya kwanza aliniandikia barua ya kutaka ku- *surrender*  eneo la bustani iliopo mbele ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, ili turuhusu ujenzi ambao Mhe. Jaku Hashim Ayoub

anauzungumzia na mimi toka nimekwenda Tawala za Mikoa sijafika miaka minne bado.

Hapo ndio ilikuwa mwanzo wa historia ya hili jambo baadae sisi tukafanya kazi ya kiserikali kitaasisi tukashirikiana wizara tatu, Wizara ya Tawala za Mikoa, Wizara ya Ardhi na Wizara ya Afya ili tuone hili jambo linaweza kupatikana na chanzo chake walijitokeza watu au wafanyabishara wenye imani kama hiyo aliyonayo Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Wakasema wao wako tayari wakipewa kibali wataweza kufanya hiyo huduma ambayo Mhe. Jaku Hashim Ayouba amekuwa akiizungumza.

Serikali ikafanya hivyo, lakini baadae wale watu wakashindwa kuweza kutekeleza hilo jambo. Kwa hiyo, serikali toka mwazo ilipokuja na dhana hii ilikuja na dhana ya *PPP* kwa maana ya kuiga mfano kama ulioko Hospitali ya Muhimbili. Muwekezaji binafsi kuweza kutoa huduma hizi kwa nia ya kupata shufaa kwa Mwenyezi Mungu yaani kama kutoa sadaka.

Pia atengeneze vitu vya kuweza kutengeneza na yeye apate chochote kwa maana ya kuweka vituo vya biashara kama *Restaurant* maduka ya *Pharmacy* na kadhalika. Sasa serikali imeshafanya hivyo na jana Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akilitolea ufafanuzi jambo hili alisema kwamba serikali hatuna bajeti ya kutekeleza hili. Lakini kama yuko mfanyabiashara anataka kulifanya hili jambo kwa nia ya kuwasaidia wanaokwenda kuangalia wagonjwa basi sisi tuko tayari na tukatangaza tenda.

Hasa Mhe. Jaku Hashim hawezi kutwambia hapa serikali tumkabidhi *document* tutakwenda katika utaratibu wa kiserikali mtu aji - *commit* aseme kama ana uwezo wa kufanya hiyo kazi tumuamini tumpe. Hatuwezi tukampa sisi hapa utaratibu wa kiserikali haukubali. Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema hayo. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hasim Ayoub nadhani sasa baada ya maelezo yalitolewa na Mhe. Waziri na Mhe. Waziri wa Tawala wa Mikao sasa tuende kwa Wajumbe maana hili jambo si lako peke yako.

Waheshimiwa Wajumbe Waziri ametoa *commitment* hiyo na hapa nimepata karatasi inaonesha kwamba wazo hilo la kuitisha utaratibu wa *PPP* kama alivyosema Mhe. Waziri imo humu ndani. Hivi Waheshimiwa Wajumbe tunasemaje tunakubaliana na Mhe. Waziri afanye hivyo au tunasemaje?

Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubalina na wazo la wizara wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

*(Hoja ilitolewa aimuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Haya tuendelee. Sasa maamuzi yameshafanywa hebu kaa kitako Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mhe. Jaku Hashim Ayoub katika hili hebu kaa kitako. Tunaendelea.

P01 Huduma za Uchunguzi na Matibabu ...
**Mhe. Mwenyekiti:** Enhe kuna hoja nyengine?

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, kama nitakosea utanirekebisha mimi mtu mtiifu sana wala sina tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, jana Mhe. Naibu Waziri alinijibu kuhusu lile suala la Mashine la *Full Blood Picture*. Mhe. Spika, kwa kweli lile suala katika maelezo yake sikuridhika nayo kwa sababu zile ni fedha. Mashine ile imenunuliwa milioni kumi na sita na mapukupuku ndani yake na fedha zilizotoka milioni ishirini. Ningemuomba sana Mhe. Waziri bado hajawa muwazi. Yeye alisema limeungua kutokana na *shortage* ya umeme anasema ni *power supplier* na *power supplier* ninavyojua mimi ni kitu ambacho kinalinda kiti ambacho kikiingia *force* kile kina-*control* ninavyoelewa mimi.

Lakini kuna kitu ambacho kinaitwa *socket* ndio iliyoungua. Sasa Mheshimiwa kwa kweli hajanipa hoja ya kuniridha. Mimi ninavyomuomba anipe hoja kwa sababu kile chombo ni muhimu sana hasa kutokana na Hospital ya Rufaa, halafu kile chombo chenyewe naamini Mhe. Naibu Mhe. Waziri hawakijui hata rangi yao. Sasa kama kweli tuone wamefatilia hili suala wanambie hata ile rangi ya ile mashine yenyewe. Kwa sababu mashine yenyewe ukiangalia haifai hata kwenda pale katika rufaa. Mashine ile inatakiwa iwekwe kwenye Wilaya na sehemu nyengine.

Sasa ningeomba Mheshimiwa anipe jambo lenye matumaini, sitaki kuzuia kifungu lakini nataka aone kuwa wanapoambiwa maneno wafatilie. Mimi hicho ndicho ninachotaka Mheshimiwa. Hoja yangu kuwa naeleza kuwa lile jambo sikuridhika nalo nataka zile fedha zirejee serikalini ili kinunuliwe kitu chengine kipya. Halafu ile mashine haina *warrant* sasa hivi ni miezi 6 tangu ianze kuletwa kile chombo. Sasa ni kweli serikali bado iendelee ikanunuliwe kwa kuwa nini haikutoka tenda kwa muhusika na zile pesa za East Africa zimeletwa ndani serikali milioni kumi inatakiwa tayari utoe tenda, seuze milioni kumi na sita, *why*?

Sasa ningeomba Mheshimiwa hapo kidogo anisaidie ili niweze kupitisha kwa ulaini fungu lake. Mimi kichwa kinaniuma zile fedha Mhe. Mwenyekiti, sina

chengine. Zile fedha zirudi pale ili tuendelee Mheshimiwa kwa uhakika. Kwa sababu hawanikaidi nimefanya *research* nimelipa mimi mwenyewe nimetolewa damu nilitobolewa kwenye mwili kufanya uchunguzi huo na hatimae kile chombo nikaambiwa hapa hakuna.

Nikaenda kwengine sasa hawa wanyonge, mimi sawa lakini wengine je?

**Mhe. Mwenyekiti:** Hoja umemaliza Mheshimiwa. Mhe. Naibu Waziri maelezo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza kwa ruhusa yako namshukuru sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwa sababu atatupa fursa ya kutoa maelezo zaidi.

Katika hoja zake ametaja vitu vitatu, cha kwanza kabisa alitaja kuhusiana na hii mashine yenyewe. Naomba nimthibitishie kwamba hii mashine tunaijua na yeye anajua kwamba tunaijua rangi yake tunaifahamu na baada ya yeye kutuletea pia picha za hiyo mashine ametuletea yeye mwenyewe. Kwa hivyo, hatuwezi kukosa kujua rangi baada ya kufatilia. Na namshukuru kwamba amekuwa anafatilia hili suala kwa karibu sana.

Pili amezungumza kuhusu *socket;* hiyo *socket* sitaki kutoa taaluma kubwa ya masuala ya umeme, lakini hiyo *socket* inakaa humo humo ndani ya *power supplier unit* kitu chochote kinachotumia masuala ya umeme kinakuwa na *sockt* ndani na hiyo *socket* inakaa katika *power supplier Unit.*

Cha tatu kuna utaratibu ambao hao East African wenyewe wanatumia wakati wa manunuzi. Tatizo lililokuwepo hapa Mhe. Mwenyekiti, ambalo mimi naliona na baada ya kuzungumza na wahusika kulikuwa na ushindani wa kibiashara. Sasa hatutaki kwenda kwenye kutoa *detail* zaidi katika ushindani wa kibiashara. Lakini kulikuwa na ushindani wa kibiashara watu ambao wanashinda katika ku- *supply* ile mashine.

Sasa mimi nitamuomba Mheshimiwa atukubalie hapa ili sasa hivi nisende mimi pake yangu akasema labda rangi hatuijui au asende yeye peke yake akapewa vitu vyengine ili kukata mzizi wa fitina, kwa sababu mimi ninazo hizi nyaraka za hii mashine na *service* yake zote. Hapa mbele yetu Mheshimiwa, tuende pamoja mimi na yeye na kwa hao wahusika tukae pamoja tuzungumze pamoja na pale atapata *true vision of the issue.* Kwa sababu hivi inakuwa ni ushindani wa kibiashara pengine kampuni hii dio iloshinda hii haikushinda kwa nini imeshinda hii. Na hilo suala Mheshimiwa lipo na tumelipata huko huko katika idara hiyo hiyo.

Sasa wale waliopitisha wazo lile au waliopitisha uamuzi ule wa kuchagua kampuni hiyo walizingatia masharti yote. Kwa hiyo, naomba atukubalie hili halafu tukimaliza hapa twende tukae nae wahausika. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, mimi sikusoma lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi natambua. Mheshimiwa *wallah* nataka nikwambie tuwe wakweli Mwenyezi Mungu atulinde hiki kitu tunasema kweli tuwe wakweli Mwenyezi Mungu atulinde. Lakini nataka kukamwambia Mheshimiwa hii mashine haikupata taratibu, sasa nakwambia maana yake unataka lazima nimfufue paka kwenye gunia, namtoa paka kwenye gunia sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kipindi fulani mimi nilisema maswala ya zile mashine za *cancer* ushanifahamu Mhe. Mwenyekiti, nikaeleza hii nikabishiwa hapa Mhe. Makamu wa Pili akenda akaona hawakuleta jibu kama Makame Mshimba kasema ukweli au uongo na Mhe. Makamu wa Kwanza alikwenda hakusema kwenye vyombo vya habari Mhe. Makame Mshimba kasema uongo.

Mheshimiwa nakuhakikishia hii mimi niko tayari na kwa kuwa niko tayari serikali haishindwi kubuni kitu. Sasa wasi wasi wangu hapa Mhe. Mwenyekiti, hawa shindwi kwa sababu *document* hizo hakuna *issue document* ambazo hakika za fundi alizotoa kuwaambia wao Mhe. Mwenyekiti.

Sasa mimi ninachosema hivi nalia tena siku ya mwanzo aliposema alinitajia kampuni nyengine, *hansard* ipo. Lakini jana alikiri kama kweli ni *East African* yenyewe. Kiutaratibu hawa walifanya *property document* wenyewe ile *department* inaomba vitu wenyewe. Sasa ni sheria lazima zile fedha zitoke kwa mujibuwa tenda aliopewa kapewa pesa kama anakwenda kununua bizari dukani hakupewa kwa mujibu wa utaratibu Mhe. Mwenyekiti.
Sasa huyu ndio kenda katafuta wale watu ambao waliokuwa wenye mambo ya kutuletea vitu *fake*. Sasa mimi ninachoomba Mheshimiwa haina haja ya kwenda mimi na wewe nitazidi kukuadhirisiheni. Ninachotaka mimi ni nikuachieni lakini naomba sana serikali hizi fedha chini ya Makamu wa Pili hizi fedha zirejeshwe.

Mimi sawa Makamu wa Pili ana mkono mrefu mimi namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili ende akafanye *wallah* atakuja kunibeba mwenyewe humu ndani atanambia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk unasema  kweli. Naachia kifungu lakini nasema serikali lazima katika Bajeti ya Wizara ya Fedha wakati wa mwisho Mhe. Makamu wa Pili atawambia zile fedha zimerejeshwa.

Mimi ninachotaka fedha zirejeshwe Mheshimiwa, wamefanya sivyo nikienda itakuwa bure tu wamenidanganya watanileta kizungu na mimi kweli miwani sikuvaa si wameshanidanganya hapo. Sasa ukweli tuseme atanilietea masuala ya

*electricity,* masuala ya kila kitu mimi atanisumbua. Naomba Mheshimiwa tuendelee, lakini ninachosema kuwa lazima zile fedha zirejeshwe bila ya kutiana aibu sasa hivi. Tuendelee Mheshimiwa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kuna *comment* yoyote hapo.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti kwanza ieleweke na yeye Mhe. Mjumbe ajue kwamba hii mashine ilikuwa ni katika utaratibu wa Jumuiya ya Afrika Mashiriki na kuzisaidia maabara. Kwa hivyo, zimetoka kwa masharti mawili.

Kwanza zimekuja serikalini pia kuna chombo cha East African ambacho kinashughulikia hizo *document*. Kwa hivyo, hakuna udanganyifu uliofanyika kwa njia hiyo. Sasa kilichokea ni kwamba mashine iliharibika kwa muda mfupi kutokana na matatizo ya kiumeme na mashine ipo ndio maana akakataa kwenda kwa sababu ipo ile mashine. Tunamuomba kama yeye hana utaalamu basi akodi mtalaamu aje nae ndio atakapopata uthibitisho.

Lakini mashine ipo kilichoharibika ni *socket,* kama alivyosema ni *power supplier* na hiyo inashughulikiwa kuna mafundi maalum ambao wanashughulikia. Sasa pesa hizo zirejeshwe kutokana na njia gani na kuna kesi wala hakuna ripoti ya *CAG* ilionesha hivyo kwamba akaja kasema kwamba serikali ni *CAG* ndie anaeshughulikia hiyo.

Sasa vile anavyotaka yeye pesa irejeshwe ni mambo haya ya sokoni nirejeshee pesa zangu. Lakini katika serikali *document* ipo hamna habari hiyo. Sasa Mheshimiwa u- *judge* kutokana na ile *sequence* ya *argument* inavyokwenda. Wewe twende ukaone mlete mtaalamu wake akaone. Lakini yote anasema aah zirejeshwe pesa tu. Kwa hivyo, Mheshimiwa naona hoja yake ni dhaifu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kama nimefahamu vizuri ni kwamba kifaa kilikwisha nunuliwa pesa haiwezi kurejesheka ndio nilivyofahamu. Lakini nadhani kinachohitajika ni kujua kwamba je, hicho kifaa kitaweza kufanywaje ili kuweza kazi inayokusudiwa. Labda utusaidie hilo tupate kuendelea. Maelezo ya wizara maana madhumuni hapa ni kuwa kifaa kifanye kazi iliyokusudiwa.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, *documet* hii hapa ya mtiririko wa matengenezo. Mara ya mwisho fundi amekuja kwenye chombo tarehe 28/4/2015. Kitu kilichojaribiwa kinaitwa *the groom testing*, kitu kilichoonekana kina matatizo *not successful* kwa sababu *machine is hoping engineer concern required*, kaandika na saini yake hapa kaweka *engineer* aliyekuja kuitizama.

Kwa hivyo ndiyo tukamwambia kama yeye hana utaalamu, atafute mtaalamu aje aisome hii *document* ili aweze kuthibitisha. Hiki chombo kinashughulikiwa kwa sababu kwa nini, sisi hospitali tunakihitaji na kuwa na chombo chengine katika hospitali ile ile ndiyo dunia nzima wanavyofanya, lakini kuwe na *twin equipment* kwa ajili kikiwa kimoja hakipo tunakuwa na *backup*. Kwa hivyo kinaweza kikaharibika chombo, lakini kila kitakachoharibika ina maana ni feki tutavitupa vingi.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*).

**Mhe. Mwenyekiti:** Kwa hivyo kwa kifupi kimeshughulikiwa.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Ndiyo naam.

**Mhe. Mwenyekiti:** Haya. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk hebu maana yake tusije tukaondoka humu ikawa lile wazo ulilolitoa ikawa ndiyo kama uamuzi wa Baraza hapana. Majibu, ngoja tulia basi.

Majibu aliyotoa Waziri ni kwamba fedha haiwezi kurejesheka kwa sababu kifaa kilikwishakununuliwa, ila kimeleta matatizo na kazi ya kuvifanyia matengenezo, uchunguzi umeshafanywa *document* kaisoma na baada ya hapo wanaendelea na kuvishughulikia.

Anachosema kama wewe una wataalamu ambao watamudu kuviweka vizuri basi uwapeleke ili chombo hiki kitengenezwe, kwa sababu bado wanakihitaji. Sasa hapo wala hakuna ubishi, Wizara wanahitaji, wewe unahitaji ninaamini na Wajumbe wanahitaji.

Sasa kinashughulikiwa ila mtaalamu aliyekwenda kuchunguza katoa taarifa yake ile pale. Kama kuna mtaalamu mwengine atayekitengeneza kikafanya kazi vizuri unakaribishwa hata wewe upeleke. Ninadhani maelezo yapo wazi. Eeh! karibu.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, ninaheshimu sana kiti chako na mtu mmoja mtiifu sana, mtu laini sana. Na nilikuwa nimeshatoa njia Mheshimiwa kuweza kuachia kwa sababu ninavyojua kitu chochote kinakuwa *guarantee*, unaponunua mheshimiwa anaku-*guarantee* mtu kwa muda fulani chombo hichi halafu baadae kikiharibika ndani ya zile siku zenyewe ina maana unatakiwa yule *supplier* au yule mtu aliyeleta aweze kukitengeneza.

Lakini kwa maelezo ya Mhe. Waziri, mimi sina, ninakubaliana nayo mawazo yangu hayana tatizo lakini ukweli utajulikana mbele ya safari. Je, hichi kitu hakina

*warrant*. Mimi nina *warrant* hawana *document* hawa ya kusema kuonesha warrant. Sasa inakuwaje wao watafute fundi watengeneze, siyo warejeshe.

*It means* kuwa anasema kuwa yule mtu aliyeleta kile kitu ametuletea kitu kibovu. Kwa maana hiyo kile kitu kibovu waturejeshee pesa zetu au watupe kitu chengine. Ndiyo *concern* yangu niliyokusudia Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kile kitu kiwe na *limit* ninarejea tena mheshimiwa sitaki zogo. Ninasemaje tuendelee lakini ukweli utajulikana Mhe. Mwenyekiti, hakuna tatizo.(*Makofi*).

**Mhe. Mwenyekiti:** Haya wacha tuendelee. Mhe. Jaku Hashim Ayoub hoja ya tatu hii ni nyengine au ni ile ile.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, hii ni Wizara nyeti Wizara ya Afya, kila mtu anahitaji afya.

Katika mchango wangu jana nilisema kwamba umegawika sehemu tatu:-

1. Kukushukuru
2. Kuchangia Hoja
3. Kuomba

Hili ninafikiri dogo tu Mhe. Waziri ninafikiri halitompa shida, lakini nimuombe tu aliharakishe lisije likachukua siku tatu au nne, kuhusu Daktari Hamza Jambiani kurudishwa alikokuwepo. Huyu daktari kuna baadhi ya wafadhili wakasaidia misaada baada ya kutokuwepo, shida inanikuta mimi Mwakilishi na watu wengine.

Nimuombe Waziri hili dogo tu asije akafika alau siku tatu amrudishe haraka iwezekanavyo. Ninataka majibu Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri kuna maelezo kuhusu suala hilo.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza hapa siyo pahala pake. Sisi tunazungumza Hospitali ya Mnazi Mmoja na huyu daktari ni daktari wa vile vituo vya afya Idara ya Kinga ishapita. Kwa hivyo, ninafikiri sijui kama kachelewa au vipi.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.(*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe hebu twende kwa utaratibu. Hapa kwa kuwa eneo hilo tushapita, shirikiana na Wizara juu ya jambo hilo, shirikiana naye kwa sababu hatuwezi tukashika popote tu tena, tutaumizana namna hiyo. Ninadhani tuendelee, shirikiana na Wizara.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu P01 | Programu ndogo ya Huduma na Uchunguzi wa Matibabu | Sh. 669,743,000/= |
| Kifungu P02 | Programu ndogo ya Uongozi na Utawala | Sh.7,334,757,000/= |

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu jana nilizungumza suala hili kuhusu *calls* za madaktari, wamekuwa wakilalamika kwa muda mrefu na mazingira wanayofanya kazi, maslahi yao hawayapati kwa wakati.

Mhe. Waziri ninafikiri anajua, Mhe. Naibu Waziri anajua nilichangia sana sehemu hiyo kuhusu maslahi ya madaktari hawapati pamoja na kuwa ni haki yao.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, hili lilitolewa ufafanuzi lakini yeye bado yupo pale pale. Daktari anaozungumza ni madaktari wa hospitali nyengine ni Kifungu cha Idara ya Tiba, hii ni Idara ya Mnazi Mmoja ina *vote* yake, ina utaratibu wake wala wao siyo anaowadaiya, hawa wanapata fedha zao. Kwa hivyo alichelewa kidogo katika kusimama, kwa sababu alikuwa na mada nyingi na hakuweza kuwakabidhi wengine.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku unakusudia madaktari wa vijijini au Mnazi Mmoja.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mnazi Mmoja huko huko, ninachokisema mimi na anakijua Mhe.Waziri pamoja na hiki kitabu ni kigeni ndiyo mara yetu ya mwanzo kweli tunapata shida sisi wengine, lakini hao madaktari wapo Mnazi Mmoja na akataka nimletee ushahidi nitampa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hawa ni wa hapo hapo Mnazi Mmoja.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, kwa madaktari wa Mnazi Mmoja hakuna tatizo lolote, kwa sababu wao wana *vote* yao, wana utaratibu wao na si rahisi hata yeye kujua kwamba hawapati au wanapata.

**Mhe. Mwenyekiti:** Jaku Hashim Ayoub.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Na ahakikishe na atachukua hatua gani.

**Mhe. Mwenyekiti:** Samahani...

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Yupo tayari kumletea ushahidi na atachukua hatua gani kuhusu hayo ninayoyazungumza mimi kuwa kuna watu hawajapata *calls* zao.

**Mhe. Mwenyekiti:** Haya, sasa huo ushahidi uupeleke Wizarani ili waufanyie kazi. (*Makofi*)

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu P02 | Programu ndogo ya Uongozi na Utawala Hospitali | Sh.7,334,757,000/= |

**Jumla Kuu** **Sh.8,004,500,000/=**

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati bila ya Mabadiliko yoyote*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, ilivvyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya Mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubli Makadirio hayo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na Makadirio hayo wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. (Makofi).

**Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu:** Mhe. Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe ninakushukurani sana. Hoja zinazotolewa mbali mbali katika kupitisha Kasma za Matumizi tusizichukie ni sehemu ya demokrasia na kimsingi tunahitaji ufanisi. (*Makofi*)

Sasa wala tusione taabu kwamba huyu kauliza, yule kahoji ndiyo utaratibu wenyewe. Isitupe shida ila tu pale tunapofika kusema kwamba sasa hii imepita, nidhamu ifuatwe kwa sababu uamuzi umeshapita. (*Makofi*)

Mhe. Waziri ninakushukuru, ninawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote na watendaji ninawashukuru sana kwa kuwepo kwa kumsaidia Mhe. Waziri. (*Makofi*)

Sasa basi ninadhani tuendelee, Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa Fedha 2015/2016

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, kwanza naomba maelezo yangu yote nitakayotoa katika bajeti yangu yaingie kwenye hansard.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subuhana Wataalla* mwingi wa rehema kwa kutujaalia kwa mara nyengine kukutana hapa katika Baraza hili Tukufu tukiwa wazima na afya njema. Mhe. Spika, ninatoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu maelezo juu ya utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na mwelekeo wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, ninachukua nafasi hii adhimu kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake makini, mahiri, jasiri na uwajibikaji na dhamira ya dhati aliyonayo katika kuongoza na kusimamia maendeleo na kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Chini ya uongozi wake Zanzibar imeweza kupiga hatua kubwa katika nyanja mbali mbali za maendeleo ya kiuchumi na kijamii ikiwa ni pamoja na kuendeleza amani na utulivu. (*Makofi*)

Aidha, jitihada zake zimeweza kuinua hali na ustawi wa wanawake, vijana, watoto, wazee pamoja na wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Hapana shaka wananchi walio wengi wanaziona jitihada zake, uadilifu wake na uwezo wake mkubwa wa kupigiwa mfano na sote tumefarijika na juhudi zake katika kipindi chote tangu ameanza kushika dhamana ya kuiongoza Zanzibar. Hongera sana Mhe. Rais tunakutakia kila kheri, afya njema na maisha marefu wewe pamoja na familia yako. (*Makofi*)

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia maalum kuwapongeza Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharrif Hamad na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa namna wanavyomsaidia Mhe. Rais katika kuhakikisha ufanisi na uwajibikaji kwenye utendaji wa shughuli za Serikali, ili kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi. Nawapongeza wote kwa kazi zao nzuri.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe kwa kuendelea kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa hekima, busara na uadilifu mkubwa. Katika kuliendesha Baraza hili, umeweza kutimiza majukumu ya Baraza lako ya kutunga sheria, kupitisha bajeti na kuisimamia Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Spika**,** napenda kuipongeza Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii chini ya Uenyekiti wa Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mwakilishi wa Viti Maalum vya Wanawake kwa mashirikiano na miongozo waliyoitoa kwa Wizara yetu. Pia nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu, kwa mashirikiano waliyonipa wakati wote tukiwa katika Baraza hili. Nawapongeza sana na nawatakia kila la kheri, afya njema na maisha marefu.

Mhe. Spika, natoa pole kwa familia na wananchi wa Jimbo la Magomeni, Unguja kwa msiba wa Mhe. Salmin Awadh Salmin. Namuomba Mwenyezi Mungu aipe subra familia yake na aiweke roho ya marehemu mahala pema peponi, Amin.

Mhe. Spika, nawapa pole wananchi wote waliopata misiba na hasara wakati wa mvua kubwa zilizonyesha katika mwezi wa Mei mwaka huu hapa nchini. Namuomba Allah awape subira na ustahamilivu.

Mhe. Spika, napenda kuwakumbusha wananchi wenzangu kwamba ifikapo Oktoba mwaka 2015 tutakuwa na zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Taifa. Nawaomba tudumishe amani na utulivu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, sasa naomba nichukue fursa hii nitoe maelezo juu ya mapato, matumizi na utekelezaji wa malengo kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2014/2015, pamoja na mwelekeo, malengo na makadirio ya bajeti kwa mwaka 2015/2016.

## MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Spika, katika mwaka 2014/2015, Wizara ilipangiwa kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi Milioni Kumi (T. Shs. 10,000,000/=) kutokana na ada usajili na huduma za ukaguzi wa vyama vya ushirika. Hadi kufikia mwezi wa Mei 2015 mapato yaliyokusanywa ni Shilingi Milioni Sita, Laki Tano na Elfu Ishirini (T. Shs. 6,520,000/=), sawa na asilimia 65 ya makadirio kwa mwaka.

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara ilitengewa jumla ya Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Sita na Arobaini na Moja (T.Shs. 3,641,000,000/=) kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja Hamsini na Tano na Laki Mbili (T.Shs. 2,155,200,000/=) ni kwa ajili ya mishahara, michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na maposho maalum kwa wafanyakazi. Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Thamanini na Tano na Laki Nane (T.Shs. 1,485,800,000/= ) kwa matumizi mengineyo. Katika mwaka huo wa 2014/2015, jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nane Thamanini na Nne (T.Shs. 2,884,000,000/=) zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Ishirini na Nne (T.Shs. 1,524,000,000/=) ni mchango wa Serikali kwa miradi hiyo na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu na Sitini (T.Shs. 1,360,000,000/=) ziliahidiwa kutolewa na washirika wa Maendeleo kupitia miradi inayotekelezwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Mei 2015, Wizara imepata jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nane Tisini na Nne laki Nane elfu Thamanini Moja Mia Nne na Sabin na Tano kwa kazi za kawaida, ambapo kati ya hizo, Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tisa na Tisa, Laki Mbili Elfu Sabini na Sita na Mia Mbili (T.Shs. 1,909,276,200/=) ni kwa ajili ya mishahara na posho za wafanyakazi. Shilingi Milioni Mia Tisa Thamanini na Tano, Laki Sita na Elfu Tano, Mia Mbili Sabini na Tano (T.Shs. 985,605,275/=) ni fedha za matumizi mengineyo, sawa na asilimia Sitini na Sita (66%) ya fedha zilizotengwa kwa ajili hiyo. (Angalia Kiambatanisho Nam. 1).

Jumla ya fedha zilizopatikana kwa miradi ya maendeleo ni Milioni Mia Nane, Elfu Tisini na Moja, Mia Mbili Kumi na Saba (T. Shs. 800,091,217/=), kati ya hizo Shilingi Milioni Mia Tatu Hamsini (T. Shs. 350,000,000/=) zilitolewa na Serikali na Milioni Mia Nne Hamsini, Elfu Tisini na Moja, Mia Mbili Kumi na Saba (T. Shs. 450,091,217/=) kutoka kwa washirika wa maendeleo, sawa na asilimia ishirini na nane (28%) ya makadirio kwa mwaka 2014/2015.

**UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2014/2015**

Mhe. Spika, Wizara kwa kipindi cha 2014/2015 ilijipangia kutekeleza malengo makuu yafuatayo:

1. Kuimarisha hali za kiuchumi za vijana, wanawake, watoto, wazee, makundi yanayoishi katika mazingira magumu na jamii kwa ujumla;
2. Kuhakikisha kuwa mapungufu ya Sera na Sheria katika masuala ya uwezeshaji na yanayohusu watoto, wanawake, vijana, wazee na makundi anayoishi katika mazingira magumu yanafanyiwa kazi;

3. Kuimarisha ubora wa huduma na upatikanaji wa hifadhi ya jamii kwa watoto, wanawake, vijana` wazee na makundi yanayoishi katika mazingira magumu zaidi;
4. Kuhakikisha kuwa taarifa zinazohusu masuala ya wanawake,vijana,watoto, wazee, hifadhi ya jamii na uwezeshaji wananchi kiuchumi zinakusanywa na kutumiwa katika kuandaa na kuimarisha Sera, Mikakati na Programu;
5. Kukuza uelewa wa jamii juu ya dhana, misingi na kanuni za ushirika; na
6. Kuimarisha uwezo wa Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mhe. Spika, Utekelezaji wa malengo hayo kwa kila Idara ni kama ifuatavyo:-

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI:**

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Idara hii ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kusimamia uingizaji wa masuala mtambuka, ikiwemo masuala ya jinsia katika Sera, Mipango, Program na Bajeti za Wizara;
2. Kusimamia uandaaji wa utafiti wa kuangalia athari za utalii na mmomonyoko wa maadili kwa vijana;
3. Kusimamia uandaaji wa Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii, Sera ya Watoto, Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Sera ya Maendeleo ya Vijana;
4. Kuimarisha uandaaji, uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya mipango na programu za Wizara;
5. Kuimarisha mashirikiano ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuleta maendeleo na ustawi wa wanawake, vijana, wazee, watoto na wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi; na
6. Kuratibu utekelezaji wa programu na miradi inayosimamiwa na Wizara.

**Utekelezaji wa malengo ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka 2014/2015:**

Mhe. Spika, Wizara imekamilisha rasimu ya Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na ipo katika mchakato wa kuidhinishwa. Aidha, Wizara inaendelea na mapitio ya Sera ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mtoto ili iendane na mahitaji yaliyopo. Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Ushirika umekamilika. *UNICEF* na *HelpAge International* wako tayari kutusaidia katika kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii.

Mhe. Spika, Wizara imewapatia mafunzo watendaji 70 (35 Unguja na 35 Pemba) kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufuatiliaji na tathmini. Aidha, jumla ya wafanyakazi 35 wa Ofisi ya Pemba wamepatiwa mafunzo juu ya uandishi na uendeshaji wa miradi.

**Utekelezaji wa Programu zinazosimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti**

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2014/2015 Wizara imekuwa ikisimamia utekelezaji wa Programu mbili zifuatazo:

**Programu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake**

Mhe. Spika, Program hii inatekelezwa kwa mashirikiano na Shirika la *UN WOMEN* kwa lengo la kusaidia jitahada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake kiuchumi, kisiasa na kijamii. Katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia programu hii imetekeleza yafuatayo:

- Imezindua Kampeni ya miaka miwili ya kupiga vita vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia tarehe 6/12/2014. Kampeni hiyo iliyozinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein ina malengo makuu yafuatayo:

    1. Kukuza uelewa wa jamii juu ya suala la ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto;
    2. Kuimarisha uwajibikaji kwenye ngazi mbali mbali katika kukabiliana na aina zote za ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto;
    3. Kuimarisha uwezo wa taasisi na jamii katika kukabiliana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto; na
    4. Kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za kupambana na ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

  Utekelezaji wa kampeni hiyo unaendelea.

- Wizara imeandaa ripoti juu ya mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa Maazimio ya Beijing kwa kipindi cha miaka 20 (1995 – 2015). Ripoti hiyo imebainisha vipaumbele vya baadae katika kukuza usawa wa kijinsia na kumwezesha mwanamke.

- Imetoa mafunzo kwa viongozi wanawake kutoka katika taasisi za Serikali, ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa kujiamini. Jumla ya watendaji wanawake sabini (70), Unguja 35 na Pemba 35, wakiwemo Wakuu wa Wilaya, Makamishna na Wakurugenzi walishiriki katika mafunzo hayo.

- Imefanya zoezi la kuvitambua vikundi vya wanawake vya kiuchumi Unguja na Pemba. Jumla ya vikundi 1,560 (Pemba 642 na Unguja 918) vimetambuliwa. Taarifa hizi zitasaidia Wizara kuweza kubuni mipango ya kuviimarisha na kuvijengea uwezo zaidi vikundi vya wanawake.

- Imetoa mafunzo kwa wajumbe wa Kikundi Kazi cha Kuratibu Masuala ya Kijinsia, ili waweze kusimamia majukumu yao vizuri.

**Programu ya Jinsia Zanzibar**

Mhe. Spika, Programu hii inatekelezwa kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu (*UNFPA*).

Mhe. Spika, katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia program hii imetekeleza yafuatayo:

- Imetoa mafunzo kwa viongozi wa dini 84 Unguja na Pemba juu ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto, kwa kutumia miongozo maalum iliyoandaliwa. Viongozi hao hivi sasa wameanza kuelimisha waumini wao kupitia mihadhara ya kidini katika maeneo mbali mbali.

- Ilifanya mikutano minne ya Kamati ya Mawaziri kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa kesi za udhalilishaji wa kijinsia. Mikutano hiyo ilijadili changamoto mbali mbali zinazopelekea ucheleweshwaji wa hukumu za kesi za udhalilishaji wa kijinsia. Pia, ilipokea taarifa ya utekelezaji wa maagizo mbali mbali yaliyotolewa.

- Imeandaa na kurusha hewani vipindi 32 vya mchezo wa redio unaojulikana kama "Mshike Mshike", kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto, athari za ndoa za mapema, afya ya uzazi na mimba za umri mdogo. Mchezo huo umerushwa kupitia *ZBC* Redio na Redio Jamii za Mtegani, Tumbatu na Micheweni.

- Imetoa mafunzo juu ya kupambana na udhalilishaji wa kijinsia kwa wajumbe 150 (100 Unguja na 50 Pemba) kutoka kamati 14 za Shehia (10 Unguja na 4 Pemba) katika Wilaya za Kati, Kusini na Magharibi kwa Unguja na Wilaya za Mkoani na Chake kwa Pemba.

**IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI**

Mhe. Spika, katika mwaka 2014/15, Idara hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kusimamia shughuli za kila siku za Uendeshaji na Utumishi za Wizara, ikiwemo Sheria na Kanuni za utumishi Serikalini na kuhakikisha wafanyakazi wanafuata Sheria na Kanuni za usimamizi wa fedha na manunuzi ya vifaa vya ofisi;
2. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Wizara kwa kuwasaidia malipo ya ada ya masomo ya muda mrefu na muda mfupi kwa kuzingatia mahitaji ya Wizara;
3. Kuimarisha utendaji kazi na kusimamia ununuzi wa vifaa muhimu vya kutendea kazi;

4. Kuajiri wafanyakazi wapya 17 (Unguja 15 na Pemba 2); na
5. Kuendelea kuviimarisha vitengo vya Manunuzi, Uhasibu na Ukaguzi wa ndani.

**Utekelezaji wa malengo ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa mwaka 2014/15**

Mhe. Spika, Katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli za kila siku za Wizara, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeshughulikia upatikanaji wa vifaa mbali mbali vya ofisi na huduma muhimu, ikiwemo mawasiliano na usafiri. Aidha, imesimamia matengenezo ya vyombo vya usafiri na vifaa vyengine vya Ofisi, pamoja na majukumu mengine muhimu yanayohusu uendeshaji wa Ofisi Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Jumla ya wafanyakazi wapya 17, Unguja 15 na Pemba wawili (2), wameajiriwa katika mwaka 2014/2015, ambapo kati ya hao 10 ni wanaume na 7 ni wanawake. Nafasi hizo zilizojazwa ni za fani za Ushirika,

Utafiti, Utumishi, Ualimu wa Watu wenye Ulemavu, Ukatibu Muhtasi, Udereva, Uhudumu na Ulezi wa Watoto.

Mhe. Spika, Katika kuimarisha uwezo wa utendaji, Wizara imewapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 9, Unguja 6 na Pemba watatu (3). Aidha, imewalipia

ada ya masomo ya muda mrefu wafanyakazi 12, Unguja 10 na Pemba wawili (2), wanaosomea fani za Ushirika, Maendeleo ya Jamii, Uchumi, Uhasibu, Utunzaji Kumbukumbu, Ukatibu Muhtasi, Ustawi wa Jamii, Uendelezaji wa Miradi na Utawala na Uendeshaji kwenye vyuo mbali mbali vya Tanzania.

Mhe. Spika, Wizara, imerusha hewani jumla ya habari 40 za matukio mbali mbali, imetayarisha vipindi 14 na makala 8 zinazohusu masuala mbali mbali yanayosimamiwa na Wizara, ikiwemo kushajiisha jamii kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Spika, Wizara imefanya vikao 11 vya Kamati Tendaji na vikao vitatu (3) vya Kamati ya Uongozi. Vikao hivyo, pamoja na mambo mengine vilijadili Rasimu ya Sera ya Uwezeshaji, Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Ushirika, Mikakati ya Utunishaji wa Mfuko wa Uwezeshaji, Mpango wa Utekelezaji wa Kampeni ya Udhalilishaji wa Kijinsia, Kanuni za Baraza la Vijana na taarifa za utekelezaji wa programu na masuala mengine mbali mbali yanayosimamiwa na Wizara.

Mhe. Spika, Bodi ya Zabuni imefanya vikao sita (6) ambavyo vilijadili taarifa zinazohusu ununuzi pamoja na kuidhinisha zabuni mbali mbali.

Mhe. Spika, Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu imefanya vikao vinne (4), ambavyo pamoja na mambo mengine vilijadili Ripoti za Ukaguzi zilizowasilishwa. Aidha, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kimefanya ukaguzi wa mahesabu na matumizi ya Wizara katika Idara, Miradi na Programu zake mbali mbali Unguja na Pemba.

**IDARA YA UENDELEZAJI NA URATIBU WA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2014/2015 Idara hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuandaa mafunzo ya ujasiriamali katika maeneo tofauti kwa vijana, wahitimu wa vyuo na vikundi vya kiuchumi;
2. Kuanzisha Mtandao wa Wajasiriamali utakaohusisha taasisi zinazotoa huduma za kifedha na huduma za biashara;
3. Kukuza mashirikiano na taasisi nyengine zinazohusika ili kuhakikisha upatikanaji wa masoko kwa bidhaa za wajasiriamali;
4. Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
5. Kukamilisha uanzishaji wa Kituo cha Kukuza Wajasiriamali *(Incubation center)* Unguja; na

6. Kutoa huduma za kibiashara kwa wajasiriamali wadogo wadogo kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

**Utekelezaji wa malengo ya Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka 2014/15**

Mhe. Spika, Utekelezaji wa malengo kwa Idara hii ulikuwa kama fuatavyo:

- Jumla ya vijana 71 (Unguja 50 na Pemba 21) walipatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kujiajiri katika shughuli za ujasiriamali.
- Wanavikundi 70 (Unguja 50 na Pemba 20) kutoka vikundi 9 vya kiuchumi vya Mkoa wa Kusini Unguja na vitano (5) vya Mkoa wa Kaskazini Pemba wamepatiwa mafunzo ya kuwasaidia kuimarisha shughuli zao. Vikundi hivyo vimebadilika kimtazamo na vimeweza kuongeza ubora wa bidhaa wanazozalisha. Aidha, wamekuwa na ujuzi wa kubuni bidhaa mpya kulingana na mahitaji ya wateja.
- Jumla ya wajasiriamali wadogo wadogo 38, kati yao 32 wanawake na 6 wanaume, wamewezeshwa kushiriki katika maonesho ya JUAKALI yaliyofanyika nchini Rwanda.
- Ili kuimarisha uratibu wa programu za uwezeshaji, Wizara iliandaa mkutano ulioshirikisha Taasisi za Serikali zinazohusika na masuala haya. Mkutano huo ulilenga kujadili mafanikio na changamoto katika kutekeleza programu za uwezeshaji, ambapo ulifikia makubaliano juu ya haja ya kuimarisha mashirikiano katika kuzitatua changamoto zinazowakabili wajasiriamali. Aidha, Wizara imefanya mkutano wa Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, ambao pamoja na mambo mengine, ulipokea na kujadili taarifa zilizowasilishwa za utekelezaji wa programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

- Katika juhudi za kuwawezesha wananchi kiuchumi, Wizara imeanzisha Kituo cha Kukuza Wajasiriamali Mbweni, Unguja. Kituo hicho tayari kimeanza kazi, kikiwa na jumla ya wajasiriamali 385.

- Wizara kwa kushirikiana na *COSTECH* na Chuo cha Karume cha Sayansi na Teknolojia Mbweni, imetengeneza mashine za gharama nafuu kwa ajili ya kukaushia mwani, matunda na dagaa kwa kutumia nguvu za jua. Mashine hizo hivi sasa zipo katika majaribio kwenye Kituo cha Kukuza

Wajasiriamali na tayari wajasiriamali waliopo kituoni hapo wameshaanza kuzitumia kwa kukaushia dagaa na matunda.

- Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Huduma za kujitolea (*Voluntary Services Overseas*) na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania imenunua jumla ya vihori/boti 100 za kubebea mwani baharini

  kwa ajili ya kuwapatia wakulima wa mwani Unguja na Pemba. Vihori/boti hizo zimetolewa kwa wakulima wa mwani kwa njia ya mkopo nafuu, ambapo kati yao 70 zimetolewa Pemba na 30 Unguja. Vihori hivyo vina uwezo wa kubeba kilo 400 za mwani mbichi kwa mara moja.

- Wizara kwa mashirikiano na Chuo cha Barefoot kilichopo Tilonia nchini India, imekamilisha ukarabati wa jengo kwa ajili ya uanzishaji wa Kituo cha kuwafunza wanawake utengenezaji wa vifaa vya umeme wa jua. Kituo hicho kilichopo Kibokwa, Mkoa wa Kaskazini Unguja kinatarajiwa kuzinduliwa rasmi mwezi wa Julai 2015.

**IDARA YA MIKOPO**

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2014/2015, Idara ya Mikopo ilipanga utekeleza malengo yafuatayo:

1. Kutoa mikopo 1,000 yenye thamani ya Shilingi 500,000,000/= kwa vikundi vya kiuchumi na wajasiriamali mmoja mmoja katika sekta zote za kiuchumi;
2. Kuongeza kiwango cha marejesho ya mikopo kutoka asilimia 85 hadi zaidi ya asilimia 95;
3. Kuanzisha fursa mpya za mikopo na kutangaza kanuni mpya zinazoendesha Mfuko huu;
4. Kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu za wateja wa mikopo;
5. Kuendelea na juhudi mbali mbali za kutafuta fedha ili Mfuko uendelee kuwasaidia wajasiriamali wengi zaidi;
6. Kuimarisha mashirikiano na uratibu wa shughuli za mikopo nafuu hapa nchini; na
7. Kuimarisha uwezo wa watendaji ili kuongeza ufanisi wa kazi.

**Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Mikopo kwa mwaka 2014/2015**

Mhe. Spika, Wizara kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, imetoa jumla ya mikopo 531 (Unguja 369 na Pemba 162) yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Nane Sabini na Tisa, Laki Tatu Elfu Arobaini na Mbili (T. Shs. 879,342,000/=). Kati ya hizo, Unguja zilitolewa Shilingi Milioni Mia Sita Kumi na Saba, Laki Sita na Elfu Tisini na Mbili (T. Shs. 617,692,000/=) na Pemba Shilingi Milioni Mia Mbili Sitini na Moja, Laki Sita na Elfu Hamsini (T. Shs. 261,650,000/=). Mikopo hiyo imenufaisha wananchi 9,236 (wanawake 4,951 na wanaume 4,285) katika Shehia 310 za Unguja na Pemba. (Angalia Kiambatanisho Nam. 2).

Mhe. Spika, Wizara imeweka dhamana ya fedha (Guarantee Fund) ya Shilingi Milioni Mia na Hamsini (T. Shs. 150,000,000/=) katika Benki ya CRDB, ili itoe mikopo kwa vijana kupitia *SACCOS* zao Unguja na Pemba. Hadi kufikia mwezi wa Mei 2015, *CRDB* imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Nne (T.Shs. 400,000,000/=) kwa vikundi 142 vyenye jumla ya wanachama 710, kupitia *SACCOS* ya Vijana ya Unguja na Shilingi Milioni Thalathini (T. Shs. 30,000,000/=) kwa vijana 60 (wanaume 23 na wanawake 37) kupitia *SACCOS* ya Vijana ya Pemba.

Mhe. Spika, Wizara imetoa mafunzo kwa jumla ya wakopaji 734 kuhusiana na uwekaji wa kumbukumbu za hesabu; umuhimu wa kutumia huduma za benki na kujiwekea akiba; na utafutaji wa masoko, ili waweze kusimamia vizuri biashara zao na hatimae waweze kurejesha mikopo waliyochukua.

Mhe. Spika, Wizara imefanya ziara za kufuatilia marejesho ya mikopo katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Pia, imefanya mikutano na uongozi wa Serikali kwenye ngazi za Wilaya na Shehia kuwaelewesha madhumuni ya Mfuko, kanuni zake, pamoja na kuhimiza urejeshwaji wa fedha za mkopo. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2015, jumla ya Shilingi Milioni Mia Tatu Sitini na Mbili, Laki Sita Elfu Arubaini na Saba na Tano (T.Shs. 362,647,005/=) ya fedha za mkopo zimerejeshwa Unguja na Pemba. Kati ya hizo, Unguja zimerejeshwa Shilingi Milioni Mia Mbili Sitini na Tisa, Laki Nane Elfu Sitini na Tisa na Tano (T Shs. 269,869,005/=) na Pemba Shilingi Milioni Tisini na Mbili, Laki Saba Elfu Sabini na Nane (T. Shs. 92,778,000/=) kama inavyoonekana katika

Kiambatanisho Nam. 3. Aidha, Wizara imekusanya jumla ya Shilingi Milioni Thalathini na Nne, Laki Mbili Elfu Tano, Mia Moja na Tisini na Tano (T. Shs. 34,205,195/=) kutoka kwa wakopaji wa uliokuwa Mfuko wa AK/JK. (Angalia Kiambatanisho Nam. 4).

Mhe. Spika, Wizara imewekeza katika Benki ya Watu wa Zanzibar jumla ya Shilingi Milioni Mia Nane (T. Shs. 800,000,000/=) kutoka Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Faida itakayopatikana katika uwekezaji huo itakwenda katika kutunisha Mfuko wa mikopo, ili wananchi wengi zaidi waweze kufaidika.

Mhe. Spika, Muongozo mpya wa utoaji mikopo, hususan kipengele kinachowataka wanaohitaji mikopo kuanzisha vikundi na kufungua Akaunti benki, umeshajiisha sana wananchi kujenga tabia ya kujiwekea akiba. Tangu utaratibu huu ulipoanza mwaka 2014, jumla ya Shilingi Milioni Sitini na Tano na Laki Saba (T. Shs. 65,700,000/=) zimewekwa akiba katika Akaunti za wateja wa mikopo.

**IDARA YA USHIRIKA**

Mhe. Spika, Idara ya Ushirika katika kipindi cha mwaka 2014/2015 ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kukuza uwezo wa ushindani wa vyama vya ushirika kumi (10) ili vitoe huduma kwenye soko la utalii ifikapo Juni 2015;
2. Kuongeza uwelewa kwa wanachama na viongozi 3,000 juu ya maadili, kanuni za ushirika na mbinu za utendaji bora kwenye vyama vya ushirika ifikapo Juni 2015;
3. Kusimamia utekelezaji wa Sheria katika uendeshaji wa vyama vya ushirika 1,400 ifikapo Juni 2015;
4. Kuimarisha mashirikiano na washirika ili kubadilishana taarifa na kujifunza mambo mapya ya kuendeleza sekta ya ushirika ifikapo Juni 2015;
5. Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya maendeleo ya vyama vya ushirika ifikapo Juni 2015; na
6. Kuimarisha mazingira ya kazi, ikiwemo mafunzo kwa wafanyakazi na upatikanaji wa vifaa.

**Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Ushirika kwa mwaka 2014/2015**

Mhe. Spika, Wizara imetoa mafunzo juu ya utunzaji wa kumbukumbu za hesabu na mbinu za uongozi kwa viongozi na wanachama 3,004 (wanawake 2,073 na wanaume 931) kutoka vyama vya ushirika 468 (Unguja 336 na Pemba 132). Lengo la mafunzo hayo ni kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa vyama hivyo, ili viweze kukidhi mahitaji ya wanachama wake.

Mhe. Spika, Jumla ya wanachama 2,208 (wanawake 1,524 na wanaume 684) kutoka vyama 163 (Unguja 143 na

Pemba 20) wamepatiwa mafunzo juu ya haki na wajibu wa wanachama katika kuendeleza vyama vya ushirika.

Mhe. Spika, Wizara kwa mashirikiano na Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani wa Mazao ya Kilimo na Huduma za Fedha Vijijini, imewapatia mafunzo ya uongozi na uendeshaji wa *SACCOS* maafisa 15 wa Idara ya Ushirika na 10 kutoka taasisi binafsi zinazotoa huduma kwenye vyama vya ushirika.

Mhe. Spika, Wizara imefanya ukaguzi wa kawaida na kutoa mafunzo ya vitendo kwa vyama vya ushirika 773 (Unguja 439 na Pemba 334). Lengo ni kuhakikisha kuwa vyama vinaendeshwa kwa mujibu wa Sheria na Katiba za vyama husika. Aidha, Wizara imeandaa Vitini na Miongozo kwa ajili ya kutoa mafunzo kwenye vyama vya ushirika.

Mhe. Spika, Vyama vya ushirika 209 (Unguja 179 na Pemba 30) vimefanyiwa ukaguzi wa hesabu. Kati ya vyama hivyo vilivyokaguliwa, 80 ni *SACCOS* na 129 ni vyama vya uzalishaji mali na utoaji huduma.

Mhe. Spika, Wizara kwa mashirikiano na Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji wa Thamani ya Mazao ya Kilimo na Huduma za Fedha Vijijini imewapatia mafunzo, Maafisa 11 wa Idara ya Ushirika na 18 kutoka taasisi binafsi wanaotoa huduma za ukaguzi wa hesabu. Mafunzo hayo yataongeza utoaji wa huduma za ukaguzi wa hesabu katika vyama vya ushirika.

Mhe. Spika, Wizara imesajili vyama vipya 249 (Unguja 168 na Pemba 81). Hii inafanya idadi ya vyama vya ushirika kufikia 2,772.

Mhe. Spika, Wizara imeadhimisha Siku ya Ushirika Duniani tarehe 5 Julai 2014. Kauli mbiu ya Maadhimisho hayo ni "Ushirika endelevu wenye tija kwa wote".

**IDARA YA USTAWI WA JAMII**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Ustawi wa Jamii ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha mfumo wa Hifadhi ya mtoto;
2. Kuratibu na kufuatilia masuala ya malezi na makuzi ya watoto;
3. Kuimarisha hifadhi ya wazee;
4. Kuendeleza utowaji wa misaada ya kiustawi kwa wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi;
5. Kuimarisha mfumo wa hifadhi ya jamii; na
6. Kusimamia ulipwaji wa fidia kwa wafanyakazi waliopatwa na ajali kazini.

**Utekelezaji wa malengo ya Idara ya Ustawi wa Jamii kwa kipindi cha 2014/2015**

Mhe. Spika, Kamati nane (8) za kuwahudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi katika Wilaya za Kaskazini "A" na "B" zimepatiwa mafunzo ya hifadhi ya mtoto. Mafunzo hayo yalilenga kuengeza uelewa na ufanisi kwa watendaji wa kamati hizo.

Mhe. Spika, Jumla ya malalamiko 132 (Unguja 50 na Pemba 82) ya watoto waliofanyiwa ukatili na udhalilishaji yaliripotiwa katika Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto cha Idara ya Ustawi wa Jamii. Kati ya hayo malalamiko 80 yalihusu kubakwa, 14 kulawitiwa, 15 kukashifiwa na 23 kutoroshwa. Walalamikaji walisaidiwa kuwasilisha malalamiko hayo katika vyombo vya Sheria.

Mhe. Spika, Wizara imepokea na kushughulikia malalamiko 140 (95 Unguja na 45 Pemba) yanayohusu malezi ya watoto, kati ya hayo, 92 ni ya matunzo na 48 ni ya mvutano wa malezi. Wimbi hili kubwa la utelekezwaji wa watoto linasababishwa na kuvunjika kwa ndoa na pia tabia ya baadhi ya akina baba kushindwa kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika,Wizara imetoa mafunzo juu ya hifadhi ya mtoto kwa wasimamizi wa vituo 10 vya kulelea watoto vilivyopo Zanzibar, vikiwemo vituo vya Serikali na vya watu binafsi. Aidha, Wizara imefanya zoezi la kuvitambua

vituo vya kulelea watoto na kusimamia utekelezaji wake. Jumla ya vituo 11, Unguja vinane (8) na Pemba vitatu (3) vimetambuliwa. (Angalia Kiambatanisho Nam. 5).

Mhe. Spika, Wizara imeendelea kuhudumia nyumba ya kulelea watoto Mazizini ambapo jumla ya watoto 30 wanaolelewa katika kituo hicho wanaendelea kupatiwa huduma za malezi.

Mhe. Spika, Wizara imetoa misaada ya kijamii kwa familia 156 (93 Unguja na 63 Pemba) zenye watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi, wakiwemo mama waliozaa mapacha watatu. Aidha, Wizara inaendelea kuwahudumia jumla ya wazee 91 (Sebleni 46, Welezo 37, Limbani 8 na 57 wanaoishi Makundeni) wanaoishi katika nyumba za wazee.

Mhe. Spika, Kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto itaanza kutoa pensheni jamii kwa wazee wote. Mhe. Spika, naomba nirudie tena hapa. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto itaanza kutoa pensheni

jamii kwa wazee wote, wenye umri wa kuanzia miaka 70 Unguja na Pemba. Hatua hii inachangia juhudi za Serikali katika mpango wake wa kupunguza umasikini kwa wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Wizara imeratibu maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani tarehe 1 Oktoba. Ujumbe wa mwaka huu ulikuwa "Wazee Wasiachwe Nyuma, Tujenge Jamii Shirikishi, Tupitishe Sheria yao".

Mhe. Spika, Wizara ilitoa mafunzo ya siku moja juu ya Sera ya Hifadhi ya Jamii kwa Wenyeviti wa Kamati za Baraza la Wawakilishi pamoja na wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, Wizara imepokea madai 24 (Unguja 11 na Pemba 13) ya fidia kwa wafanyakazi waliopatwa na ajali wakiwa kazini. Jumla ya madai 23 (Unguja 11 na Pemba 12) yameshalipwa. Madai yaliyobaki yanafanyiwa kazi. Aidha, Wizara ilizika maiti kumi na tisa (19) zisizokuwa na wenyewe.

**IDARA YA MAENDELEO YA VIJANA**

Mhe. Spika, Idara ya Maendeleo ya Vijana katika mwaka 2014/2015 ilijipangia kutekeleza majukumu yafuatayo:

1. Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana;
2. Kuratibu na kufuatilia uanzishwaji wa Baraza la Vijana;
3. Kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana Kitaifa;
4. Kuwahamasisha, kuwaandaa na kuwaunganisha Vijana na fursa mbali mbali za kiuchumi zilizopo;
5. Kuratibu utekelezaji wa kitini na muongozo wa stadi za maisha kwa Vijana walio nje ya skuli; na
6. Kufanya ufuatiliaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii za Vijana; na kuimarisha ushirikiano na taasisi zinazoshughulikia masuala ya Vijana ndani na nje ya nchi.

**Utekelezaji wa malengo ya Idara ya Maendeleo ya Vijana kwa mwaka 2014/2015**

Mhe. Spika, Wizara imepiga hatua katika uandaaji wa Baraza la Vijana. Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameshamteua Katibu Mtendaji wa Baraza hilo. Aidha, kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Baraza la Vijana la Zanzibar tayari zimeshaandaliwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu ili kutangazwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali. Kazi ya kuhamasisha vijana kujiunga na mabaraza katika ngazi za Shehia inaendelea Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliratibu kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2014 kilichofanyika Mkoani Tabora. Pia, ilishiriki katika uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2015 uliofanyika Mkoani Ruvuma tarehe 29/04/2015, ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein. Ujumbe wa Mbio za Mwenge kwa mwaka 2015 ni "Tumia Haki yako ya Kidemokrasia: Jiandikishe na Kupiga Kura katika Uchaguzi wa mwaka 2015".

Mhe. Spika, Wizara imehamasisha vikundi vya vijana na kuwaunganisha na fursa mbali mbali, ili kuimarisha shughuli zao za uzalishaji mali. Jumla ya Vijana 81 Pemba wamepatiwa mikopo ya kuwasaidia kuendesha miradi yao na jumuiya 13 za Vijana zimepatiwa mafunzo ya uandishi wa miradi.

Mhe. Spika, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi za Vijana imetoa mafunzo ya stadi za maisha kwa taasisi za vijana Unguja na Pemba. Jumla ya vijana 72 (Unguja 36 na Pemba 36) kutoka taasisi 36 (Unguja 18 na Pemba 18) wamepatiwa mafunzo hayo. Kati ya vijana hao, 33 ni wanawake na 39 ni wanaume.

Mhe. Spika, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Mipango, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma, Shirika la Kimataifa la Huduma za Kujitolea (*VSO*) na Shell International, iliratibu uandaaji wa Tamasha la Vijana na Ajira Unguja na Pemba. Jumla ya vijana 1,900 (Unguja 1,200 na Pemba 700) na taasisi za ajira 45 (Unguja 30 na Pemba 15) zilishiriki katika matamasha hayo.

**IDARA YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA WATOTO**

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kukuza uwezo wa Idara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;
2. Kuratibu na kusimamia haki za Wanawake na Watoto;
3. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mabaraza ya Watoto;
4. Kuimarisha uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za kiuchumi, kijamii na maendeleo ya Wanawake na Watoto;
5. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera na Sheria ya mtoto; na
6. Kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa mambo yanayohusu Wanawake na Watoto.

**Utekelezaji wa malengo ya Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto kwa mwaka 2014/2015**

Mhe. Spika, Wizara imetoa mafunzo kwa waratibu wa shughuli za wanawake na watoto wa Shehia 227 (123 Unguja na 104 Pemba), ili kuimarisha utendaji wa shughuli zake kuanzia ngazi ya Shehia. Mafunzo hayo yalihusu haki na wajibu wa mtoto, Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya mwaka 2011 na mbinu za kujikinga na kuchukua hatua dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Spika,Wizara imetoa mafunzo ya siku mbili (2) kwa watendaji 20 wa Idara, wakiwemo Maafisa Wanawake na Watoto wa Mikoa na Wilaya, juu ya uwezeshaji wanawake kiuchumi na kuleta maendeleo. Pia, Wizara imefanya vikao viwili vya robo mwaka vya kutathmini utekelezaji wa shughuli zake katika ngazi za Wilaya na Shehia Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Wizara imeendelea kupokea na kuyafanyia kazi malalamiko ya wanawake yanayoletwa. Kwa mwaka 2014/2015 jumla ya malalamiko 88 (40 Unguja na 48 Pemba) yalipokelewa na kupatiwa ushauri na maelekezo yanayofaa. (Angalia kiambatanisho Nam. 6(a) na (b).

Mhe. Spika, Wizara ilitoa mafunzo kwa Mabaraza ya wazazi ya Shehia juu ya malezi bora ya watoto na namna ya kuripoti matukio ya udhalilishaji. Jumla ya wazazi 64 (37 Unguja na 27 Pemba) kutoka Mabaraza ya Wazazi ya Shehia za Kizimkazi Unguja na Kichungwani Pemba walifaidika na mafunzo hayo.

Mhe. Spika,Wizara iliratibu maandalizi ya Siku ya Wanawake Duniani, yaliyofanyika Nungwi Unguja tarehe 08 Machi. Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo alikuwa Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi. Kauli mbiuya mwaka 2015 ilikuwa ni "Timiza Ahadi; Chukua Hatua Madhubuti Katika Kunyanyua Hali za Wanawake".

Mhe. Spika, Wizara imeendelea kuanzisha Mabaraza ya Watoto, ambapo jumla ya Mabaraza 43 (40 Unguja na 3 Pemba) yalianzishwa. Jumla ya Mabaraza 269 (Unguja 188 na Pemba 81) yamekamilika. Aidha, jumla ya viongozi 78 (30 Unguja na 48 Pemba) wa Mabaraza ya Watoto ya Wilaya ya Mjini, Magharibi na Kaskazini "A" Unguja na Mkoani Pemba wamepatiwa mafunzo juu ya Haki za Mtoto na Ushauri nasaha.

Mhe. Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria imezindua rasmi Mkakati wa Mageuzi ya Mfumo wa Sheria kwa Watoto. Aidha, jumla ya nakala 450 za Mkakati huo zimechapishwa na kusambazwa kwa taasisi mbali mbali.

**OFISI KUU PEMBA**

Mhe. Spika, Ofisi kuu Pemba inasimamia shughuli zote za Wizara na kutekeleza malengo ya Idara zote yaliyopangwa kwa upande wa Pemba. Hivyo, utekelezaji wa majukumu na malengo kwa mwaka 2014/15 ni kama ambavyo yameelezwa katika Idara husika.

**MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA 2015/2016**

Mhe. Spika, Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 itatekeleza majukumu yake kwa kutumia Mfumo wa Programu, ambapo itakuwa na programu kuu nne (4) na programu ndogo kumi (10). Programu kuu ni kama zifuatazo:

1. Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
2. Programu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji Wanawake;
3. Programu ya Kuimarisha Hifadhi ya Jamii; na
4. Programu ya Uongozi na Mipango ya Uwezeshaji na Hifadhi ya Jamii

Programu hizi zimezingatia Mipango Mikuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ni Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA II); Malengo ya Milenia; Ilani ya Uchaguzi 2010-2015 ya Chama Cha Mapinduzi (CCM); Mwelekeo wa Sera za CCM 2010-2020; Sera za Kisekta; na Mpango Mkakati wa Wizara.

**MALENGO MAKUU YA WIZARA**

Mhe. Spika**,** Wizara kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 imejipangia kutekeleza Malengo Makuu yafuatayo:

1. Kuimarisha hali za kiuchumi na ustawi wa jamii kwa vijana,wanawake, watoto, wazee na watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi na jamii kwa jumla;

2. Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za hifadhi ya jamii kwa wanawake, vijana, watoto, wazee na makundi ya watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi;

3. Kukuza usawa wa kijinsia na mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto;

4. Kuhakikisha kuwa mapungufu ya Sheria na Sera katika masuala ya uwezeshaji na yanayohusu watoto, wanawake, vijana, wazee na watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi yanafanyiwakazinakusimamia utekelezaji wake;

5. Kuhakikisha kuwa taarifa zinazohusu masuala ya wanawake, vijana, watoto, wazee, hifadhi ya jamii na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi zinakusanywa na kutumiwa katika kuandaa na kuimarisha Sera, Mikakati na Programu;

6. Kukuza uwezo wa Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi; na

7. Kusimamia mageuzi ya mfumo wa ushirika ili kuviwezesha vyama vya ushirika kuchangia katika kukuza ajira na uchumi wa nchi.

## PROGRAMU ZA WIZARA NA BAJETI KWA MWAKA 2015/2016

### Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Mhe. Spika, Programu hii inalenga kuinua hali za wananchi kiuchumi kwa kuwapatia mikopo, kuwajengea uwezo wa ujasiriamali na kuwaunganisha katika vyama vya ushirika. Matarajio ni kuona kuwa kila Mzanzibari anafanya shughuli za kiuchumi kukidhi mahitaji yake ya msingi. Programu hii ina programu ndogo tatu (3) zifuatazo:

1. Uratibu na Usimamizi wa Mikopo ya Uwezeshaji;
2. UsimamizinaUimarishajiwaVyamavyaUshirika; na
3. Uratibu na Uendelezaji wa Program za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Mikopo ya Uwezeshaji inasimamiwa na Idara ya Mikopo na inalenga kuwawezesha wananchi kwa kuwapatia mikopo nafuu ili waweze kujiajiri katika shughuli mbali mbali za kiuchumi. Programu hii ndogo imepanga kutoa mikopo 600 yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Sita (600,000,000/=) kwa wajasiriamali, na kuhakikisha urejeshaji wa mikopo hiyo kwa wakati. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Programu hii ndogo imekadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Milioni Sabini na Mbili, Laki Tano na Elfu Tisa (T. Shs. 72,509,000/=).

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika ina lengo la kuimarisha na kuongeza ufanisi wa vyama vya ushirikia ili viweze kuchangia katika kukuza ajira na pato la taifa. Shughuli zinazotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka 2015/2016 ni pamoja na kusajili vyama vya ushirika 200, kuvipatia mafunzo vyama vya ushirika 250 na kufanya ukaguzi wa kawaida na ukaguzi wa hesabu kwa vyama vya ushirika 1,000. Programu hii ndogo itatekelezwa na Idara ya Ushirika na kwa mwaka wa fedha 2015/2016, inakadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Milioni Arobaini na Moja, Laki Tano Elfu Ishirini (T. Shs. 41,520,000/=).

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Program za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ina lengo la kutanua na kukuza programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Shughuli zinazotarajiwa kufanywa ni pamoja na kuwahamasisha wananchi 2,500 wakiwemo vijana kuhusu ujasiriamali; kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wananchi 1,000; kuimarisha makongano ya matunda na mbogamboga na ufugaji wa kuku na kuandaa mikutano ya uratibu wa masuala ya uwezeshaji. Aidha itatoa mafunzo juu ya shughuli mbali mbali za uwezeshaji kiuchumi kupitia Kituo cha kufundisha wanawake utengenezaji wa vifaa vya umeme wa jua, Kibokwa na Kituo cha Kukuza Wajasirimali, Mbweni. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya

Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Wananchi Kiuchumi na kwa mwaka wa fedha 2015/2016 inakadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Milioni Mia Tano Hamsini na Tano, Laki Saba na Elfu Arobaini na Saba (555,747,000/=).

**Program ya Kukuza Usawa wa Jinsia na Uendelezaji wa Wanawake**

Mhe. Spika, Programu inalenga kukuza usawa wa kijinsia, kuimarisha uwezo wa wanawake kiuchumi; kuongeza ushiriki wa wanawake katika uongozi na vyombo vya kutoa maamuzi na kutokomeza udhalilishaji wa kijinsia. Matarajio ya programu ni kuimarisha hadhi ya wanawake katika jamii. Programu hii ina programu ndogo mbili (2) zifuatazo:

1. Uratibu wa Masuala ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake.
2. Mapambano Dhidi ya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Uratibu wa Masuala ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake inasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto na ina lengo la kuondosha tofauti za kijinsia na kumwezesha mwanamke kiuchumi na kijamii. Shughuli zinazotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka 2015/2016 ni pamoja na kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi 50 vya kiuchumi vya

wanawake; Kujenga uwezo wa Wanawake 140 kushika nafasi za uongozi kwenye ngazi za Wilaya na Shehia; kuzijengea uwezo kamati 30 za malezi za Shehia na kufanya mikutano 4 ya kuratibu shughuli za wanawake. Programu hii ndogo inakadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Milioni Mia Mbili Sabini na Sita, Laki Tatu na Elfu Sabini na Nne (T. Shs. 276,374,000/=).

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Mapambano Dhidi ya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto inasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Lengo lake ni kukuza mwitiko na kuratibu mapambano dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto nchini. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2015/2016 ni kuhamasisha wanajamii katika Shehia 100 juu ya kuchukua hatua dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto; kujenga uwezo wa taasisi kukabiliana na vitendo hivi, kupokea na kushughulikia malalamiko yanayowasilishwa Wizarani; na kutoa huduma za ushauri nasaha kwa waathirika wa vitendo vya udhalilishaji. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Programu hii ndogo imekadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Milioni Ishirini na Nne, Laki Mbili na Elfu Arobaini na Tano (24,245,000/=).

**Programu ya Kuimarisha Hifadhi ya Jamii**

Mhe. Spika, Programu hii inalenga kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii, hifadhi ya mtoto na huduma kwa wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi, wakiwemo wazee. Matarajio yake ni kuimarisha upatikanaji wa huduma za hifadhi ya jamii kwa wananchi wa Zanzibar wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Programu hii ina programu ndogo mbili zifuatazo:

1. Uratibu wa Huduma za Hifadhi ya Jamii; na
2. Uratibu wa Maendeleo ya Vijana.

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Uratibu wa Huduma za Hifadhi ya Jamii ina lengo la kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii na huduma kwa wazee na watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Kwa mwaka 2015/2016 shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuimarisha mfumo wa hifadhi ya watoto katika ngazi za Wilaya, kutoa misaada ya kijamii kwa watu 165 wanaoishi katika mazingira magumu zaidi, kuhudumia watoto 40 wanaoishi katika nyumba ya kulelea watoto yatima Mazizini; kufanya ukaguzi wa vituo vya kulelea watoto; kuwahudumia wazee 165 wanaoishi katika makaazi ya wazee Welezo, Sebleni, Limbani na Makundeni, kulipa fidia kwa wafanyakazi wanaopatwa na ajali kazini na kuratibu utoaji wa pensheni jamii kwa wazee wote wa kuanzia umri wa miaka 70. Programu hii itatekelezwa na Idara ya Ustawi wa Jamii na kwa mwaka wa fedha 2015/2016 inakadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Sita Ishirini na Nne, Laki Tano na Elfu

Tano (T.Shs. 2,624,505,000/=).
Mhe. Spika, Programu ndogo ya Uratibu wa Maendeleo ya Vijana ina lengo la kuratibu shughuli za vijana, ikiwemo kuimarisha ushiriki wao katika masuala ya kiuchumi na kijamii. Shughuli zitakazotekelezwa kwa mwaka 2015/2016 ni pamoja na kuanzisha na kuimarisha mabaraza ya vijana katika ngazi za Shehia, Wilaya na Taifa; kuhamasisha na kuviimarisha vikundi 30 vya kiuchumi vya vijana, kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2016 na kusimamia utoaji wa elimu ya stadi za maisha kwa Vijana 5,000. Programu hii ndogo itatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Vijana kwa kushirikiana na Baraza. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, inakadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Milioni Mia Tatu Themanini na Mbili, Laki Sita na Elfu Sitini na Sita (T. Shs. 382,666,000/=).

**Programu ya Uongozi na Mipango ya Uwezeshaji na Hifadhi ya jamii**

Mhe. Spika, Programu hii ina lengo la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mipango, Sera na Program za Wizara, pamoja na shughuli za Utafiti. Aidha, inahusika na kusimamia maslahi ya wafanyakazi na kuhakikisha mazingira bora ya utendaji wa kazi. Matarajio ya programu hii ni kuimarisha ufanisi wa kazi za Wizara. Programu hii ina programu ndogo tatu zifuatazo:

1. Kusimamia Mipango, Sera na Utafiti;
2. Usimamizi wa Huduma za Utawala na Utumishi; na
3. Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Kusimamia Mipango, Sera na Utafiti ina lengo la kuratibu na kusimamia uandaaji na utekelezaji wa sera, tafiti, mipango na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi, hifadhi ya jamii, usawa wa jinsia na maendeleo ya wanawake, watoto, wazee na vijana. Pia, inalenga katika kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Wizara. Shughuli zitakazotekelezwa kwa mwaka 2015/2016 ni pamoja na kuandaa mipango ya utekelezaji kwa sera za uwezeshaji, vijana na watoto; kufanya utafiti juu ya athari za mmomonyoko wa maadili kwa vijana; na kufuatilia, kutathmini na kuandaa ripoti za utekelezaji wa programu na miradi inayosimamiwa na Wizara. Programu hii itatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na kwa mwaka wa fedha 2015/2016 inakadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Milioni Themanini na Tano, Laki Tisa na Elfu Sabini (T. Shs. 85,970,000/=).

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Usimamizi wa Huduma za Utawala na Utumishi ina lengo la kujenga mazingira mazuri ya kazi kwa kuhakikisha upatikanaji wa maslahi ya wafanyakazi, vifaa na huduma muhimu. Shughuli zitakazotekelezwa kwa mwaka 2015/2016 ni pamoja na kugharamia mafunzo kwa wafanyakazi 9; na kusimamia upatikanaji wa maslahi ya wafanyakazi,

vifaa na huduma muhimu kwa wafanyakazi. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Programu hii ndogo imekadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja Themanini na Mbili na Laki Saba (T. Shs 2,182,700,000/=).

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba inasimamiwa na Ofisi Kuu Pemba na inaratibu utekelezaji wa programu zote za Wizara kwa upande wa Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Programu hii ndogo inakadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Milioni Mia Saba Sitini na Nane, Laki Nane na Elfu Sitini na Nne (T. Shs 768,864,000/=).

Mhe. Spika, Kwa maelezo kamili kuhusu Programu za Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii , Vijana, Wanawake na Watoto, tafadhali angalia kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu (*PBB*) kwa mwaka wa fedha 2015/2016-2017/2018, kuanzia ukurasa wa 650 hadi 671.

**MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

Mhe. Spika, Ili Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto iweze kutekeleza Programu zake kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Saba, Milioni Kumi na Tano na Laki Moja (T. Shs. 7,015,100,000/=). Kati ya hizo, Shilingi Milioni Mia Sita Sitini na Tisa, Laki Saba na Elfu Sabini na Sita (T. Shs 669,776,000/=) ni kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Shilingi Milioni Mia Tatu, Laki Sita na Elfu Kumi na Tisa (T. Shs. 300,619,000) kwa ajili ya Programu ya Kukuza Usawa wa Jinsia na Uendelezaji wa Wanawake; Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Saba, Laki Moja na Elfu Sabini na Moja (T. Shs. 3,007,171,000/=) kwa ajili ya Programu ya Kuimarisha Hifadhi ya Jamii na Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Thelathini na Saba, Laki Tano na Elfu thelathini na Nne, (T. Shs. 3,037,534,000) kwa ajili ya Programu ya Uongozi na Mipango ya Uwezeshaji na Hifadhi ya Jamii. (Angalia Kiambatisho Nam. 7(a) na 7(b)).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara inakadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Kumi na Saba, Laki Sita na Elfu Sita (T. Shs.17,606,000/=) kutokana na ada ya usajili na ukaguzi wa vyama vya ushirika.

**HITIMISHO**

Mhe. Spika, Naomba uniruhusu nitoe salam na pongezi zetu za dhati

kwa mara nyengine tena kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kuniamini kuendelea kuiongoza Wizara hii hadi leo nawasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara kwa mara ya tano katika kipindi hiki cha miaka mitano. Namtakia kila la kheri, afya njema na maisha marefu ili aendelee kutuongoza kwa kipindi kijacho.

Mhe. Spika, Nami napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu (*Subhanahu Wataala*) kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa kipindi chote hichi na namuomba aendelee kunipa afya njema na umri mrefu wenye kheri na baraka.

Mhe. Spika, Nachukua fursa hii kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuzishukuru nchi, mashirika ya kimataifa na kitaifa pamoja na taasisi mbali mbali za Serikali na zisizo za Serikali ambazo zilishirikiana na Wizara katika kutekeleza majukumu yake, zikiwemo *Jamhuri ya Watu wa China, Serikali ya India, Serikali ya Mauritius, UNDP, UNFPA, UNICEF, UN Women, IFAD, UNIDO, Shirika la Kazi Duniani (ILO), Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, SAVE THE CHILDREN, ACTION AID, FHI, VSO, COSTECH, Benki Kuu ya Tanzania, Benki ya Watu wa Zanzibar, Tume ya Haki za Binaadam, CRDB, ZAFELA, TAMWA na Kituo cha Huduma za Sheria.*

Mhe. Spika, Naomba kuchukuwa nafasi hii kuvishukuru vyombo vya habari ikiwemo Televisheni, Redio na Magazeti ambavyo vimetoa mchango mkubwa katika kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya masuala mbali mbali yanayotekelezwa na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, Napenda kuwashukuru na kuwapongeza Wafanyakazi wote wa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kuanzia Katibu Mkuu, Ndg. Asha Ali Abdulla; Manaibu Makatibu Wakuu wote wawili, Ndg. Ali Khamis Juma na Ndg. Msham Abdalla Khamis; Wakurugenzi wote, Ofisa Mdhamini, Maafisa wa ngazi zote na watendaji wengine kwa kufanya kazi nzuri, makini na juhudi kubwa zilizopelekea kutekeleza malengo na majukumu yetu kwa ufanisi. Aidha, nawaomba na kuwasisitiza waendeleze mashirikiano haya pamoja na kuzidisha upendo na nidhamu katika kazi, ili kuimarisha ufanisi.

Mhe. Spika, Kabla sijamaliza Hotuba yangu, naomba nikushukuru wewe Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika, Wenyeviti wako kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, wanawake na watoto kwa mwaka wa fedha 2015/16.

Mhe. Spika, naomba niwashukuru tena Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi na nawatakia kila la heri *Inshaallah* warudi tena tuendelee na jukumu letu hili zito.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja imetolewa ijadiliwe)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana nakushukuru sana Mhe. Waziri, maana uwasilishaji wa Bajeti hii na usomaji wako kama vile charahani. (*Vicheko*)

Hoja imeungwa mkono, kwa maana hiyo sasa hoja ijadiliwe tuanze kwa kumkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

**Mhe. Hassan Hamad Omar (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii):** Mhe. Spika, nakushukuru sana, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti, wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, naomba kusoma ripoti ya hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, kwa mwaka 2015/16.

Mhe. Spika, naanza hotuba yangu hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa vile ni jambo linalostahiki kipaumbele cha awali kutokana na neema yake ya kutujaaliya afya njema na uwezo wa kuendelea kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi na nchi yetu. Aidha, kipaumbele cha pili katika hotuba yangu hii, kabla ya kuzungumzia maudhui niliyoyakusudia ni kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo kutoa maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusiana na makadirio ya bajeti ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, naomba pia nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu mkuu kwa jitihada walizozionesha katika kutekeleza malengo na majukumu yao kwa bidii katika kipindi chote cha 2014/2015, lakini pia kwa mashirikiano yao mazuri waliyotupa wakati Kamati ilipokua ikitekeleza kazi zake.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii ya kuwapongeza wajumbe wote wa Kamati ya kudumu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa imani yao kubwa juu yangu iliyowapelekea kunichagua mimi kuwa ndio Mwenyekiti wao na pia kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonesha

wakati wote ambao Kamati ilipokua ikifanya kazi zake za ufuatiliaji pamoja na kuihoji serikali na kutoa maoni yao kwa lengo la kuimarisha utendaji na kukuza uwajibikaji katika serikali.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba uniruhusu niwatambue wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa jamii kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Hassan Hamad Omar | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Farida Amour Mohamed | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Abdi Mosi Kombo | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Ali Salum Haji | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Mohamed Mbwana Hamad | Mjumbe |

Mhe. Spika, pia napenda kuwataja Makatibu wetu wa Kamati ambao huwa tunashirikiana nao katika kazi zetu za Kamati na wamekua wakitusaidia kwa karibu katika kufanikisha kazi zetu nao ni:

1. Ndg. Asha Said Mohamed, na
2. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo napenda sasa nitoe maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ilipitia na kujadili kwa kina makadirio ya Bajeti ya Wizara hii, na hatimae kutoa maoni yenye lengo la kuengeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu kwa Wizara.

Mhe. Spika, Tathmini ya ujumla ya Kamati yangu kuhusiana na makadirio ya mapato na matumizi hayo yamejikita katika utaratibu wa programu.

Mhe. Spika, Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 imejipangia kutekeleza majukumu yake kwa kutumia programu kuu nne (4) pamoja na programu ndogo ndogo (10) kama ifuatavyo:

Programu ya 1 ni : Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi
Programu ya 2 ni : Kukuza usawa kijinsia na uendelezaji wanawake
Programu ya 3 ni : Kuimarisha Hifadhi ya jamii
Programu ya 4 ni : Uongozi na Mipango ya Ustawi wa Jamii

**Hali ya Makadirio ya Mapato**

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza wizara hii kwa juhudi kubwa wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yake. Hii imedhihirika wakati Kamati ilipokua ikichambua bajeti ya wizara katika kipengele cha mapato ikabainika kwamba kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Makadirio ya mapato yamezidi ambayo ni 17,606,000 ukilinganisha na yale ya mwaka wa fedha wa 2014/2015 ambapo yalikuwa ni 10,000,000 hii ni dalili kwamba Wizara imejipanga kuiongezea zaidi mapato Serikali, hatua ambayo Kamati yangu imefurahishwa sana.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaamini kwamba hili lengo litafanikiwa ikiwa wizara itaamuwa kuwapatia elimu ya kutosha watendaji wa Idara ya Ushirika juu ya kuwajengea uwezo kwa kazi zao wanazozifanya pamoja na kuhakikisha kwamba, Wananchi waliowengi kutoka mjini na vijijini wamepata elimu ya kutosha juu kujiunga na vyama vya ushirika pamoja na umuhimu wa usajili wa vyama vyao.

Mhe. Spika, kwa kufanya hivyo, Idara ya Ushirika itafanikiwa kupata fedha kwa njia ya malipo ya ada ya uandikishaji wa vyama hivyo pamoja na ada ya kuvifanyia ukaguzi.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa serikali yetu imeanzisha mfumo mpya wa bajeti ambayo inazingatia programu, bado bajeti yetu inaendelea kuwa ya makusanyo kwanza na kutumia baadae *(cash budget).* Katika mtindo huu wa bajeti inailazimu serikali kuwa na vyanzo vya uhakika vya kukusanya kodi na mpango madhubuti wa kudhibiti uvujaji wa makusanyo hayo. Mhe. Spika, mara nyingi katika bajeti zetu kinachokadiriwa kukusanywa sicho kinachopatikana, hili ni tatizo hasa ukizingatia hali ya upatikanaji wa mapato kwa serikali bado ni ndogo ukilinganisha na mahitaji ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, Kamati ya Ustawi wa Jamii inaishauri Wizara kusimamia kwa umakini vyanzo hivyo pamoja na kuwa wabunifu wa kuanzisha vyanzo vyengine vya mapato kwa lengo la kuisaidia Serikali na Wananchi kwa ujumla katika suala zima la kuboresha maisha ya kila Mzanzibari.

**Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

Mhe. Spika, Kamati inaishauri Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kujenga tabia ya kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi pindi inapotembelea wajasiriamali wake kwani kumejitokeza tatizo la wajasiriamali wingi hususani wale wanaojishughulisha na kazi za ufugaji wa samaki kutofahamu kuwa kuna wataalamu wa kizalendo ambao wanapatikana

Zanzibar. Mashirikiano hayo yataleta tija kwa wajasiriamali wetu na italeta ufanisi wa kazi zao.

Mhe. Spika, Kamati imeridhishwa na kiwango cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kusimamia programu hii kubwa pamoja na programu ndogo ambazo zimejitokeza katika programu hii. Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha kujenga tabia ya kuingiza fedha kwa wakati unaofaa ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi na kwa muda iliyopangiwa, kwani programu hii ina lengo la kuwasaidia wananchi kiuchumi ili kukidhi mahitaji yao ya msingi.

Mhe. Spika, Kamati pia inaipongeza Wizara ya Uwezeshaji na Ustawi wa Jamii kwa kiwango cha fedha kilichotengwa kwa madhumuni ya programu ya kuratibu na Usimamizi wa mikopo na ufuatiliaji wa malipo ya mikopo hiyo.

Mhe. Spika, Kwakweli programu hii inahitaji umakini sana hasa katika kutunza kumbukumbu kwa vile vikundi vilivyowahi kuchukua mikopo vingi husambaratika na hatimae pesa hupotea na kutorudi tena serikalini kwa lengo la kuwakopesha wananchi wengine ili na wao wafaidike na huduma hiyo. Hivyo, wizara iengeze umakini ikiwa pamoja na kuengeza nguvu kazi kwa lengo la kuhakikisha vikundi vyote vinapitiwa na kukusanya marejesho yote bila ya upotevu wa pesa.

**Programu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji Wanawake**

Mhe. Spika, programu hii imejikita katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake pamoja na kuwahamasisha wanawake kushiriki katika ngazi za maamuzi.

Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaunga mkono kiwango cha fedha kilichowekwa na Wizara ya Uwezeshaji juu ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa wawanawake na watoto.

Mhe. Spika, Kamati imebaini kuwa, kukosekana kwa kifaa cha *DNA* kunapelekea kutopatikana kwa ushahidi wa kitaalamu kwa kesi za udhalilishaji ambazo zinawalenga zaidi wanawake hasa watoto ambao wana magonjwa ya akili na hawana uwezo wa kujieleza mpaka kipatikane kwa vipimo vya *DNA* kwa ajili ya uchunguzi na kupatikana na majibu ya kipimo hicho yanasaidia katika kutoa ushahidi. Hivyo, kamati inashauri serikali ifanye ununuzi wa haraka wa kifaa hicho muhimu ili kusaidia katika kufanikisha programu ambayo lengo kuu ni kukuza usawa wa jinsia pamoja na kuondoa udhalilishaji.

Mhe. Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la ushirikishwaji wa wanawake katika ngazi za maamuzi. Hivyo, programu hii ya kuhamasisha wanawake

kushiriki katika ngazi za maamuzi ni hatua za busara zilizochukuliwa na serikali kupitia wizara hii zenye lengo la kuwakwamua wanawake wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Kamati imeridhia kima cha fedha kilichotengwa na Wizara kwa ajili ya kuwapatia mafunzo maafisa pamoja na wanasiasa juu ya uwezeshaji wanawake.Kamati yangu ya Ustawi wa Jamii inaunga mkono suala hilo kwa lengo la kuleta uwiano katika ngazi za maamuzi ndani na nje ya serikali.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza wizara hii kwa juhudi wanazozichukua za kuanzisha mabaraza ya watoto, kusheherekea siku ya watoto Duniani pamoja na kuboresha riporti za watoto. Mhe. Spika, programu hii itasaidia pia katika mapambano ya kuwatoa watoto katika ajira mbaya kutoka katika maeneo tofauti ndani ya Zanzibar na kuwarudisha skuli kwa lengo la kuwapatia elimu ambayo itawasaidia katika maisha yao.

**Programu ya Kuimarisha Hifadhi ya Jamii**

Mhe. Spika, katika riporti ya Kamati ya kudumu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ilielezea jinsi gani Idara ya Ustawi inavyofanya kazi katika mazingira magumu kwa vile ilikua haipatiwi pesa za posho kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi wanaozika maiti zisizokuwa na wenyewe.

Mhe. Spika, Kamati inatoa pongezi zake za pekee kwa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuyafanyia kazi maagizo ya kamati kama ilivyoelekeza na kuamua kutenga jumla ya shilingi 9,000,000 kwa ajili ya kutoa huduma ya kuzika maiti zisizokua na wenyewe. Aidha, Kamati imebaini kuwa, maiti zimekuwa hazina sehemu nzuri ya kuhifadhiwa kutokana na kuwa chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja ni kibovu na kichakavu hali inayopelekea uhifadhi mbaya wa maiti hizo.

Mhe. Spika, Kamati naiomba serikali ili zingatie na jambo hilo kwani sote ni maiti watarajiwa.

Mhe. Spika, sote tunaamini kuwa mazingira mazuri ya kazi yanapelekea kuwepo kwa ufanisi katika kazi na kufanyakazi katika mazingira hatarishi ambayo mfanyakazi haijui hatma yake hupelekea mtu kufanyakazi chini ya kiwango. Hili limedhihirika pale Kamati yako ilipotembelea katika wodi ya viungo bandia ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na kukutana na baadhi ya wafanyakazi ambao wameumia kazini na hawakupatiwa msaada wowote kutoka sehemu zao za kazi.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaunga mkono kiwango cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kuwalipa fidia wafanyakazi 20 wa serikali waliopata ajali wakiwa kazini. Hili ni jambo zuri ambalo serikali imelianzisha kwani kuwepo kwa fidia hizo ambazo zinapatikana katika uratibu wa huduma za Uhifadhi zitapelekea watendaji wetu kufanya kazi kwa bidii kwa vile wanauhakika na hatma zao za baadae.

Mhe. Spika, shukrani za dhati tunazitoa kwa fungu lililotengwa kwa programu hii ya kutoa misaada ya kijamii kwa watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Hii inaenda sambamba na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2015/16 uliowasilishwa na *AR* Ikulu na Utawala Bora, siku ya tarehe 13 katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi iliyoeleza kukuwa kwa uchumi ambako umeenda sambamba na kuimarika kwa ustawi wa wananchi. Kamati yangu katika kuchambua hali ya ukuaji wa uchumi kwa kuzingatia Mpango wa Utekelezaji wa MKUZA II imeona kuwa programu hii itapelekea kuimarika kwa uchumi wa nchi yetu. Mhe. Spika, ni dhahiri kuwa mgao huo wa programu ndogo ndogo umefanywa kutokana na majukumu makubwa yaliojitokeza katika programu kuu.

**Programu ya Uongozi na Mipango ya Uwezeshaji na Ustawi wa Jamii**

Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii imesikitishwa kwa kutoona mradi wa ujenzi wa Afisi kuu Pemba katika programu za Wizara hii, hali ambayo inapelekea wizara kuendelea kutumia gharama kubwa za fedha kwa ajili ya kulipia kodi kwa kila mwaka.

Mhe. Spika, Kamati inaiagiza serikali kuanza kwa ujenzi wa Afisi hiyo kwa upande wa Pemba ili kuokoa gharama hizo na hatimaye kuzitumia kwa programu nyengine ambazo Wizara itahisi zinafaa.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza wizara kwa mipango yake iliyojiwekea ya kumuajiri mtalamu muelekezi kwa ajili ya kuifanyia kazi Sera ya Uwezeshaji na kuandaa mpango wa Sera za Vijana. Progamu hizi zitasaidia kuengeza kasi ya maendeleo hasa kwa walengwa ambao ni vijana kwani wao ndio tegemezi kubwa la Taifa letu katika kutuletea maendeleo. Mhe. Spika, Programu hizi kama zitasimamiwa kiumakini basi zitatuletea faida kubwa kwa nchi kwani vijana wengi watafaidika pindi sera hiyo itakapokamilika katika ngazi zote.

Mhe. Spika, wakati wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ilipotembelea baadhi ya familia ambazo zinaishi katika mazingira magumu zaidi hapa Unguja, tuligundua kuna changamoto nyingi ambazo zinakabili familia hizo ambazo zinawasababishia kuishi katika hali duni ambayo hairidhishi kabisa. Mhe. Spika, kamati yangu inaunga mkono fungu lililotengwa kwa programu za kutoa huduma ya fedha kwa familia 70 zinazoishi katika mazingira magumu kabisa, hii

inadhihirisha kuwa Serikali yetu ni sikivu na inawajali wananchi wake hasa wale wenye hali ngumu za kimaisha ili nawe waweze kuishi kwa amani na furaha kama wananchi wengine hapa Zanzibar.

Hitimisho, Mhe. Spika, mwisho naomba tena kuchukua nafasi hii adhimu kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, aidha, ninawashukuru wajumbe wako kwa utulivu waliouonesha wakati ninawasilisha hotuba hii.

Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii kuwaomba wajumbe wako wa Baraza hili Tukufu kuchangia bajeti hii, kutoa mapendekezo pamoja na kupitisha baada ya kuafikiana kwa hoja mbali mbali zitakazoibuka wakati wa mjadala.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru sana kunipa nafasi hii leo asubuhi, ambae ni sharifu kuweza kuichangia wizara hii kubwa sana iliyokusanya vijana, iliyokusanya kinamama, halikadhalika pamoja na wazee, nishukuru sana kwa hilo na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atanijaalia nende kwa utaratibu mzuri sana.

Mhe. Spika, nianze na moja, kwa sababu hapa nilijaribu sana kutafuta sentensi ambayo inayoonesha mazingira ya mashine ya *DNA* katika kitabu hiki kwa Mheshimiwa sijaiona sentensi hiyo, lakini niweze kumwambia Mheshimiwa, umuhimu wa kuwa na mashine hasa katika usimamizi wa kitengo chake ilikuwa ni muhimu sana.

Mhe. Spika, Unyanyasaji wa kijinsia hapa ndipo pake kwa sababu hii ni wizara ambayo inayotendewa masuala hayo, ndio maana nikasema kuna jamii imekusanya wizara hii. Hilo suala mimi sitolionea tabu kulisema nitalitetea kwa nguvu zangu zote, siogopi vitisho wala siogopi kutishiwa kwamba sitopewa jimbo, naamini binaadamu haiwi viongozi wangu pengine hawanitakii mema niwemo katika jimbo lile na hiyo sijali, seuze hao ambao ndio nikapiga kelele kuhusu suala la unyanyasaji. Nitakuwa mstari wa mbele maisha milele kutetea suala hili.

Mhe. Spika, mashine hii ilikuwa wewe Mheshimiwa uidai kwa nguvu zote pamoja na uchanga wako wa kuwa na fedha ndogo za bajeti, kwa sababu kesi hazishi, kesi haziendi, ubakaji unakuja siku hadi siku, na kwa kuwa wabakaji wanakuwa wana taaluma wanajua jinsi gani ya kuweza kupoteza ushahidi. Sasa chombo hiki kilikuwa ni muhimu nimeomba sana nilisikitika sana na nilisema sana. Lakini leo

kwa bahati mbaya kwenye kitabu chako hili neno sijaliona, ninajua labda itakuwa watu wa *typewriter* au komputa binaadamu imo kukosea.

Mhe. Waziri, humu ulisema suala la Mhe. Rais wangu mpendwa kabisa, lakini nisikitike sana haiwi Mheshimiwa ameona kufanya suala hilo la kampeni na akazindua na akalieleza swali hili, lakini *still* leo Mhe. Spika, hili suala bado mimi nasema halijaungwa mkono. Kwa sababu nikasema kuwa halijaungwa mkono kwa njia moja mpaka mbili, ninaweza kutoa *example*.

Njia ya kwanza kutokana na mashine hii haijapatikana, hapa hapakuungwa mkono, kwa sababu ingeonesha wazi kuungwa mkono kwa Mhe. Rais, ni jambo ambalo mimi nimesikitika sana, huyu Rais mkubwa na amelipokea suala hili kwa masikitiko na akaona aunde Tume. Sasa mimi nashangaa Tume kwa nini isione kuweza kutafuta njia za kuweza kubana, hatujawa *serious* na hatuna ukweli, tunamvunja nguvu Mhe. Rais wetu, hili tulikubali wala tusiwe na masikitiko. Kwa sababu juzi moja kuna mtoto mmoja wa miaka miwili, mitatu mpaka minne, mzee aliyekamatwa nilimkuta mwenyewe anapigwa mikwaju nilicheka sana, ni mtu mzima amemdhalilisha mtoto mitaa ya katikati hapa meli tano kwa ndani anaburuzwa.

Mheshimiwa, hebu tuone juzi tu na tutizame Mheshimiwa kwenye kitabu ulivyotueleza kuwa Mheshimiwa alifungua kampeni muda gani na sasa hivi, maana yake ni mambo ambayo Mheshimiwa tuone jinsi gani Mhe. Rais wetu alivyozindua kampeni ile tarehe 6/12/2014 tuna matukio mangapi mpaka sasa hivi, kwa kweli hili suala Mheshimiwa hatujawa *serious* kabisa, hatujitolei kumuunga mkono Rais, mimi nasema nafsi yangu nimemuunga mkono Rais na nitaendelea kumuunga mkono Mhe. Rais, lakini ninamuunga mkono kibubu, ninamuunga mkono kibubu vipi, kauli yangu sauti yangu haina mashiko, haina sheria; Siko kwenye Tume ninaelea tu niko angani hivi, isipokuwa mimi hapa ndipo nimeona nijieleze kwa sababu hapa ndio wakili wenyewe wa kuweza kueleza suala hilo. Mhe. Spika, inasikitisha sana.

Mhe. Spika, wanaharibiwa watoto wanaume wadogo vya kusikitisha kabisa, tutakosa watoto wetu Mheshimiwa, hatimaye itatuendea wapi, kwa sababu watu wengine wanadhalilisha hata hao wanaume, pamoja na wanawake na wanaume wanawadhalilisha na kuwadhalilisha wenyewe watoto wadogo wa wavuja jasho, watoto wadogo wa maskini. Anategemewa mwananngu Mwenyezi Mungu akimjaalia atakuwa katika hali ya ustawi mzuri na kuweza kumpatia mama yake kumsaidia mbele ya safari, leo mtoto anaharibiwa mapema, kamati iko wapi, wizara iko wapi, vyombo vya sheria viko wapi. Lazima tuseme ukweli ulivyo, nini tegemeo, tuna tegemeo gani, mtoto mdogo ana miaka miwili, mitatu, anaendeshwa

sivyo na anafanyiwa vituko sivyo. Hatuko *serious* siku zote tunasema hapa, tunapitisha mafungu lakini hatimae hakuna kinachofanyika.

Mhe. Spika, mimi sishughuliki na mtu anambie na nalikosa hili jimbo, potelea mbali Mwenyezi Mungu ndio muweza; mtoa kila haki, muumba mbingu na viumbe, hiyo mimi wala sioni tatizo kabisa, sitoona shida wakati jambo limeonekana. Ndio maana nikasema sitoomba dua, lakini jamani viongozi tujiulize, je, litoke kwa mtoto wa kiongozi, narudia tena sentensi yangu pangekalika hapa, lingetafutwa fungu la aina yoyote Mhe. Spika, siwaombei dua mawaziri wangu, la hasha, tunaomba sana.

Lakini tujiulize je, hawa watu wavuja jasho wenye kuharibiwa watoto wao tuna matumaini nao vipi na sisi ndio viongozi wakubwa, tutampelekea nini zawadi Mwenyezi Mungu, sote tujiulize kabisa. Ninatoa ushauri huo kama haukafanyika *never, okay,* hakuna tatizo mimi ndio *bye bye*, ndio naondoka sasa. Kurudi kwa fitina hizi sijui ya Mungu mengi, potelea mbali wala sijali kwa sababu Mungu ndio muweza *still* niko *strong,* niko pale pale wala sijali kitu hicho, nitaendelea na maisha yangu mazuri Mungu atavyoniekea. Ushauri huo Mhe. Waziri, ukiufata komesho ya unyanyasaji, naanza kukupa ushauri, Mheshimiwa, nimekaa katika *labor* yangu nilichogundua tatizo moja, kwanza *the first time* inunuliwe mashine, ukipata mashine hiyo tayari suluhisho zuri.

Lakini la pili, vyombo viwili kama havikwenda sambamba na cha tatu upewe mwenyewe tusidanganyane, kila siku tutapigwa mpira kila kila ushahidi utapokea. Chombo cha kwanza *DPP*, askari polisi, lazima wakubaliane washuke chini lazima kwa suala hili kuweko na *special team and then* na wewe ni mtu wa tatu ndio suala hili litakuwa. *Otherwise*, pengine vyovyote ninavyosema Mhe. Spika, tusidanganywe na tusimdanganye Rais wetu, tuseme ukweli.

Kwa sababu Mhe. Spika, Mhe. Rais, ni muungwana, ameona kuwa lile jambo limemuuma, anajua ana ukoo, anajua anaendesha nani, kama ni mimi, mimi najua anaendesha ni nani. Umenilisha kiapo na nikala kiapo na nikasema hili lazima sitokubaliana nalo. Mhe. Spika, naomba sana hili suala lingali linatuumiza, wanyonge linawaumiza. *Wallahi* tangu nianze ku-*study* mwenye ninafatilia *in silence* kabisa bila kufahamu mtu ninafatilia mimi, sijamuona mtoto wa tajiri hata siku moja kubakwa katika suala hilo, *believe me*. Sijaona mtoto wa Mwakilishi hata mmoja kubakwa katika suala hili, sijamuona mtoto wa waziri kubakwa katika suala kama hili. Anayebakwa Mwatima mvuja jasho, Juma mkulima, Khamis nani, hao ndio watoto wao wenye kubakwa.

Jengine ushauri wangu shuka chini kwa Polisi Jamii, dawa ya mwisho muarubaini huo asikudanganye mtu yeyote, haki ya Mungu kwa sababu Polisi Jamii *overall*

yote katika ile shehia anawatambua wale watu Mheshimiwa, *Wallahi* tunawatupa, *Wallahi* hatuwathamini Mheshimiwa, tenga fungu onesha ujasiri mwanamama, wewe ndio mzazi, sasa wewe ndio mzazi, ndio mwenye kututotoa sisi watoto. Hasira zikujie hapa Mheshimiwa, zikuume nenda Polisi Jamii Mheshimiwa, ninakwambia wakabidhi kazi Polisi Jamii *immediately* kabisa uone kama hili suala Mhe. Spika, halitotendeka, lakini *Wallahi* husikitika sana, tukisema mwisho mnatwambia tuna hoja finyu, *why*, tuna hoja finyu kweli, hizi hoja finyu, inawezekana mtu atakwambia waziri akishindwa jambo, basi tena atafute kichaka cha kupenyea anakwambia, aa, ni hoja dhaifu, hii hoja dhaifu, vitu tunavyovitoa kama hivi haiwezi kuwa hoja dhaifu, isipokuwa udhaifu unaonekana kuwa sisi kutokufatilia, ndio maana yake, mtu unashindwa kufuatilia baadae halafu unakuja unatupiga namna hii.

Lakini hili Mheshimiwa atakaesema Mungu ndie atakaemuona. Kwa sababu kitendo kibaya cha mtoto miaka miwili wasubiri wapo hao, lakini hiyo niseme kuwa hii *paragraph* yako hapa changu mimi hakioneshi vizuri lakini ipo katika programu ya kukuza usawa na jinsia na uwezeshaji katika masuala ndio yote hayo. Una programu nzuri sana Mheshimiwa, unataka kuwainua watu uchumi katika hali halisi ilivyo, unataka kuwainua vijana, lakini leo huku nyuma bado mlango uko wazi wa kunajisiwa vijana, uchumi huo utakuja wapi, uta-*cost* kweli.

Mheshimiwa, nikupe sifa moja hapa, kuna watendaji wako wa nyumba salama, Mhe. Spika, hiyo nyumba salama kweli lakini mimi na wewe hatuwezi kuijua *of course*, mimi siijui lakini ninajua kuna nyumba salama, lakini *Wallahi* Mheshimiwa, ukiambiwa humo ndani hasa yaliyokuwemo basi wewe mwenyewe utaanza kutoka machozi na utasema mimi sitaki kuona. Wanafanya kazi vizuri sana lakini hawana sheria, tatizo sheria zao ndogo, watu hawa ninawashukuru sana wao ndio wanaoona matatizo yote, mtoto kaharibika kwa kiasi gani na mtoto kadhalilika kiasi gani, vitoto vidogo vinatoka mikojo ovyo ovyo kutokana na kuharibiwa, usifikiri labda wana matatizo ya *urine, no*, kudhalilishwa.

Mheshimiwa, ingekuwa hili suala una sheria kunipa basi mimi niwe *bouncer* kuwa kila likitokea jambo hilo mimi nikapigane niko tayari, lakini sheria huna kama unaweza kunitengenezea niko tayari, nikisikia leo mtu wapi nikatie ngumi mimi niko tayari kwa ule uchungu wa ndani ya nafsi rohoni. Lakini niseme sheria huna Mheshimiwa, mwaka ujao watakaokuja watatungiwa wakati sisi tukiwa *bench* huku tutaweza kusaidia, tukiambiwa nenda tutakwenda kufanya. Lakini Mhe. Spika, hili suala kwa kweli haliniridhishi hata kidogo. Kwa kweli linauma sana, Polisi Jamii wapo twende tukawashirikishe na ukishawashirikisha basi watafatilia.

Mhe. Spika, niingie hapo hapo upesi upesi Idara ya Mikopo, Idara ya Mikopo kwa kweli nimeona jinsi *figures* hizi ulizotutajia hizi, lakini bado haijatoshelezeka.

Bado vijana wetu katika kuchukua mikopo hatujawapa taaluma ya kuwezesha vizuri, taaluma zetu ziko ndogo sana na mpaka leo sidhani kama hizi fedha ulowekeza kama zimerudi zote *hundred percent*, sidhani kama utanipa jibu hilo, naomba Mheshimiwa unisaidie hilo jibu kama lipo.

Kwa sababu gani Mheshimiwa, tatizo letu moja niseme ufuatiliaji ndio unakuwa mgumu siku zote. Programu ya ufuatiliaji katika maidara, mawizara hiyo ndio kiu, ndio tabu, uzito hapo Mhe. Spika, sijui kwa nini tunakuwa tunaona tabu, uzito uko, sijui labda tuseme vitendea kazi maafisa mnashindwa kuwapa au kujipanga tunashindwa kujipanga, labda hiyo kwa sababu hatujiwekei *special programme day and day,* hatujifanyii hicho, sasa hilo ndio tatizo lenyewe Mheshimiwa inatu-*cost* tatizo kujipangia siku hadi siku nifanye nini, nikae nini, nipate na nini, hilo tunakosa kwenye *brain* yetu, tunakosa sana suala hilo.

Na inavyotakiwa binaadamu yeyote ajipangie *plan* ya kazi, ajipangie *plan* ya biashara ajipangie *future* yake ya mwisho ya *vision* yake ataishia vipi maishani mwake, hakuna wenye mawazo hayo. Wapo wenye *PhDs*, sijui *DH*, sijui wana *Master* na wana nini, lakini wanakosa vitu kama hivyo na ukifanya *valuation* matajiri wengi katika nchi zetu hasa za kiafrika na Tanzania na Zanzibar wengi hawakusoma, tizama Mungu alivyofanya mambo yake. Wafanyabiashara wengi hawakusoma lakini ni matajiri Mwenyezi Mungu muweza. Sasa haya mambo Mhe. Waziri ndio kinachotu-*cost*, programu ya kupanga kuwafatilia wananchi inatukosa. Mheshimiwa, nimekuona niachie nimalizie nakwenda mbio mbio.

Mhe. Spika, Idara ya Vyama vya Ushirika. Hapa napo pana vilio vikubwa sana, ndio yale niliyokwambia kuwa hatu-*work* vizuri, hatwendi vizuri kuwa-*train* hawa, hatuwapi mifumo ambayo ya kujitajirisha, tunashindwa kutoa mifumo ya kujitayarisha Vyama vya Ushirika, Mheshimiwa inasikitisha sana. Lakini niweze kusema kitu kimoja niwasifu sana watu wa Ustawi wa Jamii wale Kitengo cha Afya kule hospitali ya Mnazi Mmoja, tunashirikiana nao vizuri, ninawashukuru sana wale jamaa. *Wallahi* wale vijana nasema ninawashukuru tena sana wapelekee *special request* na pongezi, sijawaona wale watu wanaoringa, sijaona kunipotezea misaada yangu ambayo ninapelekea wananchi, ninapokwenda tunakaa wote, tunabadilishana mawazo na wa kuliweza wao wanalifanya *immediately* kabisa, wananizikia maiti, wananihudumia watu ambao wanajua kuwa anastahiki nyumba za nini, *Wallahi* wale nimejikosha ndani ya nafsi.

Mhe. Spika, wale Mwenyezi Mungu atakaewapa pepo, ni wale kwa upande wangu nilivyoiona hiyo. Kwa hivyo, wale niwashukuru sana na waendeleze katika shukurani hizo.

Mhe. Spika, nije katika kumalizia huku ukurasa wa 34 katika mambo ya uwezeshaji mambo ya kiuchumi na nini. Mara nyingi sana huwa nasema suala la Benki ya Kinamama. Kinamama ndio nguvu kazi sasa hivi, kinamama na wao wanataka na wao waendelee kama kinababa, lakini suala la Benki basi kama hatuwezi Benki tufanye dirisha dogo, ambalo litaondoa urasimu, litaondoa kuwawekea riba kubwa, jamani hawa wazee wetu. mimi ninachoshangaa Mhe. Spika, humu ndani mna Waheshimiwa wengi tu kinamama wanashindwa hata kulitetea hili, la wao wenyewe ninawatetea mimi.

Kwa sababu ninaona uchungu kinamama naona jimboni kwangu wanavyohangaika, Jimbo la Kitope sasa hivi nenda *population* kubwa ya kinamama wamejiunga katika vikundi vya visanduku, wengi sana tu, lakini wanashindwa sasa kujiendeleza kwa sababu wanapokwenda kwenye mikopo wanakuta riba kubwa, *asset* watoe kubwa, wataweza wapi maskini ya Mungu, wizara yao ipo hii hapa. Mheshimiwa, hili lipiganie, hawa kinamama tunapata tabu wanadhalilika ni hawa, *the first time* kudhalilika kinamama Mheshimiwa, asikwambie mtu, watajirishe.

Sera ambayo tunatakiwa sisi Waheshimiwa tuwe na sera ya utajirisho. Tuwe na safari ya matumaini ili wananchi wetu waweze kuwa na matumaini yakuweza kujitajirisha. Ni kweli kabisa watoto wadogo wapo wana uwezo, kina mama, kwa nini kina mama washindwe. Mimi nataka nione leo kila mkisimama kina mama liteteeni hili suala ili watu waondokane na umasini, watoto wadogo wanamaliza masomo muda mdogo sana bado ni wadogo, lakini hawajui wafanye biashara gani. Nenda Bara sasa hivi *Harrier* anayoendesha Mhe. Hamza, Mwatima kule Bara anaendesha *Harrier*, hapa mpaka uwe Mwakilishi. Hapa uwe Mwakilishi au uwe katika sehemu ya fedha ndio unaendesha *Harrier*, lakini mkulima kule *Harrier* ya Mhe. Hamza, tulikwenda wote mimi na yeye tuliona haya, tuliificha pembeni tumesema tunajiamini kumbe tunakwenda kule kuwapeleka pahali yeye mwenyewe mkulima anayo kama ile. Mheshimiwa naomba sana.

Mhe. Spika, kwa kumalizia hili naomba hili lazima lishughulikiwe, Mheshimiwa, vijana wengi sasa hivi hawana kazi wako *jobless*. Kwa mfano, Mheshimiwa…

**Mhe. Spika:** Unamaliza kwa dakika tatu.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Kumi na tano, eeh?

**Mhe. Spika:** Tatu.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Nasikia kumi na tano.

Mhe. Spika, niende katika ukanda wangu wa uwekezaji kwa mfano kama kule Kiwengwa. Mhe. Spika, kule Kiwengwa angalia *population* ya kule, wananchi wa Kiwengwa hawana kazi, wananchi wa Kiwengwa wanaingizwa kwenye hoteli *just abortion* tu ikisha wanafukuzwa, kenda afisa gani kwenda kutetea kule na nyinyi ndio wenye vyombo vya sheria. Sisi tunazidiwa kwa sababu hatuna sheria, leo Kiwengwa watu wako nje utalii uko pale kulikuwa na *African Dinner, high population* ilikuwa kubwa zamani sasa hivi *population* imepunguzwa kwenda *African Dinner.* Tunakwenda wapi Mhe. Spika, utauinua uchumi kweli, vijana wanahangaika wako tele kule Kiwengwa, kina mama wako tele, wanajua kila aina ya kazi, mahodari wamejisomesha mpaka lugha wanajua sasa hivi, lakini leo Mheshimiwa, hakuna sheria zinazowalinda wakaweza kutumia uchumi wao.

Mheshimiwa, vijana wa *jobless* wapo, hivyo, tunaomba sana, sasa hivi nasikia kuna Naibu Katibu Mkuu wa Vijana, cheo kipya kimetolewa nashindwa hata kukitaja Mheshimiwa, ni vizuri, Katibu Mtendaji. Ni vizuri sana Mheshimiwa, kijana mzuri tumeona jinsi gani alipotoka, sheria anazo alikuwa akimuendesha uzuri tu waziri wangu wa majenzi na ndio maana sifa ikampa akaweza kuteuliwa. Namuomba sana kwa hili awe *serious* nalo akifanya mchezo mimi na yeye tutakutana kwenye ulingo nikirudi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa, niseme kuwa nishukuru sana kwa hilo, nitoe pongezi kubwa sana kwa Mhe. Waziri pamoja na Katibu wake na watendaji wake, lakini haya niliyoyasema ndio dira kubwa ya kuweza kuondoa unyanyasaji, ndio dira kubwa yakuondoa vijana kunyanyasika katika *jobless* na kuweza kupata kazi. Mheshimiwa, naunga mkono kwa asilimia kwanza kidogo nije kupata taarifa ya *machine* ya *DNA* waziri wangu amefikia wapi, nampa kidogo 50 halafu 50 naitia mfukoni, 50 nitakuja kumpa mwenyewe. Ahsante sana Mheshimiwa. (*Makofi*)

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, na mimi nataka nikushukuru kunipa nafasi hii kwa kuweza kuchangia hii wizara ambayo inayohusu *foundation* ya maisha yetu ya baadae. Pamoja na kwamba namshukuru Mwenyezi Mungu kama walivyotangulia wenzangu, lakini vile vile nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri. Mhe. Spika, Waswahili wanasema "Isiyokongwe haivushi".

Mhe. Spika, wewe mwenyewe shahidi, Mhe. Zaynab, wengi humu Barazani ametulea nikiwemo mimi, Mhe. Machano Othman Said, hata Mwalim Haroun na yeye amelelewa na Mhe. Zainab, hata Mhe. Ali Abdalla, kwa kweli wengi ametulea. Na leo mimi nataka niseme hiki kitabu chake pamoja na udogo wa hiki kitabu, lakini kwa kweli tumeona mafanikio makubwa sana ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano kama alivyosema alipopewa ridhaa na Mhe. Rais ili aweze kuisimamia wizara hii.

Mhe. Rais, anaona mbali na kwa kweli hakukosea na wizara hii angelimpa kijana basi leo haya matunda ambayo tunayaona mimi nadhani yasingefikiwa kiasi kama hiki, lakini aliona kwamba wizara hii ni ya ulezi ina kina mama, ina watoto na ina wazee, kwa hiyo, akaona mtu ambaye atakayeweza kuisimamia vizuri basi ni mzee lakini vile vile mwanamke kwa sababu wanawake kwa kweli wanajua kulea. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa nini nataka nianze kutoa hizo sifa, Mhe. Spika, Waswahili wanasema kwamba unaweza ukamuangalia kobe ukafikiria hachezi, lakini kobe anacheza, lakini lile gamba lile ni kubwa sana, lakini kama lisingelikuwa sio lile gomem kwa kweli watu wote wangekuwa wanamtunza yeye kwa namna anavyozungusha yale mabega yake. Sasa Mhe. Waziri, sifa hizi ninazokupa kwa sababu umeweza kuandaa misingi ambayo misingi hii Mhe. Spika, kwa nchi zetu hizi za dunia ya tatu zinazoendelea si rahisi sana kuweza kuji-*commit* serikali kuanza kuweka misingi imara ya huduma za ustawi wa jamii kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, suala la kuangalia utaratibu wa wazee, kwanza kuweza kuwajua wazee wako wangapi na wako wapi na wapi na wanafanya shughuli gani? Lakini vile vile baada ya kuangalia hizo shughuli zao, ukasema ah, basi bila ya kujali kwamba huyu alifanya kazi serikalini, huyu alikuwa mkulima na huyu alikuwa mvuvi, kwa hiyo, wazee wote serikalini baada ya Mhe. Waziri, kupeleka waraka wake serikalini. Hivyo, serikali waraka ule uliukubali na ukasema sasa hivi tuhakikishe kwamba wazee wote katika hii bajeti ambayo tumeipitisha, wazee wote ilimradi akishafika miaka 70, basi na yeye kila mwezi alau awe anapata posho japo ndogo yakuweza kukimu mambo yake madogo madogo. Kwa kweli hili ni suala kubwa sana, ni suala kubwa kwa nchi zetu za Kiafrika hasa sisi dunia ya tatu.

Mhe. Spika, leo Mhe. Waziri, msingi ambao aliouweka na tunategemea huko mbele nchi yetu itakuwa na utajiri mkubwa sana wa gesi, basi nadhani tutakapokuja kupitisha Sera ya gesi na mafuta, nadhani muongozo wa mwanzo tutauchukua muongozo aliouanzisha Mhe. Waziri, kwamba asilimia fulani ya mapato ya gesi moja kwa moja iende kwa wazee kuwahudumia katika kujenga maisha yao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa ni vizuri ukaandaa mipango yako kabla hujapata kitu, ili utakapoweza kupata kile kitu basi kazi yako itakuwa ni kuimarisha katika ile misingi ambayo uliyoiandaa. Kwa kweli Mhe. Waziri, katika jambo ambalo tunakupa pongezi sana ni hili.

Mhe. Spika, mimi kuna hizi *NGO's,* unajua siku hizi wanaharakati wako wengi na kuna wanaharakati wazee wenyewe wameamua sasa hivi wamejitoa hawasubiri

kusemewa wanaamua kujisemea wao yenyewe. Mimi walinifata wanayo ofisi yao pale Sebleni katika jimbo la Mheshimiwa jirani yangu hapa Mhe. Fatma, wameniita wakaniambia Mheshimiwa, sisi tunataka kuleta sera yetu ya wazee na katika sera ile ya wazee sisi tumeshafanya kazi sana serikali tumeshalitumikia Taifa, lakini tunafika pahala tunapita tukaomba tukaomba mpaka ile pesa ya sabuni tunaomba, kwa nini hamuwezi mkatufikiria? Mimi niliwaahidi kwamba mimi nitakuwa ni mmoja katika balozi wenu, kwa sababu na mimi uzee unakuja, kwa hiyo hili nitaweza kulisimamia.

Mhe. Spika, tuliwahi kumnong'oneza Mhe. Waziri, akaniambia Mheshimiwa, tulia, sisi tuna mpango mzuri zaidi wa wazee kuliko hata huo waliokuwa nao wao wenyewe, haikuchukua muda Mhe. Waziri, akanialika semina pale *Grand Palace* Malindi pale tukenda katika semina ile na tukaelezwa mtiririko wa wazee namna gani watakavyoweza kuja kuhudumiwa. Sasa mimi nataka niseme Mhe. Waziri, kumbe ile semina ilikuwa sio vile vibaja vya kuku na vikeki keki, lakini kumbe tayari ulikuwa umeshaandaa mpango ambao unaupeleka serikalini.Leo tunashuhudia serikali yetu *foundation* hii ambayo uliyoianzisha Mhe. Waziri, kwa kweli wale wazee wetu sasa hivi wanafarijika sana angalau sasa hivi wanakuwa wanasemwa, lakini wanasemwa katika lugha nzuri kwamba wanasemwa wazee kuwa wawezeshwe ili maisha yaende vizuri huko baadae.

Mhe. Spika, zamani watu walikuwa wanatafuta kila namna wana-*forge* vyeti ili kupunguza umri ili aweze kupata maslahi zaidi. Lakini Mheshimiwa naamini baada ya bajeti ya mwaka huu wakaonekana wazee wanavyoanza kutononoka, wakawa wanaonekana sasa hivi wazee wanafua, wanapiga pasi kwa ile sabuni ambayo watakaoanza kupewa, naamini sasa hivi watu wataanza ku-*forge* vyeti vya uzee, maana yake wataona kwamba ah, kumbe sasa hivi uzee mali. Maana yake zamani uzee ulikuwa unakimbiwa; watu wanatafuta ujana, wanatafuta udogo ili kupata maslahi, lakini sasa hivi maslahi yametangulia mbele, kwa hiyo, ina maana sasa hivi kila mtu atasema na mimi nimeshafika miaka 70 na tumeona humu humu ndani Barazani kila mtu anasema na mimi nishafika miaka 70 na mimi nishafika miaka 70, kwa sababu tayari wameona kwamba Mhe. Waziri, ameshaanza kuweka *foundation* nzuri ambayo wazee wetu wataweza kufaidika.

Mhe. Spika, mimi kwa bahati mbaya kitabu changu leo nimekiacha lakini ningejaribu kutoa aya, lakini nitajaribu kutoa japo hadithi ndogo ambayo tunayopewa na mashekhe wetu. Wanatwambia duniani baada ya kumuabudu Mwenyezi Mungu basi mtu wa pili unayetakiwa kumuangalia ni mzee wako. Leo Mhe.Waziri, amefata yale maandiko ile miongozo yetu ya Waislamu tunaoambiwa kwamba baada ya kumuabudu Mwenyezi Mungu na kumuheshimu Mwenyezi Mungu jambo la pili mshughulikie mzee wako.

Mhe. Waziri, tunakushukuru hapa umewajali wazee wako na wazee wetu. Mimi mama yangu alikuwa hajawahi kupata posho, posho anayoipata ninayogaiwa mimi, na mimi ninamgaia. Lakini kupitia bajeti ya Mhe. Waziri na juzi Mhe. Waziri wa Fedha ametenga fungu la kuja kuangalia wazee. Namuomba Mwenyezi Mungu mama yangu aniwekee hai aanze kufaidika na matunda ya Mapinduzi. Sasa Mhe. Spika, haya aliyoyafanya Mhe. Waziri, kama sisi bajeti hii kama hatukuiunga mkono tunataka nini chengine.

Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Waziri, nimechukua muda mrefu kuzungumzia suala hili kwa sababu lina umuhimu wake, kwa sababu wewe umeweka msingi. Sasa nawaomba hasa Mhe. Ali Mzee, kwamba tutakapokuja na mimi nakuombea sana uwe unarudi hapa Barazani kwa sababu gani? Katika mtu ambaye unatusaidia sana miongozo ya historia nakujua tulikotoka na tunakokwenda, basi serikali itakapoleta sera ya hii rasilimali mpya, uchumi mpya, moja katika eneo tutakaloliangalia kwenye mikopo ya elimu ya juu, fursa za watoto, lakini fungu hili la wazee ili waweze kutononoka. Kwa sababu Mhe. Spika, kama nilivyosema tunategemea baada ya hii serikali kupitia mfumo huu, kwa sababu wenzetu sasa hivi wana kigezo kwamba katika dunia ya tatu watu wanaishi mpaka miaka fulani. Mimi nadhani hata kile kiwango cha kuishi Zanzibar sasa hivi tunategemea tutakuwa na wazee wengi wanaishi muda mrefu. Tumezoea tu nchi za wenzetu Ulaya huko, Japan ukienda.

Mhe. Spika, kule Japan kuna sehemu kuna mitaa fulani ukienda wazee watupu, yaani hapo kuanzia miaka 90 mpaka 120, watupu, sasa nafikiri tujiandae na sisi kuwa na wazee wengi sana ndani ya Zanzibar. Lakini sio kama tunachukia tunapenda kwa sababu mzee wako anapokulea ukaendelea kwamba anakulea mpaka unakuwa mtu mzima anaendelea kukulea, kwa kweli inatupa faraja sana. Sasa Mhe. Spika, hizo ni pongezi maalum za wazee Mhe. Waziri, nakuletea ili ujue kwamba ulilolifanya umetengeneza *Sadakatujaria*.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nakwenda katika Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, mwenzangu Mhe. Mshimba, leo amejiita Sharifu ameshapata cheo kingine, Sharifu Mshimba, maana yake alikuwa Profesa Mshimba sasa hivi ni Profesa Sharifu Mshimba. Mimi kwa kweli naendelea tena kumuunga mkono katika suala zima la uanzishwaji wa benki ya wanawake.

Mhe. Spika, pamoja Mhe. Waziri wa Fedha, alieleza mambo mengi mtaji wa kuanzisha benki, lakini vile vile hii benki. Mhe. Spika, katika eneo serikali inatakiwa iekeze ni eneo la kuwahudumia wanawake.

Mhe. Spika, sisi hapa pamoja na hizi suti zetu tunazozivaa kama sijitihada za mama zetu, Mheshimiwa, sisi hapa wengine tusingeingia humu, tunajua hali zetu. Mhe. Spika, si vizuri kutoa historia ya wazee wako na nini, lakini mimi nilikuwa naona mama yangu alikuwa akichanja kuni pamoja na yeye mwanamke, anapika maandazi, anapika chapati, anafanya kila biashara kuhakikisha kwamba mtoto wake anafanikiwa katika mambo yake mbali mbali. Mababa sisi si mnatujua, mababa sisi ulichokiacha asubuhi kama kimetosha ndio hicho hicho, hakikutosha ndio hicho hicho, hurudi isipokuwa unarudi unauliza nikafunue wapi au unasubiri kuwekewa juu ya meza.

Na mara nyingi katika familia zetu Mhe. Spika, na wewe shahidi, nafikiri pamoja na kwamba uko Mjini siku nyingi lakini Makunduchi huwa unatembea tembea siku moja moja. Mazee kule akishaondoka nyumbani harudi mpaka wakati wa kula, hajui kama katimiza chungu au hakutimiza. Sasa chungu kile anakitimiza nani Mhe. Spika, wanawake, wanawake Mhe. Spika, laiti kama ingekuwa sikuongezea ongezea kuni kwenye chungu, wanawake hawa wangekuwa ni watu ambao wana uwezo mkubwa sana. Lakini fedha zao nyingi mara nyingi zinaishia katika kuwahudumia watoto wetu.

Mhe. Spika, sisi wengine pamoja na uwakilishi wetu, lakini inafika pahala unarudi unakuta kitu amefanyiwa mtoto wako, mama anakwambia mimi nimekifanya maana kila nikikwambia unajitia hamnazo, kila siku ukiamka una shughuli nyingi lakini mama tayari anakuwa ameshatengeneza. Sasa Mhe. Spika, kama tathmini waliofanya wao wenyewe ya kuangalia hali ya wajasiriamali, Mhe. Spika, serikali katika watu ambao wanaoisaidia sana serikali ni wanawake, karibu zaidi ya asilimia 70 ya watu ambao wanaofanya ajira sio rasmi ni wanawake, fedha hizo wangelikuwa wanasubiri tu kuajiriwa serikalini Mheshimiwa, wanawake kwa kweli wangelikuwa kanga zote zina matundu. Lakini leo Mheshimiwa, wanajitegemea wao wenyewe, tunashukuru Mhe. Waziri, kwa jitihada yako unatoa mikopo kidogo kidogo hivyo kwa wanawake. Lakini kwa kutegemea hii mifuko Mhe. Waziri, hawa kina mama bado wataendelea kupiga kelele.

Mhe. Spika, wewe mwenyewe ni shahidi nimeshakuja karibu mara tatu ofisini, nakuja kuwalilia kina mama wangu vikundi vya ushirika. Namshukuru sana Mkurugenzi wa Idara ya Mikopo baada ya kumuendea na kilio cha wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura alikuja tukafanya kikao nilipita jimbo zima kikundi kwa kikundi, vijana watu wazima sikujali mwanamke au mwanamme. Lakini asilimia kubwa ya walioitikia kwa sababu nilimwambia Mkurugenzi wa Idara ya Mikopo anataka kuja kukuoneni nyinyi wajasiriamali. Namshukuru sana alikuja pale Skuli ya Chekechea Mkele Bondeni maarufu, nishakuona Mhe. Spika, unataka kuniambia dakika zangu zimebakia kama kumi.

**Mhe. Spika:** Basi tumia dakika tano.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Haya ahsante.

Kwa kweli kina mama wale nashukuru sana walisikiliza maelezo ya Mkurugenzi na takriban karibu wote zaidi ya vikundi 35 walifuata yale masharti, wamekwenda kujisajili na vikundi vyao sasa hivi vimeshasajiliwa na tayari barua zao ziko Idara ya Mikopo.

Mhe. Spika, namshukuru Mkurugenzi baada ya kuona nafuatilia sana kaniletea ile orodha, lakini kwa kweli ile orodha ni ndogo sana na mule naweza nikasema labda ni vikundi viwili kwa sababu kaniletea idadi ya majina ya watu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa Mhe. Waziri, kama alivyonipa maelekezo na yeye ni mama yangu kwa kweli naheshimu sana mwongozo wake, basi naomba akija aje awape moyo, pale anapokuja ku-*wind up*, uje awape moyo wale kinamama hasa wa ndani ya jimbo la Kwamtipura kwa sababu ndio walionituma zaidi kuja kusema hivi. Basi na wao angalau ndani ya bajeti hii na watakaobakia japo bajeti ya mwaka ujao ambao na yeye ataweza kuwafikiria na nafikiri na wao wananisikiliza kilio chao kimefika.

Mhe. Spika, kwa kweli nawapongeza sana Idara hii ya Mikopo kwa sababu kweli tuko wengi lakini ndio kama tulivyosema bila ya kuwa na benki kwa kutegemea hii Mifuko kwa kweli tutakuwa tunapata tabu sana. Sasa hapa pia nilikuwa naomba, katika bajeti ya Wizara ya Fedha na naomba kwa kuwa watendaji wa Mhe. Waziri, pia wapo kuna fedha tulizitenga kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo, kuna Mfuko wa Miundombinu.

Mhe. Waziri, kuna fedha pale na fedha zile zimewekwa kwa makusudi ku-*support* Mifuko mingine. Naomba sana Mheshimiwa, tukishamaliza bajeti yetu muwaambie Wizara ya Fedha kwamba Waheshimiwa wanasema kinamama hao katika majimbo fedha wanazozipata hazitoshi. Kwa hivyo, katika fedha zitakazochangwa safari hii katika Mfuko wa Miundombinu, maana yake ule Mfuko wa Miundombinu usije ukafikiriwa labda Wizara ya Miundombinu, hakuna, Mfuko wa Miundombinu ili kuangalia kwenye mapungufu kuweza kuingiza fedha. Kwa hiyo, angalau kule akipata kama shilingi bilioni moja zikiingizwa huko katika Mfuko naamini kinamama wetu wengi wataweza kupata hizo fedha kwa wingi. Huo ulikuwa ni ushauri Mheshimiwa.

Jengine nataka nipongeze sana jinsi wanavyoshughulikia sasa hivi nyumba za Wazee. Mhe. Spika, sasa hivi wazee ukienda pale Sebleni utasema si wazee, utafikiria vijana, wanakula kutwa mara tatu, wanakunywa kutwa mara tatu.

Mhe. Spika, samahani siwasimbulii, sasa hivi pale nyumbani kwangu ilikuwa asubuhi kila wiki lazima utawakuta wazee wa majumba ya wazee siku hizi siwaoni, siku hizi wanakuja wale wananchi wa kawaida wa jimbo la Kwamtipura. Lakini sasa hivi wizara hii imefanya kazi kubwa sana, wazee wale sasa hivi wanakula kutwa mara tatu  na posho yao ya mwezi wanapata tunashukuru sana.

Mhe. Spika, nakuja la mwisho ili kwa kujali heshima yako. Sehemu ya suala zima la udhalilishaji wa watoto na wanawake. Kwa kweli hapa tunamuomba sana Mhe. Waziri, akaze buti. Bado kuna watu wanaendelea kutuchezea akili, mimi ninashauri serikali ilifanya maamuzi magumu kipindi cha nyuma na bila ya kujali mtoto wa nani, mtoto wa nani, tulianzisha Chuo cha Manunda na wale watoto watukutu walikuwa wanakamatwa wanapelekwa Chuo cha Manunda.

Mhe. Spika, mimi naomba, pamoja na kwamba kuna taratibu nyingi, ushahidi kamili, Mahakamani kwa kweli kesi zetu zinakuwa hazipati ile *priority,* mimi nafikiri tuanzisheni utaratibu.

Mhe. Spika, Marekani walipoona tatizo la madawa ya kulevya ni kubwa, kesi za madawa ya kulevya zilitengenezewa sheria maalum, hakuna ule utaratibu wa kwenda kwa *DPP*, ukigundulikana unafanya biashara ya madawa ya kulevya unakuwa *detained,* hata Mahakamani huendi, unakamatwa unakuwa *detained* pale kwa muda maalum.

Sasa na hawa kuna wababakaji wazoefu, hebu tuleteeni sheria. Mhe. Mwanasheria Mkuu, naomba tuandae sheria ya *detained* kwa hawa wababakaji. Mhe. Spika, utaratibu wa kusema sijui kesi iende kwenye Kitengo cha Ushauri Nasaha, sijui *DNA* mpaka ikaangaliwe, sijui kitu gani, hakijakauka, mtu baada ya kuchafuliwa mtoto wake, alimfua. Mimi nafikiri tukiweka utaratibu wa *detention* hawa wababakaji wakiwekwa Tunguu Chuo cha Manunda, nafikiri kile chuo bado kipo wawekwe hawa, sasa tuangalie, je, watabakana wenyewe kwa wenyewe?

Mhe. Spika, kwa sababu inafika pahali sasa hivi mitaani unaona tabu wewe, yaani watoto siku hizi imekuwa aibu, mtoto akienda skuli akirudi apekuliwe, akienda akirudi apekuliwe, hii tutafika pahala gani. Kuna maeneo hayapekuliwi pekuliwi, lakini kutokana na hofu sasa hivi ya wazee na watoto wao, vitoto kila siku vinapekuliwa. Sasa mimi nilikuwa naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu, hebu waangalie utaratibu tunaweza tukafuata mfumo wa Marekani alipodhibiti madawa ya kulevya. Mtu yeyote ambaye ana kesi zaidi ya tatu za ubakaji tumuandalie sheria ya kum-*force* na kumkamata na kum-*detain* halafu baadae tufanye uchunguzi.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru sana, naunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri, kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Mhe. Spika, nami nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami kuweza kuchangia machache katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, kwa kuanzia kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, kwa kazi nzuri ya kuwasilisha hotuba. Lakini pili niwapongeze watendaji kwa msaada wao wanaoutoa kwa Mhe. Waziri, ili kuona kwamba anafanikisha yale majukumu yake ambayo amepangiwa.

Mhe. Spika, kwa kuanzia kabisa naomba niunge mkono hoja ya Mhe. Makame Mshimba, ambayo amezungumzia kuanzishwa kwa benki ya wanawake. Mhe. Hamza Hassan Juma na yeye akatilia mkazo nikaona na sisi wametunyooshea vidole sana ni vyema na mimi nikasema kuhusu hili.

Kipindi cha nyuma tulisema sana kuhusu uanzishwaji wa benki ya wanawake kwa sababu tuliona kwamba inaweza ikawa ndio utatuzi wa shida za kinamama ambazo zinawakuta za ugumu wa maisha ya kila siku, tulidhani kwamba kuanzishwa kwa benki hii kutakuwa angalau ni mkombozi wa zile shida ambazo zinawakuta kinamama. Kwa hiyo, nami niseme tu Mhe. Waziri wa Fedha, wakati kipindi kile tunaisemea benki hii akasema kwamba serikali hivi sasa haina mtaji wa kutosha. Lakini tukaomba basi angalau wafanye *initiatives* baina yao na ile benki ya wanawake ya Tanzania Bara ili kuona kwamba angalau wanafungua hata tawi kama benki nyengine zilizofanya za kawaida. Kwa hivyo, hili Mhe. Waziri bado tunaomba kwa sababu tunaona benki ya wanawake ikianzishwa itakuwa ni kimbilio la kinamama wengi na itakuwa ni mkombozi wa akinamama.

Mhe. Spika, baada ya kulikazia hilo sasa naomba nianze kwa kuingia katika kitabu hiki cha Mhe. Waziri na naomba nianze na utekelezaji wa malengo ya wizara kwa mwaka 2014/2015. Kiujumla Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kufikia na mengine hadi kupitia malengo ambayo wamejipangia kwa mwaka ule wa 2014/2015. Hili limedhihirishwa katika Idara ya Mikopoo ambapo ilipanga kukopesha shilingi milioni mia tano na utekelezaji halisi idara hii ilikopesha shilingi milioni mia nane na sabiini na tisa zaidi ya lile lengo ambalo wamejipangia.

Kwa hiyo, niipongeze wizara kwa ujumla na idara hii kwa kuvuka lengo, lakini pia waone kwamba uvukaji wa lengo hili umetokana na shida ambazo wananchi wetu wanazo, kwamba ilibidi wakopeshe zaidi ya kile ambacho walijipangia kukopesha. Kwa hiyo, niseme tu, hii inaonesha hali halisi ya ukwasi ambayo wananchi wetu

wanao katika maisha yao ya kila siku hivyo niiombe idara kuwa iendelee kutoa mikopo hii na isichoke kukopesha watu hawa ili kuona kwamba watu wanajikwamua katika maisha yao.

Jengine ambalo nimeliona linaelekea kutia sura ni suala la Baraza la Vijana. Nimpongeze Mhe. Rais kwa kuanzia kwa kumteuwa Katibu Mtendaji wa Baraza hili la Vijana na tayari kwamba Kanuni ziko Ofisi ya Mwanasheria Mkuu zinafanyiwa kazi kwa kukamilisha Kanuni hizi. Mimi niseme kwamba nimtakie kheri Katibu Mtendaji huyo ambaye ameteuliwa na ninaamini kwamba atatutumikia vijana vizuri sana ili kuona yale matatizo yetu yanayotukabili kama ya ajira, madawa ya kulevya, sasa tunapata chombo cha kusemea na hatimaye matatizo haya kuchukuliwa hatua kwa ujumla.

Mhe. Spika, ninalotaka kusisitiza hapa kwamba, basi kwa vile Katibu Mtendaji huyo ameshateuliwa na Kanuni zinaelekea kukamilika kwa Mwanasheria Mkuu, basi tuombe kwamba Baraza hili liharakishwe kuanzishwa rasmi, lakini pia na yale Mabaraza ya Wilaya na Shehia nayo yaharakishwe kuanzishwa ili kuona kwamba vijana wanapata vyombo vyao vya kusema matatizo yao na baadae kuchukuliwa hatua matatizo haya.

Mhe. Spika, nilikuwa najiuliza tu labda Mhe. Waziri, akija anipatia ufafanuzi, kwamba haya Mabaraza nilikuwa najiulia kuwa yataanza yale ya shehia na wilaya halafu lije la Taifa au litaanza Taifa halafu *then* litatoa matawi kuelekea katika wilaya na shehia. Kwa sababu nikiangalia katika mfumo wa chama chetu sisi tunalo Mabaraza ya Vijana na lina utaratibu mzuri tu, kwamba kuna Mabaraza ya Shehia na Mabaraza ya Wilaya ambapo katika wilaya ndio mnatoka wajumbe wa kwenda kwenye Baraza Kuu la Taifa na ni utaratibu mzuri tu, serikali inaweza ikakopia kutoka Chama cha Mapinduzi na kuufuata ule utaratibu ambao umepangiwa vizuri sana. Sio mbaya Mhe. Salim, zuri *copy*, lakini mabaya tu mtuachie.

Kwa hivyo, serikali inaweza ikatizama mfumo ule ambao ni mzuri kabisa ambao utatoa vijana kutoka wilaya na kwenda Taifa ku-*present* vijana wenzao. Hivyo, Mhe Waziri, mimi niseme tu kwamba nimtakie kila la kheri katika hili na nimuombee Katibu Mtendaji kila la kheri katika kuwakilisha vijana wenzake.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo limezungumziwa hapa ni udhalilishwaji wa kijinsia na watoto. Mhe. Spika, na hili pia niipongeze wizara tumeona imechukua jitihada katika hatua mbali mbali kuona kwamba hili tatizo linamalizika.

Hivi karibuni tuliona kwamba Rais naye aliunga mkono jitihada hizi kwa kuanzisha kampeni rasmi za udhalilishaji na ukatili dhidi ya wanawake na watoto

na kuzindua kampeni rasmi ya "Udhalilishaji Sasa Basi", ambayo ilibeba ujumbe mbali mbali ikiwemo kama hiyo "Udhalilishaji Sasa basi", "Mwanamme jasiri hapigi mwanamke" na ujumbe mbali mbali ambao ulibebwa katika kampeni ile. Sasa nimpongeze Mhe. Rais pamoja na wizara hii kwa ujumla kwa kuona kwamba inachukua jitihada mbali mbali kuona kwamba udhalilishaji unamalizika.

Mhe. Spika, kiujumla serikali inajitahidi sana katika kushughulikia suala hili lakini kama tunavyojua kila binadamu ana hulka yake, wengine ni hulka yao tu na kubadilisha hulka ya mtu hiyo nahitaji *degree* ya peke yake, yaani kumbadilisha *mindset* yake. Kwa hiyo, tunaona kwamba kwa jitihada za ujumla serikali inajitahidi kuchukua na wizara tunaiona kabisa inafanya kazi, lakini tatizo lipo katika jamii na niwaombe wanajamii kwamba katika hili sasa tubadilike.

Mhe. Spika, ukina mtu mzima analia ujue kuna kitu, mpaka Mhe. Rais kuingilia hili ujue kwamba ni tatizo. Kwa hivyo, niwaombe tu wale ambao wanaendelea na vitendo hivi waache na kuona kwamba hili tatizo linakwisha katika jamii zetu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, amezungumzia kuhusu hii mashine ya *DNA* na nafikiri katika Wizara ya Katiba na Sheria pia alilizungumzia suala hili lakini kama kawaida yake Mhe. Makame Mshimba, akimaliza kusema hasikilizi majibu. Nafikiri Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri walilitolea ufafanuzi vizuri suala la *DNA*, wakasema kwamba kuna Balozi wa *EU* ambaye ameahidi kuwa ataleta mashine hii. Na mimi niipongeze serikali kwa kuchukua hatua za makusudi kuona kwamba hawa wafadhili wanatusaidia katika hili tatizo na kuona kwamba udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto unaendelea kwisha.

Niseme kwamba, kwa kuwa vile hii mashine haijapatikana bado serikali pia iendelee kuchukua hatua za makusudi kuhimiza hili suala kwa sababu hali ni mbaya ili kuona kwamba ile mashine inakuja na inatusaidia katika kutatua matatizo haya ya udhalilishaji wa watoto.

Jengine ambalo niliseme katika hili kuna tatizo. Wakati Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ana-*wind up* katika hotuba yake alisema kwamba mashine hii tayari tumeshaahidiwa kuwa italetwa, lakini kilichobakia ni kwamba hawajui mashine hii itakwenda katika wizara gani. Kwa sababu imekuwa kama ni suala mtambuka linagusa wizara tofauti; Wizara ya Katiba na Sheria imo, Wizara ya Wanawake na Watoto imo, Wizara ya Afya imo. Kwa hiyo, niseme tu kwamba mimi nadhani serikali ikae ijipange kabla ya hii mashine kuwasili waone kuwa mashine hii ikifika haswa mshughulikiaji atakuwa nani, isije ikawa kama ule mradi wa *e-Government* mkiuliza mawasiliano mnaambiwa nendeni fedha, mkiuliza fedha mnaambiwa aa, iko utumishi, haijulikani iko wapi. Kwa hiyo, na hili nalo

lichukuliwe hatua mapema ili kuona kwamba wakati mashine hii inapowasili tujue nani hasa mhusika ambaye atahusika na mashine hii.

Mhe. Spika, jengine katika hili tuna tatizo la *evidence decree,* yaani sheria ya ushahidi. Sheria ya Ushahidi bado ni tatizo kuna baadhi ya vifungu vinanyima haki wale *victims* ambao wanafanyiwa haya matendo. Kwa hiyo, katika hili niiombe serikali hapa itamke ni lini hasa sheria hii itafanyiwa marekebisho ili kuona kwamba yale mambo madogo madogo ambayo yanapelekea hawa watendaji kuachiwa huru yanawekwa sawa na wale waathirika wanapata haki yao ya msingi ambayo wanatakiwa kuipata zidi ya matendo haya.

Kwa hiyo, niiombe serikali ikija hapa itamke na hili nimwambie Mhe. Waziri. kwa sababu hivi vitendo sana lawama nyingi zinakwenda kwenye Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa sababu wao ndio wahusika. Lakini kuna mambo mengine ambayo katika zile taasisi nyengine ambazo zinatakiwa ndio ziwachukulie hatua ili kuona kwamba haya mambo yanakwisha kuna uzembe kama huo unafanyika. Kwa sababu urekebishaji wa sheria sio kazi ya Wizara ya Uwezeshaji, ingawa nayo inaweza ikaona jambo ika-*propose* kwa Tume ya kurekebisha sheria kwamba kuna hili tatizo. Kwa hivyo, tunaomba sheria hii itizamwe.

Mhe. Hamza Hassan Juma, amemwambia waziri akaze buti na mimi namwambia akaze buti ili kuona kwamba haya mambo madogo madogo ambayo yanasababisha uzembe katika hizi kesi yanatatulika ili na yeye abaki kuwa msafi.

Jengine katika hili nimetizama programu ndogo ya mapambano dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto, kuna shilingi 24,240,000 zimetengwa kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kwa ajili ya kuhamasishwa wana jamii katika shehia mia juu ya kuchukua hatua dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wanawake na watoto.

Mhe. Spika, naendelea kuunga mkono jitihada hizi lakini niseme tu, niiombe wizara iangalie yale maeneo ya *priority*, maeneo ya kuwapa kipaumbele. Kuna maeneo ambayo yamekithiri vitendo hivyo. Kwa hiyo, niombe tu kwanza, najua kwamba hii bajeti baadae mtakuja kusema haikuingia yote, kwa hivyo, kuna badhi ya maeneo hayakufikiwa, hivyo, niseme tu kwa kuanzia waanzie yale maeneo ambayo ni sugu kwa vitendo hivi halafu baadae mengine yatafuata.

Kwa hiyo, niseme kwamba mpango ni mzuri lakini ni vyema wizara ikatizama yale maeneo ambayo ni sugu ili kuona kwamba tatizo hili linapungua na baadae kwisha kabisa.

Mhe. Spika, nikiachana na udhalilishaji na ukatili wa wanawake na watoto, naomba niingie kidogo katika propramu ya kukuza uendelezaji wa wanawake. Katika *paragraph* ya 83 Mhe. Waziri,  amesema kwamba shughuli zinatarajiwa kutekelezwa kwa mwaka 2015/2016 ni pamoja na kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi 50 vya kiuchumi vya wanawake. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri, akija anipatie maelezo katika hili. Kwa sababu kuna vikundi vingi vya wanawake ambavyo vimeanzishwa na bado vyengine kuanzishwa vimeshaanzishwa, lakini uwezeshwaji bado haujawafikia vizuri na katika hili bado tunapanga kuanzisha vikundi 50 vyengine vya kiuchumi vya wanawake.

Hebu labda Mhe. Waziri, ukija unipatie maelezo hivi vikundi 50 vyengine vya wanawake vinautafauti gani na vile ambavyo zimeanzishwa sasa hivi na bado havijapata uwezeshwaji. Kwa sababu naona kwamba kama kunaenda kuanzisha vikundi vyengine wakati kuna vyengine huku nyuma ambavyo havijapata ule uwezeshaji kikamilifu.

Sasa ni vyema kwamba kama viko vikundi vyengine tukavitizama hivi ambavyo vimeanzishwa kwanza zikawezeshwa kisawa sawa, baada ya wao kukaa sawa ndio tukanzisha hivi vikundi 50 vya wanawake ambavyo vinaenda kuanzishwa. Mhe. Spika, malalamiko yamekuwa mengi kwamba vikundi vinaanzishwa lakini huu uwezeshaji hauwafikii vizuri.

Kwa hiyo, naona kwamba kama wizara inaenda kujizonga kuanzisha vikundi vyengine ambapo vyengine ambavyo zimeanzishwa lakini bado havijafikiwa vizuri. Kwa hiyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri, akija anieleze hivi vikundi 50 ambavyo vimeweza kuanzishwa vinautafauti gani na vile ambavyo vimeanzishwa nyuma na vinaendelea kufanya kazi hivi sasa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri asilimia mia kwa mia na naomba wanawake wenzangu waichangie asibaki hata mmoja tuchangie tuwasemee watoto, tuwasemee wanawake ili kuona kwamba zile shinda ambazo zinawakabili basi wizara inazichukulia hatua katika kuzitatua. Mhe. Spika, nakushukuru.

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia machache hotuba ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nichukuwe fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana wataala* kwa kunijaalia leo hii nikaweza kusimama hapa nikiwa katika hali ya uzima.

Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri, mama yangu bi Zainab kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba hii. Pia nichukuwe fursa hii niwapongeze watendaji wote wa wizara hii inayoshughulikia watu muhimu katika nchi hii.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu kwenye Idara hii ya Mikopo. Mhe. Spika, Idara imetoa mikopo elfu moja yenye thamani ya shilingi milioni mia tano kwa vikundi vya kiuchumi na wajasiriamali moja kwa moja katika sekta zote za kiuchumi.

Mhe. Spika, kuongezeka kwa asilimia 85 ya marejesho mwazo ilikuwa ni asilimia 85 za marejesho ya pesa hizi. Lakini hadi kufikiria leo ni asilimia 95 ya marejesho. Namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja aje anambie ni sababu gani zilizopelekea asilimia hii ya marejesho ya mikopo ikaongezeka.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende kwenye uzalilishaji wa kijinsia. Mhe. Spika, uzalilishaji wa kijinsia unakuwa ukiongezeka siku hadi siku na hili Mhe. Spika, tatizo kila baada ya mwaka wa bajeti ya Wizara hii iwezeshaji huwa tunapata malalamiko makubwa ya uzalilishaji wa kijinsia wakiwemo wanawake na watoto na watoto wanaume kulatiwa.

Mhe. Spika, katika kitabu cha Mhe. Waziri, wamesama katika utafiti wao kuangalia watoto katika mazingira magumu wamebaini kuwa ni ndoa zinazovunjika za watoto wadogo, ndoa zinazovunjika za kiholela. Mhe. Waziri, nakuomba utakapokuja uje unambie ni sababu zipi ambazo kuwa zinapelekea ndoa hizi zikawa zinavunjika.

Mhe. Waziri, kwenye kitabu chako umetwambia  umeshughulikia malalamiko ya jamii 132 kwa Unguja na Pemba, Unguja malalamiko 50 na Pemba 82 ya Watoto waliofanyiwa ukatili na udhalilishaji yaliyoripotiwa katika kitengo cha hifadhi ya mtoto cha Idara ya Ustawi wa Jamii kati ya hayo malalamiko 80 yalihusishwa na ukubwa, malalamiko 14 kulawitiwa, malalamiko 15 kukashifiwana 25 kudhoroteshwa walalamikaji walisaidaia kuwasaidia malalamiko hayo katika vyombo vya sheria.

Mhe. Spika, malalamiko haya yanayokuwa yanaendelea siku hadi siku na kila mwaka tunasikia malalamiko haya ya uzalilishaji. Hili ni tatizo katika nchi yetu Mhe. Spika, Mhe. Waziri, nakuomba ukija uje unambie ni kesi ngapi ambazo kuwa zimehukumiwa na zimechukuliwa sheria.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende kwenye Idara ya Maendeleo ya Vijana. Mhe. Spika, nichukuwe fursa hii nimpongeze Mhe. Waziri, kwa kuweza kulifuatilia

vyema kuhusu uundwaji wa Baraza la Vijana Zanzibar. Mhe. Spika, tokea Mhe. Rais wa Zanzibar alipokuja kulizindia Baraza lako tukufu aliahidi uundwaji wa Baraza la Vijana Zanzibar.

Mhe. Spika, niipongeze wizara kwa jitihada kubwa walizozichukuwa mpaka kukamilika kwa Baraza hili angalau kwa hatua chache ambazo kuwa zina muelekeo mzuri wa kuundwa kwa Baraza hili la Vijana Zanzibar. Mhe. Spika, hivi karibuni tunakaribia kuingia katika uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na Baraza hili kama litakuwa halijakamilika uundwaji wake litakuwa limetimiza ahadi ya Rais ya miaka 5.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri, kwa kushirikiana na watendaji wake wote aache mambo yake yote Baraza hili ahakikishe limekamilika. Mwenzangu Mhe. Wanu hafidh Ameir, amesema hapa kama sisi vijana wa Chama cha Mapinduzi tunalo Baraza hili la Vijana na lina muundo mzuri mpaka kupelekea na kuweza kuchaguliwa sisi hapa tukawa Wawakilishi tukaweza kuwawakilisha vijana ndani ya Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo, niende kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii inayoshughulikia wazee. Nichukuwe fursa hii niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuona umuhimu wa wazee wetu. Hii ni hatua nzuri sana kwa serikali kuona wazee wana umuhimu mkubwa sana. Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri, asimamie kikamilifu na watendaji wake posho hili ambalo litatolewa kwa wazee wanaotimiza miaka 70.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono bajeti hii ya Mhe. Waziri, asilimia mia moja. (*Makofi*)

**Mhe. Kazija Khamis Kona:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Wanawake na Watoto.
Mhe. Spika, kwa kweli dakika kumi hazinitoshi lakini nitaenda kwa ufupi ufupi nikiwa sijamalizia utakuja kuniongezea jioni.
Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, kwa jinsi anavyofanya kazi zake pamoja na watendaji wake wote.

Lakini kwa kuanzia mchango wangu naaza na ukurasa wa 24 kitabu hichi kidogo kuangalia namba uangalie kwa makini kwa sababu vina weusi mwingi.
Mhe. Spika, Mhe. Waziri, katika kitabu chake cha namba 24, kifungu 53 naomba nikinukuu;

> "Wizara imepokea na kushughulikia malalamiko 140, 95 Unguja na 45 Pemba yanayohusu maelezi ya watoto kati ya hayo 92 ni ya matunzo na 48 ni ya mvutano wa malezi, wimbi hili kubwa la utelekezwaji wa watoto

linasababisha na uvunjikaji wa ndoa na pia tabia ya baadhi ya akina baba kushindwa kutelekeza majukumu yao."

Mhe. Spika, kwanza hili mimi nataka nikiri moja kwa moja ni kweli wanaume wanapowaacha wanawake huwa wanashindwa kutekeleza majukumu yao hasa kwa kuwahudumia watoto. Sasa Mhe. Spika, ushauri wangu kwa hili nimuombe Mhe. Waziri na anisikilize kwa makini na pia alifanyie kazi. Kwa kuwa mzigo wanaopewa akina mama huwa mzito sana na akina baba hawawashughulikii watoto ipasavyo na wengine hawawashughulikii kabisa. Sasa nimuombe Mhe. Waziri, akae pamoja na Afisi ya Mufti na ya Kadhi pamoja na baadhi ya mashehe katika Mashehia ili kuwapa taaluma wana ndoa waache mtindo huu wa kuacha kiholela holela.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, akifanya hivi basi itapunguza haya malalamiko na pia zitapungua talaka za kiholela, lakini pia na Afisi ya Mufti nayo iangalie inapopelekewa kesi za malalamiko haya ya ndoa huwa hawawaelimishi sana wale wananchi na kuwaingiza katika imani zaidi ili kukaa sawa wengine huamua tu kutoa talaka.

Sasa nayo niombe ichukuwe muda mrefu sana ya kuwaelimisha wale ambao wenye mgogoro ndani ya ndoa kabla ya kutoa maamuzi ya kuachisha zile ndoa zao. Tukifanya hivyo Mhe. Waziri, kwa kweli haya malalamiko yataondoka na watoto wetu watakuwa wanajisikia vizuri na watapata malezi kwa wazazi wao wote wawili.

Lakini pia hapa hapa Mhe. Waziri, kwa kweli akima mama huwa sisi tunapoachiwa hawa watoto tunateseka sana, sasa labda serikali itafute namna ya kwamba hawa wanaume wanapofika hatua ya kuwaacha hawa wake zao lazima kuwe na sheria kidogo inawabana angalau sheria hiyo inambana kwamba lazima baba yule awahudumie watoto wake ipasavyo, tusipofanya hivyo kwa kweli wanawake kila siku tutakuwa tunalalamika na tutakuwa na mzigo mzito, inaweza kuwa pia serikali yetu haijatusaidia itabakia tu kutupigia kelele akina mama wanafanywaje, akina mama wanadhalilishwa. Nalo hili na jumla ya dhalilisho kwa wanawake Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, naenda katika kifungu cha 59, Mhe. Waziri, hapa ulitwambia kwamba wizara ilitoa mafunzo ya siku moja tu ya Sera ya Hifadhi ya Jamii kwa Wenyeviti wa Kamati pamoja na Wajumbe wa Kamati hii inayohusika ya Wanawake na Watoto. Lakini Mhe. Waziri, taaluma kama hii kuitoa kwa Wajumbe wachache tu ni tatizo, kwa sababu ukitoa taaluma kama hii inayohusu jamii nzima na sisi sote ni Wawakilishi, kwa maana hiyo kama umewapa taaluma hii ni wachache, wengi wamekosa.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri, hapa sisi itakuwa hutatutendea haki au hukuwatendea haki wananchi kupitia Wawakilishi wao. Kwa sababu utakapowapa taaluma Wajumbe wote nao wote wamezungukwa na wananchi katika maeneo yao, ikitokea migogoro inayohusu na mambo ya kijamii kule wanaweza na wao kuwapa taaluma. Sasa sijui sababu gani zilizokupelekea hapa ukaamua kuwapa watu wachache tu taaluma hii sisi wengine tukakosa.

Mhe. Spika, niende kifungu cha 57 tunaambiwa kwamba;

> "Wizara itaanza kutoa pencheni ya jamii kwa wazee wote wa Zanzibar Unguja na Pemba wazee ambao waliotimia miaka 70."

Lakini mimi nataka nijue hapa, je, Mhe. Waziri, hapa atatumia utaratibu gani ili wazee hawa wafaidike na pencheni na atahakikisha vipi wazee hawa wanaipata haki hii.

Lakini Mhe. Spika, Idara ya Maendeleo ya Vijana katika ukurasa wa 26 ilijipangia 2014/15 kuhakikisha kuandaa na kuwaunganisha vijana na fursa mbali mbali za kiuchumi zilizopo. Utelezaji sasa, utekelezaji wake unasema wizara imeanzisha vikundi vya vijana na kuwaunganisha na fursa mbali mbali ili kuimairisha shughuli zao za uzalishaji mali. Jumla ya vijana 81 Pemba wamepatiwa mikopo ya kuwasaidia na kuendesha miradi yao na jumuia 13 na vijana wamepatiwa mafunzo ya uandishi na miradi.

Mhe. Spika, hapa mimi nampongeza kidogo tu kwa kuwapatia mafunzo. Lakini kutokana na wimbi la vijana tulilokuwa nalo katika nchi yetu, mimi sijaridhishwa kwamba ni vijana 81 tu, tuna vijana wengi ambao vijana wengine wana uwezo mkubwa, kwa nini wizara yake umewaunganisha vijana 81 na tuna vijana walio wengi katika nchi hii. Halafu pia aje anambie ni vijana wangapi ambao ana dhamira ya kuwaunganisha katika bajeti yake ijayo.

Lakini kwa kweli Mhe. Waziri, kama mimi ni kijana nilie mwanamke hapa nasikitika sana. Kweli nchi hii vijana 81 tu, aah, Mhe. Waziri, uje nifafanulie ili na mimi yanitwange nifahamu. Je, vijana hawa hawajitokezi au bado wizara yako haijawa tayari na mimi ninachokiamini hapa wizara haijawa tayari.

Mhe. Spika, naomba Wajumbe wanapiga makofi sijui muda ushaisha. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Nakushukuru Mhe. Kazija, kwa mchango wako huo na kuunga mkono hoja.

Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa mashirikiano makubwa ya kuendesha shughuli hii na nataka niwakumbushe suala muhimu sana ambalo lipo kwa mujibu wa Katiba. Waheshimiwa Wajumbe na hili nalisema kwa sababu ya umuhimu wa suala zima la kuhudhuria vikao na kuangalia Ibara ya 82, ibara ndogo ya pili inasema;

> "Bila ya kuathiri masharti yaliomo katika kifungu cha 80 cha Katiba hii idadi wa Wajumbe kufanya mkutano..." maana ile kufanya tu mbali ya kuamua "...itakuwa nusu ya Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi."

Sasa Baraza lina Wajumbe 81 nusu yake basi iwe angalau wawe Wajumbe 41 kiilivyo kama hivi sasa mkutano tungevunja mapema, lakini mara nyingi angalau unazingatia wakati wa uamuzi. Wakati wa uamizi kwamba maamuzi yetu lazima yaende kwa mujibu wa taratibu za Katiba tuwe na Wajumbe angalau nusu halafu wengi wataamua kwamba jambo liweko mezani lipite, basi lipite na hiyo itakuwa ndiyo utaratibu wa kidemokrasi kama ilivyo katika ratiba hii chini ya Ibara ya tano.

Kwa hiyo, masuala haya ya mahudhurio Waheshimiwa Wajumbe, ni masuala muhimu sana yanaendana na Katiba,na si suala ambalo tutenge Kanuni kando, hapana, Katiba huwezi ukatenga Kanuni. Kanuni ni ya kwetu lakini katiba ni nchi haiwezi ikatengwa kisehemu chake kando hata wakati mmoja wa chombo hiki. Ila iwe mmerekebisha hiyo Katiba na utaratibu wa kurekebisha Katiba nao una taratibu zake.

Haya nayasema kwa sababu ya kuendeleza na kuhakikisha kwamba Wajumbe tunahudhuria vikao na huo ni wajibu wetu, vyenginevyo, kwa kweli huwa tunakwenda kinyume na taratibu ya Katiba hii na inakuwa hatutekelezi majukumu yetu kama vile tunavyokiwa. Waheshimiwa Wajumbe, wanahimiza sana wananchi hawatutizami vyema juu ya jambo hili. Naomba sana kwamba tuwe tunahudhuria vikao kwa wakati na tushiriki katika shughuli za Baraza hili.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya machache haya basi sasa naakhirisha kikoa hichi hadi saa 11:00 jioni leo.

*(Saa 7:00 mchana kikao kiliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Majadiliano yanaendelea na kwa nafasi ya kwanza jioni hii naomba nimkaribishe Mhe. Mgeni Hassan Juma, afuate baadae Mhe. Shadya Mohammed Suleiman, wakati Mhe.Farida Amour Mohammed, anajitayarisha.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa fursa hii adhimu kuchangia katika Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, kwanza nilikuwa ninamuuliza Mhe. Kazija, kama alikuwa anataka kuendelea kwa sababu ananyanyuka nyanyuka, ndiyo maana uliniona nimechelewa kusimama kwa sababu bado ninamuona alikuwa na hamu ya kuchangia zaidi.

Lakini nitaendelea kwa ruhusa yako Mhe. Spika. Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma ambaye ametujaalia afya njema na kuweza kuja hapa kwa ajili ya kukamilisha shughuli zetu ambazo zimetuleta hapa.

Mhe. Spika, vile vile, nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia. Mhe. Spika, nitaanza kwa pongezi kwa Waziri pamoja na watendaji wake kwa namna ambavyo na niseme kwamba mimi nilikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Wizara hii inayosimamia Wizara hii, kwa hivyo, ninachokizungumza ni jambo ambalo nina uhakika nalo lakini vile vile ni jambo ambalo nimeweza kuli-*experience* katika muda wote nilipokuwa ninafanya kazi nao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninampongeza sana Waziri. Katika kufanya kazi na Wizara mbali mbali, kwanza ninampongeza Waziri kwa sababu kipindi chote ambacho tulikuwa tunakwenda kwenye Kamati, ambapo katika Wizara nyengine tunajikuta kwamba hatumuoni Waziri kwa sababu ya kazi nyengine, lakini Mhe. Waziri, alikuwa anafanya kila mbinu kuhakikisha kwamba anakuwepo ndani ya Kamati kufanya kazi pamoja na Kamati. Ninampongeza sana Mhe. Waziri. Mhe. Spika, lakini ninampongeza vile vile kwa namna ambavyo alivyokuwa anafanya kazi kwa kushirikiana na watendaji wake wote. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Mhe. Waziri Bi. Zainab, Mungu kamjaalia kipaji cha kwamba anaweza kuongoza kuanzia mfanyakazi wa chini kabisa hadi watendaji wa juu kabisa. Na hilo limefanya Wizara ile imekuwa na sioni ajabu kwa sababu yeye ni mama na hizo ndizo sifa za mama kuwa kiongozi bora wa familia. Lakini tumeona wakati wote tunapofanya kazi, kila jambo ambalo linahusu Idara lakini

wafanyakazi wote walikuwa wanalijua na wakati wa kuchangia wote wanachangia kama sauti moja. Niipongeze sana Wizara kwa hili. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Spika, mimi pamoja na yale ambayo yamejitokeza ndani ya maoni ya Kamati, nilikuwa na machache sana ya kusema na zaidi ninataka kujaribu kuangalia namna ambavyo tutaweza kuboresha katika taarifa zetu ambazo zinakuja ndani ya hotuba za Waziri.

Mhe. Spika, kidogo ninafikiri mimi hata na wenzangu wanakuwa wanapata ukakasi na ninafikiria Mheshimiwa, pale Mhe. Kazija, alilizungumzia hili, kidogo aliligusia lakini nilikuwa nimemfahamu vizuri sana. Katika taarifa nyingi ambazo zimetolewa ambazo ni taarifa za kutoa idadi takwimu halisi ya shughuli mbali mbali zikiwemo za mafunzo, zikiwemo shughuli namna walivyowafikia vikundi mbali mbali kwamba taarifa zile zinakuja zinajielezea kama ni idadi ya watu wangapi wameweza kuwafikia. Lakini tukiangalia kwa mfano kuna baadhi ya makundi ambayo ndiyo zaidi Wizara wameya-*target*. Lakini tunataka kutizama ni kwa asilimia ngapi wale ambao tunakusudia kuwa-*target* kwa kuwafikia, ndiyo ambao japo asilimia hamsini. Je, tumewafikia.

Mhe. Spika, ninafikiri ninafahamika vizuri kwamba wakati tunapotoa ripoti tuweze kueleza maendeleo ambayo tumeyafikia yapo kiasi gani kwa kiasilimia. Ninasema mfano huo Mhe. Spika, kwa mfano Wizara imesomesha vijana inavyosema imesomesha vijana sabini na moja. Mhe. Kazija Khamis Kona, alisema vizuri sana, karibu asilimia ninafikiri sitini ya wananchi wote ni vijana. Lakini sasa ikiwa vijana sabini na moja na pengine tuliowakusudia hasa pengine labda wapo vijana kama ishirini na elfu. Ukisema sabini na moja, kidogo inakuwa haina uzito hii sana, lakini ukitoa *in percentage*, tulikuwa tuwafikie vijana mia mbili labda lakini tumewafikia vijana sabini na moja ambao ni asilimia fulani ya vijana ambao tuliokuwa tumewa-*target*. Hiyo italeta picha nzuri zaidi na tutaona tumefikia wapi, hasa katika hii sasa mfumo huu wa *Programme Base Budget*.

Mhe. Spika, mimi ninafikiria ni jambo muhimu sana tuanze kulifikiria na tuone kwamba ili na sisi tuweze sasa kuweza kuishauri Serikali tufanye nini. Lengo ni kuwafikia wale ambao wamekusudia, lakini kwa kiasi gani tumewafikia watu hao na hiyo kwa makundi yote.

Lakini jengine ambalo nimeliona katika suala kwa mfano la ajira. Kuna maeneo ambayo wameweka ajira ambayo pengine labda wameajiriwa watu kumi na saba. Lakini katika wale wamesema tu hawakutoa kwamba ni wanawake au ni wanaume, wamesema tu kwamba ni watu kumi na saba ndiyo wamewaajiriwa. Mimi ningeomba sana Wizara iwe makini sana katika kueleza takwimu za jinsi wakati

ambapo wanatoa taarifa zao. Hilo ni suala jengine ambalo ningeliomba sana Wizara iliangalie.

Lakini vile vile kuna takwimu nyengine ambazo zinakuja zinasema kwamba labda ukiona, unasema labda wamefikiwa wanaume au wamepewa mafunzo wanaume hamsini na wanawake mia moja. Katika wale wanaume hamsini pengine waliokuwepo ni sabini, lakini wanawake wapo elfu moja. Sasa ukilinganisha ukitazama pengine wanawake kwa ukilinganisha kijinsia, wanawake waliopata mafunzo ni kidogo sana kuliko wale wanaume. Kwa maana hiyo bado tutakuwa hatujafikia lile lengo la kuwainua wanawake.

Sasa ningeomba sana katika taarifa zetu ambazo tunazitoa tuangalie na tuweze sasa kujua kutafakari, tutachukua hatua gani nyengine kuhakikisha kwamba huo uwiano unapatikana. Lakini taarifa zi-*base* kwenye uhalisia kwa asilimia zaidi kuliko kuandika katika *data* za tarakimu zile, zitatusaidia sana Mheshimiwa.

Mhe. Spika, lakini jengine ambalo ninataka kulizungumzia ni suala ambalo kwanza nimpongeze sana Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kweli kwa kuweza kutuzindulia rasmi suala zima la udhalilishaji wa watoto. Mhe. Spika, lile lilikuwa ni tatizo kubwa sana na hapa kila mtu alikuwa anajua kwamba tatizo lile kwa kweli lilimuarifu kila mtu katika Taifa hili. (*Makofi*)

Lakini Wizara peke yake kwanza imechukua juhudi kuhakikisha kwamba tunafanya mbinu zote suala hili liweze kutokomezwa, vipi ni suala la kujipanga. Lakini kwa kuwa Rais amelizindua rasmi, kwa hivyo, sasa tumepata nguvu Wizara pamoja na wadau wengine kuweza kulifanyia kazi vizuri. Na niseme niishukuru sana Wizara kwa nje hivi utaliona kwamba hili jambo bado linaendelea, ni kweli lakini Wizara imekuwa ikifanya kazi sana. Kwanza katika suala la kuelimisha. Wizara imefanya kazi kubwa sana ya kuelimisha wakishirikiana na wadau mbali mbali wa maendeleo, kuhakikisha wananchi wanafahamu suala hili na wanafahamu haki zao pindipo wanapopata mambo kama haya.

Lakini kuna vikwazo Mhe. Spika, na hivi vikwazo siyo suala la Wizara moja. Hivi vikwazo ni suala la Wizara nyingi; zaidi ni Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imo, Wizara ya Afya imo. Kwa mashirikiano yanatakikana makubwa sana ili kuhakikisha kwamba suala hili kwetu tumeliondoa kabisa.

Mhe. Spika, kuna suala la sheria zetu ambazo bado zinatukwaza katika kuwapatia haki hawa wahanga ambao wanapata matatizo haya. Mfano mmoja umetolewa leo asubuhi na Mhe. Wanu Hafidh Ameir, kuhusu Sheria ya Ushahidi, haijakaa sawa

kiasi ambacho tunatoa *loophole* ya hawa wanaofanya vitendo hivi wanaendelea kuvifanya.

Ningeiomba sana Serikali tusitoe mwanya huo. Hawa wanaofanya vitendo hivi wanafanya kwa sababu wana njia ya kupenya. Kwa bahati mbaya sana watu wanakuwa wanyonge na wanaondosha imani katika Serikali yao. Mengi ambayo yanafanyika vile vile katika maeneo mbali mbali hasa ya kupewa hizi haki, hayaridhishi wananchi kabisa. (*Makofi*)

Lakini sisi ambao tumejihusisha moja kwa moja na vitendo hivi, pia haturidhiki kwa sababu tunaona. Mhe. Spika, Waziri mwenyewe anafika kwenda mpaka polisi, kwenda kusimamia kesi. Lakini Waziri akifika pale wanamfanya kama siyo Waziri wala hawamtambui. Mimi nimeshakwenda si mara moja wala si mara mbili, inavunja moyo. Watendaji wanakuwa kabisa zile kesi hawazitilii maanani. Kwa hivyo, hili ni suala gumu lakini linatakiwa kufanyiwa kazi. Kama kweli tuna imani na kitendo ambacho amekifanya Rais wetu cha kuzindua rasmi suala hili la kuondosha udhalilishaji wa wanawake na watoto, ningewaomba sana Mawaziri walifanyie kazi, wawe *serious* katika kulifanyia suala hili. (*Makofi*)

Mhe. Spika, lakini jengine mimi nimefurahi kwamba Wizara hii sasa hivi imepewa vile vile nafasi ya kuwa katika maabara inayohusiana na utafiti wa masuala ya utalii. Mhe. Spika, moja katika jambo ambalo linatupa shida sana ni suala zima la maadili kwa vijana wetu. Lakini Wizara hii kwa sababu ndiyo inayoshughulikia vijana imepewa nafasi ya kushiriki katika maabara hii ili kuona namna gani tutaweza kuwasaidia vijana katika masuala ya maadili yao.

Lakini tatizo nililoliona ambalo linasema hapa katika Ibara ya 17, inasema;

> "Wizara kusimamia uandaaji wa utafiti na kuangalia athari za utalii na mmomonyoko wa maadili kwa vijana."

Mhe. Spika, ni sawa Wizara inaweza ikafanya huo utafiti na ikapata matokeo, lakini mengine vijana ndiyo wanaofanyiwa ambao wapo katika sekta ya utalii.Vijana ambao wapo katika sekta ya utalii wanafanyiwa vitendo vichafu na wanashitaki. Lakini Wizara hii ndiyo mama, ndiyo mlezi wa vijana, lazima ishirikishwe ili kuhakikisha kwamba vijana wake wapo salama. Ndani ya yote hayo wapo vijana ambao wanalalamika wanasema tunaambiwa tuvae nguo ambazo sisi hatutaki kuzivaa.

Sasa tunafahamu kwamba maadili yetu yapo vipi. Sasa mimi ninaomba sana Wizara na ninaiomba sana Serikali katika mambo ambayo yataweza kusimamia Wizara hii ni suala hilo la kuwachunga wale vijana wetu ambao wanafanya kazi au

wapo katika maeneo yanayohusiana na sekta ya utalii. Baada ya kufanya huo utafiti wote, hilo ni jambo muhimu Wizara hii kuweza kulisimamia.

Mhe. Spika, ninafikiri katika masuala mengine niseme kwamba Wizara imefanya kazi nzuri sana na niipongeze sana, lakini niipongeze kwa jitihada ambayo wameichukua kuhakikisha kwamba Mfuko wa Wazee unaanzishwa rasmi katika kipindi cha mwaka huu 2015/2016. Niipongeze sana Wizara. (*Makofi*)

Kwa kweli katika watu ambao walifaidika kupata mafunzo mbali mbali ya Wizara kuhusiana na kuanzisha mfuko huu na mimi nilikuwemo. Niseme tu kwamba Mhe. Spika, Wizara hawakukurupuka, walifanya utafiti mkubwa sana ikiwemo kuangalia katika Mataifa mbali mbali, wamechukua mfano mzuri sana ambayo kisiwa kilichofanana na Zanzibar, Mauritius na wameona namna ya wenzetu wanavyoangalia ustawi wa wazee wao. Hiyo ni jitihada ya makusudi. (*Makofi*)

Sasa niipongeze sana Wizara na mimi ninataka kuwatoa wasi wasi wenzangu, hili jambo halikuwa jepesi kwa wao kulifanyia kazi na wanaendelea kufanya kazi hiyo. Lakini hapo tunaanzia, mimi niseme hapo tunaanzia, lakini kuna jengine ambalo mimi ninanikereta Mhe. Spika, naomba nilisema hilo na ninaamini tukenda huko mbele tutaweza kufanya kwa makundi mengine.

Mhe. Spika, kuna makundi mengine ambayo tunayasahau. Kuna familia ambazo zinaishi na walemavu wa kudumu wanataka kusaidiwa. Lakini kuna familia zinaishi na wagonjwa wa akili na kwa bahati mbaya kwa kushindwa kwao Mhe. Spika, pita mitaani huwezi kufika mita kumi usikutana mgonjwa wa akili. Na wale wanaachiwa kwa sababu wazee au familia inashindwa kumudu yule mgonjwa kwa sababu ule ugonjwa hawakutaka wale.

Kwa hivyo, mimi niombe kwamba tujipange kwenda huko mbele, leo tutaweza na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatujaalia tutaweza na hasa bahati mbaya Mhe. Waziri wa Fedha hayupo, lakini hasa tukianza kukusanya mapato kwa kutumia njia ya *electronics*, tukayakusanya mapato yote yasiingie kwenye mifuko ya watu. Tutaweza kuweza mambo yetu muhimu kuweza kuyafanyia kazi.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba Hifadhi ya Jamii inatakiwa ifanywe na Serikali. Sisi wananchi hawawezi kufanya kuhifadhi kutokana na hali tofauti, nyengine za kiuchumi lakini nyengine za uelewa, yote haya yanataka serikali iyasimamie kwa makini na kumfikia kila mwananchi.

Tukianza kulikamata kundi kubwa, ni lazima tuelekee kukamata na makundi mengine madogo madogo, ili basi ustawi wa jamii yetu yote ihakikishe kwamba utakuwa ustawi bora kiafya, lakini vile vile kiakili na mengine yote.

**Mhe. Spika:** Unazo dakika tano.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Spika, nimekusikia na naomba sasa nitamke kwamba naunga mkono hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Mgeni tunakushukuru kwa kuunga mkono hoja hiyo. Nimkaribishe basi Mhe. Shadya Mohammed Suleiman, baadaye Mhe. Farida Amour pia atafuata Mhe. Fatma Mbarouk Said.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia muda huu jioni hii kuweza kuchangia machache katika hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kunipa pumzi zake, na jioni hii nikaweza kusimama hapa katika Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kwanza kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote, kwa kazi nzito za wizara hii wanazozifanya za kuhakikisha kwamba mwanamke na mtoto wanapata haki zao ipasavyo. Chini ya Uongozi shupavu wa Jemedari Naibu Katibu Mkuu Mhe. Msham Abdalla Khamis. Nasema Mhe. Waziri hongera umepata kifaa. *(Makofi).*

Baada ya pongezi hizo Mhe. Spika, naomba uniruhusu nitumie nafasi hii kuzidi kumpa pole na kumuombea kwa Mwenyezi Mungu mwenzetu amzidishie subra, Afisa Mdhamini wa Wizara hii mama yetu Maua aliyepata mtihani wa kufiliwa na mumewe. Tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu amzidishie subra ili arudi aweze kutekeleza majukumu yake katika kufanikisha kazi za nchi yetu na Taifa letu hili kwa jumla.

Mhe. Spika, nikianza mchango wangu, nitaanza katika ukurasa wa 17 unaohusu Idara ya Mikopo. Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kuipongeza wizara, kwa juhudi kubwa wanayoifanya ya kutoa mikopo kwa wananchi wetu mbali mbali, tukizingatia kwamba mahitaji wanayotaka wananchi ni mengi, na pesa inayotiwa kwenye mfuko huu ni chache sana, lakini wananchi wetu wanaweza kufaidika na mkopo huu.

Vile vile Mhe. Spika, niiombe serikali kwamba zile fedha zilizotengwa kwa ajili ya miundombinu, basi zile waingiziwe kwenye hii Idara ya Mikopo ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo na kuwakwamua vijana wetu hawa katika

tegemezi. Kwani Mhe. Spika, ajira sio serikalini tu, ajira ziko nyingi, ndio kama hivi wizara inatoa mikopo na wanaweza wenyewe kufanya vikundi na kuweza kujiwezesha na kupata pesa kuweza kukidhi mahitaji yao ya kila siku.

Mhe. Spika, nikimaliza hapo naomba niende katika ukurasa wa 26. Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba uniruhusu nisome kifungu namba 52.

Kifungu cha 52.

> "Jumla ya malalamiko 132, Unguja 50 na Pemba 82 ya watoto waliofanyiwa ukatili na udhalilishaji yaliripotiwa katika kitengo cha hifadhi ya mtoto na idara ya ustawi wa jamii. Kati ya hayo malalamiko 80 yalihusu kubakwa, 14 kulawitiwa, 15 kukashifiwa na 32 kutoroshwa. Walalamikaji walisaidiwa kuwasilisha malalamiko hayo katika vyombo vya sheria".

Naamini kwamba Mhe. Spika, malalamiko tunaambiwa kila siku yakishafika kwenye vyombo vya sheria, sisi hatupaswi kutia mkono wetu, lakini naomba kidogo Mhe. Waziri anieleze, natambua kwamba watakuwa na wao na mwanasheria wao ambao wanafika katika kusikiliza hizi kesi. Sasa naomba nielezwe, wanapopata ripoti kwa mwanasheria wao wakati anafuatilia hizi kesi, mwenendo wa kesi nzima unatia moyo wa kujua kwamba hawa watuhumiwa wanaweza wakapatiwa adhabu.

Nasema hivyo Mhe. Spika, kwa sababu haya matendo yamekuwa ni mengi sana yamekithiri vibaya sana na sisi kama wazazi tunaumia. Kwa hivyo, nilikuwa namtaka Mhe. Waziri anieleze, wanapopata ripoti kutoka kwa Mwanasheria wao, haya mambo yanatia moyo ya kuweza kuwa hawa wanaofanya ukatili huu, wanaweza kutiwa hatiani na kupewa kifungo kirefu.

Mhe. Spika, naendelea na ukurasa huu huu wa 24, kifungu hiki cha 53. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu ninukuu;

Kifungu cha 53.

> "Wizara imepokea na kushughulikia malalamiko 140, 95 Unguja na 45 Pemba yanayohusu malezi ya watoto. Kati ya hayo 92 ni ya matunzo na 48 ni ya mvutano wa malezi. Wimbi hili kubwa la utelekezwaji wa watoto linasababishwa na kuvunjika kwa ndoa, na pia tabia ya baadhi ya akina baba kushindwa kutekeleza majukumu yao."

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri kidogo anifafanulie. Hawa akina baba wanaotuhumiwa kufanya mambo kama haya, kwa sababu haya mambo ni mengi mno Mhe. Spika, hususan vijijini utayakuta mambo kama haya, baba keshakimbia kamuachia mama watoto, mama anahangaika na kupita kuombaomba. Je, sasa ni hatua gani zilizochukuliwa kwa hawa akina baba wanaowatekeleza watoto wao, ili na wao waweze kushirikiana na hao kinamama waliowaacha kuwatunza watoto hao.

Baada ya hapo Mhe. Spika, naomba niende katika ukurasa wa 26 Idara ya Maendeleo ya Vijana. Mhe. Spika, hapo nilikuwa na ombi. Namuomba Mhe. Waziri katika hili suala zima la maendeleo ya vijana, washirikiane na Wizara ya Elimu ili kuunda vituo vya amali. Kwa sababu Mhe. Spika, vijana wetu wengi sasa hivi wanaomaliza daraza la kumi na mbili, kwa kweli utaona kama kafika darasa la tano, hawezi kujieleza, na wale ukimwambia akuandikie hata barua yake mwenyewe anashindwa kujieleza.

Kwa hivyo, nimuombe waziri washirikiane na hii Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuandaa hivi vyuo vya amali ili watoto wetu hawa wanapomaliza skuli waweze kujiendeleza na wao ili kujikwamua katika harakati zao za kimaisha.

Mhe. Spika, na mimi nitoe pongezi zangu kwa wizara jinsi wanavyolishughulikia suala zima la kuwatunza wazee wetu, kwa kuweza kuwapatia makaazi mazuri, mlo wa uhakika na pia tunasikia kuanzia mwezi huo unaofuata wazee wale watapata posho.

Kwa hivyo, jambo hili ni jambo la kupewa hongera sana na ni la kuonesha mfano kwa wazee wetu watakavyoweza kupata mafanikio haya.

Vile vile nimuombe Mhe. Waziri naye kwa kule upande wa Pemba, hali ya fedha itakaporuhusu, naomba basi angalau na yale majengo ya wazee nayo kidogo yatupiwe macho yaweze kutengenezwa na kuwa katika hali nzuri.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba mchango wangu utakuwa mdogo, naomba mwisho nimalizie na mimi kwa hii benki ya wanawake.

Mhe. Spika, kila mwanamke atakayesimama hapa ataipigia kelele hii benki ya wanawake, kwa sababu kelele zimekuwa nyingi kila siku tunaambiwa benki ya wanawake. Sasa tumuombe Mhe. Waziri amkamate koo Mhe. Waziri wa Fedha, ampe fedha ili benki hii ifunguliwe, na akina mama hawa nao wapate mikopo waweze kujiendeleza katika maisha yao ya kila siku. Kama tunavyofahamu Mhe. Spika, mama ndio kiungo katika nyumba.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan alisema hapa, hakuficha ukweli wao alipochangia asubuhi, kwamba akina baba wakishatoka, akiacha pesa yake hiyo hajui kama imetosha au haikutosha anarudi usiku. Lakini mwanamke hawezi kuamini hivi hivi mpaka ahakikishe watoto wake wamepata chakula kizuri chenye afya na kuweza kukamilisha vizuri.

Kwa hivyo, tumuombe Mhe. Waziri washirikiane na Mhe. Waziri wa Fedha japo hayupo pale, ampe pesa Mhe. Waziri aweze kufungua benki hii ya wanawake, au serikali ifungue benki hii ya wanawake.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Shadya Mohammed, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Farida Amour Mohammed, afuate Mhe. Fatma Mbarouk Said, wakati Mhe. Hussein Ibrahim Makungu anajitayarisha.

**Mhe. Farida Amour Mohammed:** Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi jioni hii kuchangia machache katika hotuba hii ya Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, nataka nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kunifikisha hapa nikiwa na afya njema, na kunipa pumzi ya kuweza kuzungumza haya ninayotaka kuyazungumza.

Pia Mhe. Spika, naomba uniruhusu nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba yake kwa umakini na kwa *speed*, ambayo ulikuwa hufikirii kutokana na umri wake alionao na jinsi alivyowasilisha hotuba hii.

Mhe. Spika, nataka nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, hakukosea kumteua Mhe. Zainab kuwa waziri katika nafasi hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi ni mjumbe wa kamati hii, na ninachotaka kukizungumza hapa chochote nitazungumza kwa uhakika nimekiona kwa macho yangu.

Nataka niipongeze wizara kwa jumla jinsi ya utendaji wake na jinsi tulivyoshirikiana katika miaka miwili na nusu hii ya kunipeleka katika Kamati hii, tumefanya kazi vizuri kama ndugu, hatukufanya kazi kama kamati na wizara. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 8. Mhe. Spika, naomba uniruhusu ninukuu inasema;

Ukurasa wa 8

"Programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano na Shirika la *UN Women*, kwa lengo la kusaidia jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika kuimarisha usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake kiuchumi, kisiasa na kijamii katika mwaka 2014/2015".

Sasa katika hili wizara hii kwa kupitia programu hii imetekeleza mambo muhimu yafuatayo:

Jambo la mwanzo lililo muhimu zaidi ilizindua kampeni ya miaka miwili ya kupiga vita vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia tarehe 06 Disemba, 2014.

Kampeni hiyo ilizinduliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Spika, kwa kweli suala hili la udhalilishaji limekuwa ni kero kubwa ndani ya Taifa letu hili, mpaka Mhe. Rais tunamshukuru kwa kuzindua rasmi kampeni hii ya udhalilishaji, lakini bado udhalilishaji umekuwa ni kero ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, vijana wetu ndio nguvu kazi ya Taifa hili, lakini bado tatizo hili linaendelea siku hadi siku, katika kuwadhalilisha na kuwaumiza vijana wetu ambao ni nguvu kazi ya Taifa hili.

Sasa hapa mimi nataka niombe kidogo, maana yake katika malengo makuu waliyonayo hapa, moja ni kukuza uelewa. Jamii tayari imeshaelewa, jamii imeelewa sana na imefahamu jinsi ya udhalilishaji, jinsi ya kuwajibika na kujua haki zao. Lakini hapa nataka nitoe ombi maalum kwa jamii tushirikiane.

Mhe. Spika, hili sio kwa ajili ya serikali tu, kama jamii hatujashirikiana kwa nguvu moja, wanawake na wanaume na bila ya kujali itikadi ya mtu jinsia na bila ya kujali dini, rangi au kabila. Kama hatujashirikiana kwa hili, itakuwa tatizo gumu na haliondoki.

Mhe. Spika, kwa sababu kuna mambo mengi yanajitokeza ya udhalilishwaji. Waziri wetu kafanya kazi kubwa mno ya kwenda mpaka mwenyewe mpaka kwenye vituo vya polisi, lakini bado tatizo linajitokeza pale pale, tuseme sijui ni dharau, maana yake hatuna uhakika, tuseme labda wale baada ya kwishakufanya yale mambo yao wanatoa rushwa.

Kila pahali tutakwenda kusema kwa sababu tunavunjika moyo, kwa sababu kwa nini kesi hizi kila siku ziwe zinaendelea badala ya kupungua. Kwa hivyo hapa naiomba jamii tushirikiane katika  kulitatua tatizo hili, hili linakuwa kama ni janga ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 10. Mhe. Spika, katika mwaka 2014/2015, wizara katika programu hii imetekeleza mambo yafuatayo. Imetoa mafunzo kwa viongozi wa kidini 84 kwa Unguja na Pemba, juu ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto kwa kutumia miongozo maalum iliyoandaliwa.

Viongozi hao hivi sasa wameanza kuelimisha jamii kwa kupitia mihadhara ya kidini katika maeneo mbali mbali. Mimi hapa naomba niipongeze sana wizara, kwa kuchukua hatua hii ya kuwapa mafunzo hawa viongozi wa kidini, na viongozi wa kidini wakalikubali hili na sasa na wao tayari wanaanza kutoa mihadhara katika maeneo mengine.

Mhe. Spika, naomba niseme kitu kimoja, kwa sababu kuna matatizo hujitokeza kwa baadhi, sisemi wote, lakini wako wachache. Watu wa zamani walisema *kombe ikioza moja basi inaozesha mtungo mzima*.

Sasa kuna baadhi ya hawa viongozi wa madrasa wanafanya matatizo haya ya matukio kuwa makubwa. Sasa sisi kama wananchi wa nchi hii tunaona aibu tukisikia kama kuna mwalimu fulani au taasisi fulani inafanya tendo hili, wakati wao ndio wanatakiwa kuielimisha jamii katika hali kama hii.

Kwa hivyo, naomba sana wao wasiwe chango za kusababisha haya, wao wawe ndio chachu ya kufanya kazi hii kwa nia safi; kwa kutegemea kipato hapa duniani na kesho pia kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuwatetea vijana wetu.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 11, kuna sehemu katika malengo waliyoyaendesha pia imeandaa na kurusha hewani vipindi 32 vya michezo ya redio, unaojulikana kama mshike mshike kwa lengo la kuwaelimisha jamii juu ya kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji.

Mhe. Spika, ni kweli hili ni jambo zuri, lakini nataka niseme, kwa sababu vijijini. Kuna sehemu hapa wamesema katika redio jamii, *ZBC*, Tumbatu na Micheweni, lakini kuna maeneo mengine vijijini watu hawana  hiyo redio na wengine hawana hata huo muda wa kusikiliza redio.

Mhe. Spika, naomba hapa nishauri, kwa sababu zamani kulikuwa na zile sinema za magari. Kwa hivyo, katika michezo hii hii waliyoiandaa, wangetafuta katika vijiji

vile vya ndani ambavyo wanawaona watu hali zao ni ngumu kidogo, basi watafute pengine kama katika mwezi waweke eneo moja, ili watu waone zaidi, pengine wakiona ile hali angalau wataweza kuelimika zaidi.

Mhe. Spika, ukurasa wa 16, katika juhudi za kuwawezesha wananchi kiuchumi, wizara imeanzisha kituo cha kukuza wajasiriamali Mbweni Unguja. Kituo hicho tayari kimeanza kazi, kwa jumla ya wajasiriamali 385.

Kwa hivyo, mimi nataka niwapongeze, kwa sababu mimi mwenyewe binafsi tumekwenda pale na Kamati, na tumewaona wale vijana pale wanafanya kazi vizuri, na tunawapongeza sana walimu wale kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nishauri najua wizara bado bajeti yake ni ndogo, lakini hebu ikiwezekana wafanye utaratibu kama huu katika kisiwa cha pili cha Pemba, na wao wawaandalie lile eneo angalau na wao wapate kujifunza, ili kupunguza ule msongamano wa vijana wetu wote kutoka Pemba kuja hapa kutafuta maeneo ya kujifunza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 17, nataka nitoe pongezi kwa wizara kwa kushirikiana na chuo kilichopo India, kukamilisha ukarabati wa jengo kwa ajili ya kuanzisha kituo cha kuwafunza wanawake kutengeneza vifaa vya umeme. Mhe. Spika, hapa pia sisi tulikwenda.

Naipongeza sana wizara kwa kuwajali wanawake wasiosoma, kwa sababu hawa ni wanawake waliokuwa hawana elimu. Kuna wanawake hata darasa la pili hawajasoma, hawa wamewachukua na kuwapeleka nje, wamewasomesha jinsi ya kutengeneza umeme wa jua na wamewakabidhi nyumba, kila mtu nyumba 100 kwa kufanya mazoezi.

Kwa hivyo, nawapongeza sana katika hili, kwa sababu ya kuwajali wanawake, hivi ndivyo inavyotakiwa serikali kuwajali wananchi wake, sio wale waliosoma tu, hata wale waliokuwa hawana elimu na wao wana mambo wanayoweza kuwafahamisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Mikopo. Naomba niwapongeze kwa kutoa mikopo 100 yenye thamani ya shilingi milioni 500, kwa vikundi vya kiuchumi vya wajasiriamali mmoja mmoja, katika sekta zote za kiuchumi.

Lengo la pili, kuna kuongeza kiwango cha marejesho ya mikopo katika asilimia 85 hadi kufikia asilimia 95. Nataka nizipongeze sana jitihada za Idara hii ya Mikopo kwa kurejesha. Kwa sababu kipindi cha nyuma Mhe. Spika, tulikuwa tunalalamika

sana, kwa sababu watu wakishakopa hawajui maana ya kukopa na kulipa ili na wenzao wapate kukopa. Lakini kwa jitihada za idara hii, wamefanya jitihada nzuri, watu wakikopa wanalipa ili na wenzao na wao wapate kukopa.

Kwa hivyo, naiomba Idara iendelee na hatua hiyo hiyo, ili watu wengi wapate kukopa na wapate kujikwamua kimaisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 24, hapa kuna wizara imepokea na kushughulikia malalamiko 140 Unguja 95 na 45 Pemba. Suala hili hata Mhe. Kazija alilizungumzia,l na Mheshimiwa Mwenyekiti pia alilizungumzia na mimi pia kwa umuhimu wake naomba nilizungumzie kidogo.

Mhe. Spika, jambo kubwa linaloonekana wanawake tunapoachwa na waume wanatutelekeza na watoto, na suala hili baadae ndio linakuja wale watoto wakabakia ni omba omba. Mama anashindwa kuwahudumia watoto, kwa hivyo naomba niwanasihi sana akina baba, akina baba ndio walezi na hata kisheria na kidini wao ndio wamepewa nguvu na wamepewa kila kitu, kwa hivyo nawaomba wastahamili kwani katika ndoa hakuna mema matupu wala hakuna mabaya matupu.

Sasa wajaribu na wao kukaa nao wale wanawake na watakapoamua kuwaacha kwa sababu rizki imekwisha, wasaidiane watoto, kwa sababu mtoto ni malezi ya baba na mama, kinyume na hapa tutabakia na kuwa na watoto wabaya wanaoranda randa ovyo wakibakwa halafu matokeo yake tunatia aibu ndani ya nchi yetu na hata dini zetu kwa jumla. Dini zote zinakataza mambo haya.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 25. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto inaanza kutoa pencheni jamii kwa wazee wote wenye umri wa miaka 70.

Mhe. Spika, hili ni jambo zuri na naipongeza sana Wizara katika hili, lakini pia naomba na mimi niseme katika jamii zetu kwa sababu Serikali imeamua kwa makusudi kuwasaidia wazee wenye umri huu kupata pencheni, pencheni ile isionekane kama sisi sasa watoto tuliozaliwa tukwepe majukumu yetu, kwa hivyo ninaiomba jamii, naomba vijana wenzangu na watu wazima waliokuwa bado wana wazazi wao, hii tuone kama ni motisha tu ya Serikali lakini bado tuendelee na majukumu yetu ya kulea wazazi wetu kama walivyotulea.

Mhe. Spika, nikiendelea kuna idadi Wizara imepokea madai 24; Unguja 11 na Pemba 13. Fidia kwa wafanyakazi waliopatwa na ajali kazini. Hili ni jambo zuri na naipongeza Wizara kwa sababu katika kipindi cha nyuma walikuwa na deni kubwa sana. Wizara hii watu waliokuwa wamepata ajali kazini mpaka kwa bahati njema

kwa majukumu makubwa na jitihada kubwa tuliyoifanya pamoja na Wizara wakashirikiana na Wizara ya fedha na kulipwa fidia ile yote iliyobakia ni chache mno, nawapongeza na Mwenyezi Mungu awazidishie imani.

Pia naomba niwapongeze kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuzika maiti zisizokuwa na wenyewe, hili ni jambo kubwa ndani ya nchi yetu; unapata hapa duniani na kesho pia mbele ya Mungu unapomstiri mwenzio.

**Mhe. Spika:** Umebakiwa na dakika tano.

**Mhe. Farida Amour Mohammed:** Ahsante namalizia Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nije katika suala la mwisho kwenye Baraza la Vijana. Wenzangu wamesema sana hapa kwenye Mabaraza ya Vijana. Mimi si kijana tena lakini vijana bado wapo, na kwa vile sheria hii imepitishwa, na kama sheria ilivyozungumza tumeipitisha hapa hapa ndani ya Baraza hili sasa haya Mabaraza yaendelee kuundwa na wenzangu walitoa mifano hapa wachukue mifano katika Chama cha Mapinduzi, yako Mabaraza haya, na sisi pia katika Chama cha *CUF* yako Mabaraza na yameanza katika ngazi za tawi, ngazi za Majimbo, hadi Wilaya mpaka Taifa.

Kwa hivyo Serikali inaweza tu kupitia Wizara hii kuchukua mfano wa kuundwa yale Mabaraza yetu yafanye kazi vizuri bila ya ubaguzi wa kuchagua huyu katoka chama hichi huyu katoka chama hichi, ili kupata ufanisi katika kufanya shughuli zetu.

Mhe. Spika, juu ya kuwa umenihimiza lakini nina suala moja la mwisho naomba uniruhusu nilimalizie katika kuundwa kwa Mabaraza ya Watoto. Tulikwenda kutembelea pale Pemba tukayaona mabaraza ya watoto watoto wenye umri mdogo katika baadhi ya shehia, wale vijana wadogo lakini wana mwamko mzuri wameelimika na wanawaelimisha vijana wenzao mpaka kufikia wakati kuwarudisha skuli ambao wametoroka skuli kwa muda mrefu.

Kwa hivyo naiomba Wizara iendelee na kuwahamasisha vijana katika maeneo tofauti kuundwa yale Mabaraza ya Watoto ili kuwapunguzia watoto zile ajira za watoto kwenda kufanyishwa kazi zisizokuwa zao.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wanawake wa Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja, na nawashauri wanawake wenzangu wote waichangie na waipitishe ili tufanikishe suala letu hili katika Wizara. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii siku ya leo na saa hizi nikachangia machache katika hotuba hii ya Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Pia nichukue fursa hii kumshukuru Waziri pamoja na watendaji wake kwa ufanisi mzuri katika kushirikiana kwa pamoja kusimamia Mapato na Matumizi kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, pia kwa heshima kubwa sana nimshukuru na kumpongeza Mwenyekiti wa Uwawaza kwa juhudi kubwa alizozichukua kwa kushirikiana na Jumuiya ya *Reclaim Women's Space in World Heritage* kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la *Search For Common Ground* kwa kutuendesha vizuri sana kwenye mafunzo ya uongozi yaliyotolewa kwa ajili ya Wajumbe wanawake.

Mhe. Spika, kusema kweli Wizara hii ina majukumu na majukumu mazito na ya msingi yanayogusa jamii moja kwa moja. Mimi niende moja kwa moja kwenye Idara za Wizara hii zote kwa ujumla na majukumu yake mazito, niombe Serikali ili zifanye kazi idara hizo ni kuzipatia fedha kwa wakati.

Kwa kweli kama nilivyosema na wenzangu wameshasema sana, kwamba Wizara hii inaendeshwa na Mwanamama shupavu ambaye anastahili sifa zote, na nimuombe Mwenyezi Mungu ampe uwezo zaidi ili aweze kuiongoza Wizara hii.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja kwenye Idara hii ya Mipango na Sera ambayo katika utekelezaji wa malengo ya mwaka 2014/15 imeweza kusimamia uandaaji wa utafiti wa kuangalia athari za utalii na mmong'onyoko wa maadili kwa vijana. Kwa kweli hili Mhe. Spika, ni jambo la busara sana, kwani tumeona namna gani watoto wetu wanavyoporomoka kimaadili, kwa hivyo hili ni jambo la msingi sana.

Mhe. Spika, nikienda mbele nishukuru vile vile Idara ya Mipango katika utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Mipango Sera na Utafiti kwa mwaka 2014/15 imeweza kukamilisha rasimu ya sera ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi na ipo katika mchakato sasa hivi, kwa hivyo niishukuru sana Idara hiyo.

Vile vile Mhe. Waziri ametueleza hapa kwamba Wizara imewapatia mafunzo watendaji 70; 35 Unguja na 35 Pemba kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufuatiliaji na tathmini. Aidha jumla ya wafanyakazi 35 wa Ofisi ya Pemba wamepatiwa mafunzo juu ya uandishi na uendeshaji wa miradi. Nimuulize Mhe. Waziri katika hawa ni wanawake wangapi ambao wamepata mafunzo haya.

Mhe. Spika, utekelezaji wa programu zinazosimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kuna moja ni hii programu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji

Wanawake, hii ni programu nzuri na ambayo tunapata mashirikiano kutoka *UN Women*, kwa lengo la kusaidia jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuwawezesha wanawake kiuchumi, kisiasa kijamii katika mwaka 2014/15. Niipongeze sana Idara hii ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kufikia malengo ya namna hii.

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi vile vile ina mambo mengi na moja katika hayo ni kusimamia shughuli za kila siku za uendeshaji. Hii ni Idara ambayo ni muhimu na inakuwa ina mambo mengi, hata Waziri ukimkuta mambo mengi anakuwa anapata kwenye maeneo haya, kwa hivyo ni lazima zile pesa ambazo zinaingizwa basi ziwe za kutosha kwa sababu hata Mhe. Waziri mwenyewe anakuwepo hapa, hata na Katibu Mkuu pengine ni hasa ndio ilivyo kwamba anakuwa anasimamia kwa hapa mambo yake mengi yanakuwa yanapatikana hapa.

Kwa hivyo niwatake tu kusimamia vizuri fedha hizo ambazo zinaingizwa, kwa sababu Katibu Mwenyewe ndio anakuwa ndio mas-uli wa masuala haya, kwa hivyo zile sheria za manunuzi zote pamoja na Sheria za fedha basi wazifuate vizuri ili kuwe na ufanisi mzuri.

Mhe. Spika, pia Idara hii ina majukumu vile vile kuendelea kuviimarisha vitengo vya Ununuzi, Uhasibu na Ukaguzi wa ndani. Kwa kweli kama hakutokuwa na uimara wa vitengo hivi kwa kweli itakuwa hata hii pesa ambayo imekusudiwa itakuwa haitotumika vizuri, basi kutakuwa na mapungufu mengi na ni lazima tuwe na *working plan;* ndilo litakaloturahisishia kazi zetu.

Kwa hivyo niishukuru sana Idara hii, lakini vile vile Idara hii ambayo ni idara ya uendelezaji na uratibu wa programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi ambayo vile vile ina mambo kwa mwaka 2014/15 Idara hii ilijipangia kufanya yafuatayo;

Kuandaa mafunzo ya ujasiriamali katika maeneo tofauti ya vijana wahitimu wa vyuo na vikundi vya kiuchumi. Kwa kweli kama walivyokwisha kusema wenzangu vijana ndio tegemeo la Taifa, kwa hivyo ni lazima Serikali kupitia kwa vijana basi iweze kuwawezesha vizuri sana, pamoja na hao wahitimu wa vyuo na vikundi vya kiuchumi. Kwa kweli hii ni dhana nzuri sana, kuwasaidia vijana. Vijana wetu wa leo ndio viongozi wa kesho.

Mhe. Spika, Idara ya Mikopo imeweza kutoa Mikopo 1000 yenye thamani ya shilingi milioni 500 kwa vikundi vya kiuchumi na wajasiriamali mmoja mmoja katika sekta zote za kiuchumi. Niwaaidhi tu hawa wanaochukua mikopo waweze kurejesha mikopo kwa wakati, kwani kama watarejesha mikopo hii kwa wakati basi tutaweza kutoa mikopo mingi na watu wetu wengi watapata mikopo, hii ili kujinasua na hali ngumu ya kiuchumi.

Mhe. Spika, wenzangu wamezungumza mambo mengi na sitaki kurejea rejea lakini vile vile nitilie mkazo wa wale ambao wanawanyanyasa watoto basi kuanzia sasa, kwa kuwa Rais wetu ameshazindua ile sera ya kuondosha kunyanyaswa kwa mtoto, kwa hivyo nitilie mkazo tu na sheria zifuatwe.

Wenzangu pia walisema kuhusu kumdhalilisha mtoto kile kifaa cha *DNA* ikiwa hakitopatikana, na wala mpaka sasa hivi haionekani kwamba kitapatikana. Hebu nimuulize Mhe. Waziri kweli kama hakikupatikana hichi kifaa kutakuwa hakuna chochote kinachoendelea juu ya mambo haya.

Kwa hivyo lazima tuone sasa tunabadilika namna gani ikiwa hiki kifaa kimekuwa ni tatizo basi tutafute hili hili, madam mwenyewe mtoto ameshasema na ameshaonekana kwamba kaharibiwa, na haiwezekani jambo limetendeka likawa halikutendeka, kama limeshaonekana na mtoto ushahidi akatizamwa akaonekana basi iwe ndio ushahidi tosha iweze kuchukuliwa hatua. Si kweli mtoto ana akili yake asiweze kujua nani kamfanyia jambo hili, kwa hivyo ni lazima hili jambo tulititilie mkazo sana, ili haya matatizo yaondoke.

Mhe. Spika, niishukuru Serikali kwa kushirikiana na taasisi za vijana kwa kutoa mafunzo ya stadi za maisha kwa taasisi za vijana Unguja na Pemba. Jumla ya vijana 72; Unguja 36 na Pemba 36. Kwa kweli ni kazi kubwa sana ambayo imefanywa, kwani ukitaka kumfahamisha mtu au ukitaka kumtoa mtu katika ujinga basi kwanza, au ukitaka kumfanyia jambo lolote ili afanikiwe vizuri kwanza umpe mafunzo ya kutosha. Kwa hivyo hili ni jambo ambalo Wizara hii imelifanya kwa mustakbali ule ule na njia ile ile ya kufanikisha na kuwapenda vijana.

Mhe. Spika, niishukuru Serikali kwa mwaka huu wa bajeti kuanza mfumo huu wa programu. Kwa kweli ni mfumo mzuri kwa kuboresha uwezo wa Serikali katika mgawanyo wa rasilimali zake kulingana na vipaumbele vya sera ya nchi. Ninachokiomba kwamba zile fedha zipatikane kwa wakati, kwani Serikali sasa kupitia mpango huu wa programu ni kurahisha na kutumia rasilimali za nchi kwa ubora na ufanisi wa kuhusisha gharama za matokeo yaliyotarajiwa na thamani halisi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, baada ya kusema hayo niseme kwamba naunga mkono hotuba hii ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Mhe. Spika, nakushukuru. Kwanza awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuwa katika afya njema jioni hii. Aidha nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba

ya Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2015/16.

Kwanza Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri, Bi Zainab Omar Mohammed kwa umakini wake mkubwa katika wizara hii. Nimpongeze sana kwa juhudi yake aliyoionesha katika kipindi chake hichi.

Nawapongeza pia watendaji wake wote kwa juhudi zao walizofanya katika Wizara yake hii, lakini pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati hii na watendaji wake wote na Wajumbe wake wote kwa kazi yao kubwa na hotuba yao nzuri waliyoitoa hapa kwenye kuchangia katika bajeti hii.

Mhe. Spika, sasa nianzie kwenye ukurasa wa 10. Niipongeze sana Serikali kwa juhudi zake, Wizara imefanya zoezi la kuvitambua vikundi vya wanawake vya kiuchumi Unguja na Pemba jumla vikundi 1,560 lakini Pemba peke yake 642 na Unguja 918.

Mimi nasema Serikali naipongeza, kwa sababu imeangalia umuhimu mkubwa na hapa imeangalia sana vikundi hivi kwa ajili ya wanawake, ndio maana nikasema Serikali kwa kuwaona wanawake wamewapa kipaumbele kwa kuvitambua vikundi vyao, jumla ni vikundi 1560 vilivyopo Unguja na Pemba. Mhe. Spika, wazo ni zuri walioliona kwa kuvitambua vikundi vya wanawake. Mimi nasema wanawake ni lazima wawezeshwe, bila ya kuwawezesha wananchi itakuwa ni tatizo sana katika maisha yao.

Mhe. Spika, mimi niseme wanawake mara nyingi kazi ngumu wanakuwa hawawezi kufanya angalau wanaume. Mimi binafsi nikiona mwanamke anabeba zege au anafanya kazi nzito kwa kweli inaniuma sana roho yangu. Lakini nikimuona mwanamme anabeba zege, hizi ni kazi za kawaida kwa wanaume. Kwa hiyo wanawake naomba sana wapewe kipaumbele.

Kama alivyoandika Mhe. Waziri katika kitabu chake vikundi 1560 Pemba na Unguja. Kwa kweli mimi naomba uongeze juhudi yako kwa kuangalia vikundi hivi, ili kuwapa vipaumbele zaidi wanawake.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 17, kifungu 34 Idara ya Mikopo. Kutoa mikopo 1000 yenye thamani ya Sh. 500 milioni/- kwa vikundi vya kiuchumi kwa wajasiri amali mmoja mmoja katika sekta za kiuchumi.

Kwanza mimi niipongeze sana serikali kutoa hizi fedha kwa kikundi, kwani fedha hizi ukizigawa kwa vikundi hivi 1000 basi kila kikundi kitapata shilingi milioni moja. Mimi nawashukuru sana wizara kwa kuwa na juhudi hii ambayo inafaa na

nzuri, nawaunga mkono. Naamini milioni moja kwa vikundi vyetu itawasaidia sana katika kuwezesha kazi zao za kila siku katika kujipatia riziki zao.

Naamini Serikali yetu ya Zanzibar ikipata fedha nyingi naamini mwakani inaweza kufikisha hata elfu mbili au elfu tatu, kwa mwaka huu tumeanza na elfu moja. Lakini naamini kwa nia nzuri na nia njema ya serikali hii tutaongeza mpaka vikundi elfu mbili kwa mwakani.

Mhe. Spika, nije kwenye suala jengine hili la kuongeza kiwango cha marejesho ya mikopo kwa asilimi 85 hadi zaidi ya asilimia 95.

Mhe. Spika niipongeze sana serikali na wizara kwa juhudi zao, kwani mikopo hiyo wanavyoitoa wanaichukua wananchi lakini marejesho yao yanaonesha hapa yanaendelea vizuri imeongezeka asilimia 10 kwa marejesho hayo. Naamini itafika wakati watarejesha mikopo hii kwa vizuri.

Lengo kuu la serikali kuwawezesha wale wananchi wote waweze kupata mikopo hii ili waweze kukidhi maisha yao na kupata kazi za kudumu katika maisha yao ya kila siku. Mhe. Spika, hii inaonesha dalili nzuri kuwa hii mikopo inakwenda na inarudi kwa wakati na inaweza kuendelea na watu wengine wakapata baadaye.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 18 kifungu cha 36. Hii Mhe. Spika, napenda niipongeze sana serikali. Mimi kwa kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar naiamini na naipongeza kila siku, kwa sababu juhudi zake na malengo yake yanakwenda kwa vile yanavyotakiwa na wakati huu, tatizo kubwa inakuwa ni fedha tu. Lakini naamini tukipata fedha serikali hii itafanya kazi vizuri kwa kuwatumikia wananchi wake kwa nia njema kabisa.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu nimeona hapa kwenye fungu la 66 wizara imeweka dhamana ya fedha *guarantee pound* ya shilingi milioni 150, katika benki ya *CRDB* ili itoe mikopo kwa vijana kupitia SACCOSS zao Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, nimesema hii ni ishara nzuri sana. Ukitizama hali ya ugawanyo hata hii mikopo inakwenda vizuri, kila zikipatikana fedha basi utakuta Pemba kuna asilimia fulani inapelekwa na Unguja zinapelekwa. Inaonesha ishara wazi kabisa haya mashirikiano ni mazuri ya kindugu, ya kijamaa na kirafiki kabisa. Kila inapotokea neema basi wenzetu wa Pemba na wao wanafaidika katika neema hiyo na Unguja pia. Kwa hivyo naishukuru sana serikali kwa mpango huu, na iendelee kugawa mpango huu, ikitokea keki kama hii, au zikitokea fedha kama hizi basi ziende kwa pande zote mbili.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Mei 2015 Benki ya *CRDB* imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 400 kwa vikundi mbali mbali, jumla ni vikundi 142 kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mimi napongeza sana serikali kwa juhudi zake na kwa kutimizama uwiano wa Pemba na Unguja. Pia niipongeze sana hii Benki ya *CRDB* kwa kutoa milioni 400 kwa mkopo. Kwa kweli hiyo ni juhudi kubwa na naomba na benki nyengine pia waige mfano huu kuweza kusaidia vikundi hivi, kila inapotokezea bahati kama hii ya kupata mikopo ya serikali basi naomba benki zisaidie.

Mfano mzuri wa *CRDB* wa kusaidia milioni 400 kwa vikundi vyote vya Unguja na Pemba. Mimi naipongeza sana serikali kwa mashirikiano yake hayo na mabenki na iende kila baada ya awamu tuwe na mashirikiano mazuri na mabenki ili viweze kufaidia vikundi vyetu hivi vya wajasiriamali hawa.

Mhe. Spika, nikiacha hapo twende kwenye ukurasa wa 20 kifungu cha 39. Ukitizama serikali yetu ya Zanzibar Mhe. Spika, kwa kweli fedha kidogo tunazo, lakini jitihada kubwa ya serikali yetu na viongozi wetu walivyokuwa na imani ya nchi hii na wananchi wake, wizara imewekeza katika Benki ya Watu wa Zanzibar jumla ya shilingi milioni 800 kutoka mfuko wa uwezeshaji.

Hii ni ishara tosha kabisa kuonesha Mhe. Waziri una moyo wa imani kabisa kuwekeza katika Benki na wewe baadaye upate mikopo kuweza kuwafaidisha wananchi wetu. Mimi naamini tutafika mbali sana Mhe. Waziri kwa juhudi zako hizi unazopiga hatua kwa kutafuta mikopo kila aina ya Benki kwenda na kupata kuwekeza na baadaye kukopa. Kwa sababu Benki kama hujawekeza na wewe huwezi kukopeshwa, ili kuweza kufaidisha wananchi wetu waliokuwa wanyonge na masikini katika nchi yetu. Kwa hivyo nakupongeza sana Mhe. Waziri kwa juhudi yako nzuri unayoitumia katika Wizara hii.

Mhe. Spika, mimi kama nilivyosema mwanzo, mimi naiamini sana serikali na naamini malengo haya yatafika mbali, na kuna siku hapa tutafika kiwango ambacho maisha ya ndugu zetu wa Zanzibar hapa itakuwa mtu anaishi kwa siku haipungui dola tano. Kwa hivyo naamini maisha yatapanda na wajasiriamali wakiwa wengi basi watafanya kazi vizuri sana ili waweze kujikomboa katika maisha yao.

Mhe. Spika, nikija katika ukurasa 23 kifungu cha 50, Idara ya Ustawi wa Jamii kuimarisha mfumo wa hifadhi ya watoto. Kifungu hichi kinasema jumla ya malalamiko 132; Unguja 50 na Pemba 82, hili ni ongezeko kubwa sana.

Mhe. Spika, naendelea na malalamiko haya ya watoto waliofanyiwa ukatili na udhalilishaji. Jambo hili ni baya na kubwa sana, na ni aibu kwa mila na silka za Mzanzibari kufanya mambo kama hayo.

Kati ya malalamiko hayo 80 ni kesi za ubakaji na 14 kesi za kulawitiwa. Mheshimiwa mimi inaniuma sana, mtoto mdogo kama hivi kubakwa au kulawitiwa. Serikali ina jitihada kubwa sana kuwasomesha watoto wake ili waweze kusoma, waweze kufikia malengo mazuri ili waweze kuwa viongozi wa Taifa la kesho kuongoza nchi hii vizuri.

Ninavyojua mimi katika ufahamu wa mtoto, mtoto wa kuanzia miaka minne na kuendelea akili yake ndiyo inafunguka ndiyo wanavyotwambia wanasayansi, anapata ile hali halisi ya sehemu husika kujua kila kitu kuanzia miaka minne.

Mtoto yule akianza kufanyiwa jambo lolote baya hasa kama hili la kulawitiwa au kubakwa yule mtoto unamchanganya kwenye maisha yake yote. Hatokuwa tena mtoto yule mzuri katika jamii au hatokuwa na faida katika jamii, utakuwa umeshamuharibu saikolojia yake yote.

Mhe. Spika, mimi naiomba sana serikali tuliangalie sana suala hili na tuweze kulidhibiti vya kutosha. Lakini mimi niseme nasikitika sana hii mashine ya *DNA* mpaka leo tunashindwa kuipata lakini tunaambiwa hapa wafadhili wa kutaka kutununulia itakuja, lakini mpaka leo bado. Lakini serikali ikitaka haishindwi, tumeweza kununua meli ya dola milioni 38, tushindwe kununua chombo hichi cha *DNA*, ili kuweza kuwagundua hawa watu wenye tabia mbaya kama hizi. Tumeweza kujenga jengo jipya hapo *Airport*, la dola milioni mia moja na zaidi, sidhani kama tutashindwa kununua chombo.

Tukiangalia nia ya serikali yetu, nia ya Rais wetu wa Zanzibar kaondosha mita zote kwenye vianzio vya maji na kulipa kila mwezi milioni 500. Hili jambo kubwa sana Rais wetu kalifanya. Kwa hivyo mimi naamini na hii kanunua *DNA* mashine hata kama wafadhili hawajaweza kuleta mashine hii mimi naomba Mhe. Spika, serikali ifanye kila jitihada iweze kununua ili tuweze kuwakamata hawa wahalifu. Suala hili la udhalilishaji ni baya sana, kila siku tukienda mbele suala hili linajitokeza. Mimi nitoe mfano mmoja mzuri.

Mhe. Spika, kuna kipindi kabla sijachaguliwa kuwa Mwakilishi nilikuwa nimekaa Darajani watoto watatu walikuwa wanakwenda Bububu. Kufika pale Darajani wakapanda daladala, yule utingo akawasukuma watoto wale. Mimi nikawa nipo karibu, nikamuuliza kwa nini unawasukuma watoto. Akasema nawasukuma kwa sababu wawili nimeshawapakia na nikiwapakia na hawa watakuwa watano, hiyo itakuwa haiwezekani kwa sababu mimi nitakosa fedha na tajiri anataka pesa zake.

Mimi nikawalipia wale watoto fedha, lakini nikasema pale pale. Mimi nikija nikipata uongozi au nikija nikipata uwakilishi basi mimi nitawanunulia watoto hawa basi, na ahadi yangu itakuwa ni kutekeleza kweli kweli sio mchezo. Sitaki kuona hawa watoto wanapata tabu.

Mhe. Spika, mimi mpaka leo ninavyokwambia hivi sasa akili yangu yote ipo Darajani, hakikisha watoto wangu wote wanaingia kwenye basi wanakwenda kwao. Sitaki kuona mtoto anadhalilishwa pale kwa ajili apate elimu bora, na aweze kujua usafiri napata wa kwenda skuli na kurudi nyumbani kila siku.

Mtoto huyu Mhe. Spika, sio kwa ajili yangu, Mheshimiwa mtoto huyu atakuja kusoma na atakuja kulitumikia Taifa hili, na tunawategemea sana hawa watoto. Hii ni moja ya kuisaidia serikali yetu ili hawa watoto waweze kusoma. Mimi naipongeza serikali kwa juhudi zake hizi kubwa wanazozifanya kwa kuongeza maskuli kila sehemu ili watoto wapate elimu na kuweza kusoma kwa uzuri.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 23 kifungu cha 53, kuimarisha hifadhi ya wazee. Mimi niipongeze serikali sana kwa juhudi zake kubwa katika kuona suala hili ni muhimu sana na hawa wazee wetu wana hali ngumu ya kimaisha.

Kwa hivyo katika wizara yetu inaendelea kuwahudumia jumla ya wazee 91 kwa kuweza kuwashughulikia wakiwa Sebleni 46 na Welezo 37. Pia niipongeze serikali kwa juhudi zake kubwa kwa kuona suala hili la wazee waliofikia miaka 70 kuwalipa pencheni.

Mimi nashukuru sana kwa wazo hili la serikali na hili ni jambo muhimu sana, na naomba suala hili liendelee ili tuweze kufikia katika malengo mazuri kwa wananchi wetu hawa ambao ni wazee, tukawaweka katika hali nzuri kabisa.

Mimi nashukuru sana na mimi napongeza sana na naiunga mkono wizara hii au bajeti hii asilimia mia kwa mia. Nashukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa muda wako.

**Mhe. Abdi Mosi Kombo:** *Bismillahi Rahmaani Rahiim*. Mhe. Spika, awali ya yote na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kwa kutufikisha mpaka sasa hivi na akatujaalia kuendelea katika Bunge letu hili Tukufu.

Mhe. Spika, na mimi nakupongeza vile vile kwa kunipa fursa hii kwa hivi sasa ili kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Waziri Bi Zainab ingelikuwa tupo jeshini tungempa cheo cha *brigadier*. Watendaji wake tungewapa vyeo vya ukanali kwa jinsi ya kazi kubwa waliyoifanya juu ya kuwashirikisha na kuwasomesha wanajamii wanawake na watoto jinsi ya kujiendeleza katika maisha.

Mhe. Spika, nikiendelea katika mchango wangu nakwenda katika ukurasa wa 20 Idara ya Ushirika. Naomba kukariri katika kifungu hichi cha 41.

> "Mhe. Spika, Idara ya Ushirika katika kipindi cha mwaka wa 2014/2015 ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:
>
> 1. Kukuza uwezo wa ushindani wa vyama vya ushirika kumi (10) ili vitoe huduma kwenye soko la utalii ifikapo Juni 2015;

Mhe. Spika, mimi naipongeza wizara, naiomba wizara katika shirika hizi ambazo walizozichagua ziwezeshe ili wawe na uwezo wa kuweza kufanya biashara katika masoko yetu haya ya utalii. Kwa hivyo katika kuranda kwetu na kutembelea katika wizara hii tuliona kwamba bado wizara hii bajeti yake ni ndogo.

Kwa hivyo naiomba serikali kupitia Wizara ya Fedha, mama Zainab wampe fedha ili wastawishe vikundi vya ushirika. Kwa sababu wizara yetu hii imechukua jamii zote; wanawake, watoto, vijana na sisi watu wazima tunaoitwa leo ma-*baby*, vile vile tumo katika wizara hii. Mimi naiomba serikali imzidishie bajeti mama Zainab ili atuwezeshe.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 20 Ibara ya 61 maendeleo ya vijana. Hivi sasa tuna vijana wengi sana na vijana hivi sasa ndio watenda nguvu. Kwa hivyo naiomba wizara wawezeshwe vijana kiuchumi na wapewe elimu ya kutosha katika kujiendeleza maendeleo yao. Hivi sasa tuna vijana wengi, hasa vijana na wanawake wameshazidi sasa hivi. Wanawake wameshatuzidi na vijana wameshatuzidi. Kwa hivyo hawa wote wanahitaji kuwezeshwa hivi sasa.

Mhe. Spika, nakwenda katika Ibara ya 67; Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Mheshimiwa sasa hivi hapa tunao wanawake, tunao watoto. Watoto hivi sasa wanawategemea akina mama na akina baba. Lakini sasa akina mama hawa ndio walezi wa watoto wetu, kwa hivyo wizara iwatizame sana akina mama kuwawezesha, iwatizame sana akina mama kuwakopesha, iwatizame sana akina mama kuwafungulia miradi ili wapate kujiwezesha ili wapate kulea watoto hawa. Kwa sababu mama kutwa yupo na mtoto, mtoto anataka kushiba kwa mama, mama akiwa hana shibe na mtoto hatopata kushiba. Kwa hivyo naiomba Wizara ihakikishe kuwasaidia akina mama zaidi.

Katika nchi yetu kuna akina mama wajane na ni wajasiriamali. Kwa hivyo naiomba wizara kupitia mama Zainab *brigadier,* mimi namwita mama *brigadier* kwa sababu lazima nimwite *brigadier* kwa ufanisi wake wa kazi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ili akina mama waendelee lazima wasomeshwe na wakopeshwe fedha ili wajiendeleze kiuchumi. Nafikiri Mhe. Spika, mimi kama ni Mjumbe wa Kamati hii ya Uwezeshaji ya Wanawake na Watoto na nimetembelea na nimeona tatizo kubwa lililokuwepo ni fedha, ni bajeti ndogo.

Kwa hivyo naiomba serikali iwape bajeti kubwa mama Zainab atuimarishe. Kwa sababu sote hivi sasa, jamii nzima tupo kwa mama Zainab.

Mhe. Spika, kwa machache haya niliyoyatoa naiunga mkono hotuba ya Mhe. Zainab. Namuombea dua, kheri, fanaka, ufanisi, apate bajeti kubwa atuendeleze sisi jamii. Nakushukuru. *(Makofi).*

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia. Kabla sijachangia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii nikawa mzima wa afya.

Mhe. Spika, naomba kuchangia hotuba ya Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto Mhe. Zainab Omar Mohammed kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote kwa kumpa mashirikiano mazuri Mhe. Waziri katika kipindi chao cha kazi. Nimpe pongezi za dhati Mhe. Waziri kwa kusimamia Benki ya Wanawake.

Suala hili la Benki ya Wanawake sio ndio kwanza leo lizungumzwe, Mhe. Waziri na watendaji wake wamejitahidi kadiri ya uwezo wake lakini baada kwenda Wizara ya Fedha kulikuwa na masharti ndio maana hapa Mhe. Waziri kusema kweli ikabidi wafanye mazungumzo na Wizara ya Fedha ndio maana mpaka hii leo ikawa hii Benki haijawa tayari. Lakini kwa jitihada zake Mhe. Waziri huyu akishirikiana na Katibu wake Mkuu na watendaji wake wote wapo tayari kuona Benki ya Wanawake inapatikana Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo pia nimpongeze Waziri na Ofisi yake yote nzima kusimamia wazee mpaka kuona wanapatiwa pencheni ya jamii. Mhe. Spika, Mhe. Waziri kajitahidi sana hapa kusema kweli usiku na mchana mpaka hili suala limefanikiwa si mchezo. Ninawapa hongera sana, tena sana kabisa. Walianza kutoa semina sisi tukiwa kamati na kutoa maelekezo kusema kweli mpaka hii leo tayari Mhe. Rais kabariki suala hili na tayari ikimalizika bajeti wazee wetu hawa

wataanza kupatiwa pencheni ya jamii. Nasema Wizara hii hongera sana tena sana kabisa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, niende Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mhe. Spika, kusema kweli Idara hii pia imejitahidi inafanya kazi zake vizuri, inatoa mafunzo yake vizuri kama ilivyosema bajeti hapa, inasema katika juhudi za kuwezesha wananchi kiuchumi Wizara imeanzisha kituo cha kukuza wajasiriamali Mbweni Unguja, kituo hicho tayari kimeanza kazi kikiwa na jumla ya wajasiriamali 385.

Mhe. Spika, kusema kweli sisi kama kamati sisi kituo tumekwenda kutembelea...

**Mhe. Spika:** Nilikuwa najua kwamba watu wanakwenda kusali lakini ingefaa wakawa wanatoka angalu kwa awamu, vyenginevyo mtaniacha peke yangu hapa kwenye kiti. Sasa tujitahidi tunapotoka kwa ajili ya kwenda kusali basi tutoke angalau kwa awamu tupate kuendelea na shughuli zetu. Mhe. Mwanaidi endelea.

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa:** Mhe. Spika, ni kweli Idara hii inajitahidi kituo hiki kiko Mbweni kama kamati tumekwenda kukiona, ni kweli wanajitahidi sana na wanafunzi hawa wapo na walimu wao wapo wanafundisha kwa makini na pia wanajitahidi kwa kuwapa mafunzo mazuri.

Mhe. Spika, nikiendelea katika Idara hii pia niwapongeze Wizara kwa mashirikiano na chuo kutoka India ambacho kipo Kibokwa nacho chuo hiki tumekwenda kukitembelea. Chuo hiki kipo tayari na kama kinavyojieleza katika kitabu hiki cha bajeti, kinajieleza kwamba kuzindua rasmi mwezi wa Julai, 2015. Kwa hivyo ninawapongeza sana wanajitahidi kwa uwezo wao wote wana mashirikiano mazuri katika Wizara hii.

Mhe. Spika, nikija katika Idara ya Mikopo, katika Idara hii kwa kipindi cha mwaka 2014/2015 Idara ya Mikopo ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo. Hapa walitwambia kwamba wametoa mikopo 1000 yenye thamani ya shilingi milioni mia tano kwa vikundi vya kiuchumi na wajasiriamali mmoja mmoja katika sekta zote za kiuchumi. Lakini huku kwenye utekelezaji wa malengo ya Idara ya Mikopo kwa mwaka 2014/2015 panaonesha wametoa mikopo 531 ambayo inaonesha mikopo hiyo ni shilingi milioni mia nane sabiini na tisa elfu laki tatu na arubaini na mbili (879,342,000), tukilinganisha na hawa huku 1000 pesa zao kidogo, lakini hawa huku waliopewa mikopo kidogo lakini pesa zao nyingi, ilikuwa Mhe. Waziri akija nataka anipe maelezo ili niweze kufahamu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende katika Idara ya Ushirika. Idara ya Ushirika inajitahidi kutoa elimu kwenye vikundi mbali mbali, kwenye *SACCOSS* lakini

Mhe. Spika, bado katika Idara hii wanapofanyia kazi kusema kweli hapakidhi haja. Kama kamati tuliwahi kwenda kutembelea jengo ambalo wamekabidhiwa Idara hii lakini kwenye kitabu hiki cha hotuba sijaona sehemu ambayo inajieleza kwamba jengo hili litafanyiwa ukarabati ili Idara iweze kuhama kule ambapo hapastahiki kufanya kazi kwa sababu kule ikiwa mvua imo ndani, kwa ufupi ofisi haitoshi. Kwa hivyo humu nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje kunipa maelezo ili ile Idara itaanza ukarabati lini na bajeti yake imepangiwa wapi.

Mhe. Spika, nikiendelea Idara ya Ustawi wa Jamii. Kusema kweli Idara hii imefanya kazi vizuri tukianza katika nyumba za wazee zilizokuwepo Sebleni wazee hawa kama wenzangu walivyokuwa wamechangia tayari wanapata mlo wao vizuri mara tatu na posho lao wanapewa kwa wakati. Lakini pia nipongeze kuhusu wazee wetu wa Welezo vile vile Mhe. Spika, Idara hii imefanya kazi vizuri wazee hawa wanashughulikiwa vizuri sana kabisa, yaani wewe mwenyewe ukienda unaridhika, wapo wasafi, wanakula kwa *time*. Tatizo lililokuwepo hapa wafanyakazi waliopo pale hawatoshelezi.

Mhe. Spika, lakini pia nikija katika suala walilozungumza wenzangu wanakamati tulivyokwenda kwenye kamati katika wizara hii Mhe. Waziri baada ya kutueleza malalamiko yaliyokuwepo katika kufuatilia masuala ya wanawake na watoto jinsi wanavyonyanyaswa, alivyokwenda Polisi mwenyewe kusema kweli hii ilitusikitisha sana kabisa. Kwa sababu mpaka inafikia Mhe. Waziri anakwenda Polisi hili ni tatizo.

Mhe. Waziri anaacha kazi ofisini kwa kwenda kusimamia wanawake halafu basi katika hilo eneo alilokwenda Polisi hao Polisi wala hawana habari naye, na kaenda kusimamia wanawake. Hili Mhe. Spika, ni tatizo, mpaka Mhe. Waziri baada ya kuliona hili tatizo anaingia mwenyewe mpaka Polisi. Serikali ninaiomba isimamie vizuri hatua hii huko tunakokwenda sio kuzuri, kila siku wanawake tunapiga kelele unyanyasaji lakini bado hatujakuwa makini kushirikiana na vyombo vya dola kuona hili suala linamalizika.

Mhe. Spika, nikiendelea pamoja na changamoto zilizokuwepo katika Wizara hii naomba Wizara ya Fedha iangalie vizuri katika bajeti yao, kusema kweli bajeti yao hawa ni ndogo na wana kazi nyingi za kufanya. Wanashughulikia mambo mengi ya kijamii yana masuala ya kutoa mikopo lakini bado bajeti yao ndogo. Lakini pamoja na hayo nitoe pongezi nyingi sana kwa *ZAFELA*, wanawake hawa wa *ZAFELA* wanafanya kazi vizuri na wizara hii, wanatoa mashirikiano mazuri katika kusaidia kinamama na watoto.

Mhe. Spika, kuhusu suala la ulipaji wa fidia, Mhe. Waziri anastahiki pongezi pamoja na Katibu Mkuu na Naibu Wake, Makatibu Wakuu na watendaji wao suala

hili wamelisimamia mpaka hivi sasa limeshamalizika na linakwenda kwa utaratibu kila likiendelea hatua zinachukuliwa kwa kulipwa mafao yao kwa hawa waliopata ajali kazini. Kwa vile mimi ni mjumbe katika kamati hii sina maneno mengi isipokuwa niwapongeze sana, sana kabisa Wizara hii ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Baada ya kusema kwa niaba ya wanawake wa Mkoa Mjini Magharibi naunga mkono bajeti hii mia juu ya mia.

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, pia napenda kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uzinduzi wa kampeni ya uzalishaji juu ya wanawake na watoto. Hii inaonesha kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar hapendi vitendo vya udhalilishaji vya wanawake na watoto anachukizwa navyo sana.

Mhe. Spika, pia napenda kutoa pongezi kwa Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu wote wawili, Wakurugenzi na watendaji wote kwa kazi nzuri ambao wameifanya hata wenzangu waheshimiwa Wawakilishi kila anayesimama hapa anampongeza Mhe. Waziri kwa utendaji wake mzuri anatenda.

Mhe. Spika, naomba nichangie katika Idara ya Mikopo, katika kitabu cha Mhe. Waziri ameeleza hapa kuhusu ugawaji wa mikopo. Lakini katika malengo yake ya mwaka 2014/2015 alisema atatoa mikopo 1000 yenye thamani ya milioni mia tano. Lakini katika utekelezaji Mhe. Spika, ameweza kutekeleza mikopo 531 kwa Unguja na Pemba lakini jumla ya fedha ni milioni mia nane sabiini na tisa, mia tatu arubaini na mbili. Kwa hivyo kwenye lengo kuna idadi kubwa ya watu lakini thamani ya pesa ni ndogo, lakini kwenye utekelezaji watu kidogo thamani ya pesa ni kubwa. Sasa sijui kama Mhe. Waziri hizi *figure* zimekosewa au lakini naomba ufafanuzi.

Mhe. Spika, pia nitakwenda kwenye hiyo Idara ya Mikopo lakini suala la urejeshaji wa mikopo. Hapa napenda kuipongeza wizara kwa ufuatiliaji wa mikopo hiyo na imeelezwa hapa, hadi kufikia Mei, 31 jumla ya milioni mia tatu sitini na mbili laki sita elfu na arubaini zimelipwa kwa Unguja na Pemba. Lakini ninachotaka kusema hapa Mhe. Spika, deni ni kubwa kutokana na mikopo ambayo imetolewa kwa watu wahusika, lakini naomba wazidi kufuatilia kwa sababu wengine wanaweza wakajisahau wakaona pengine mikopo hii kama ni sadaka. Lakini sheria za mikopo unafanya shughuli zako na unarudisha ili wengine wapate kufaidika na mikopo hiyo.

Mhe. Spika, nitakwenda katika Idara ya Ustawi wa Jamii, Idara hii na pia hapa nichukue nafasi tena ya kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuwajali wazee wetu kwa kuwapatia pencheni jamii ambao wenye umri wa miaka 70. Hii ni hatua nzuri kwa Serikali yetu, Serikali ambayo inawajali wazee wetu ambao wametumikia nchi hii katika shughuli mbali mbali katika sekta ya afya wengine, sekta ya elimu, sekta mbali mbali wametumikia nchi hii. Kwa hivyo Mhe. Rais kwa ahsante yao kaona kwamba awapatie pencheni jamii ili tuweze kuwasaidia katika hatua zao za mwisho za kuishi kwao. Naipongeza sana na ninamtakia kila la kheri Mwenyezi Mungu amzidishie afya njema na aweze kuendelea na kipindi kijacho panapo majaaliwa.

Mhe. Spika, nitakwenda katika Idara ya Vijana. Mhe. Spika, nitazungumzia kuhusu suala zima la Mfuko huu wa Hifadhi. Vijana ni wengi, ajira ni chache kwa hivyo niiombe wizara kama itawezekana mfuko huu uzidi kuongezwa ili fursa zaidi wapatiwe vijana kwa ajili ya kupatiwa mikopo waweze kujishughulisha shughuli mbali mbali, na hii itasaidia hata kujiingiza katika vitendo viovu ambavyo vinaweza vikawahatarishia maisha yao.

Pia napenda kuipongeza wizara pamoja na Mikoa yote pamoja na Wilaya katika suala zima la mapokezi ya mwenge katika mwaka huu. Mhe. Spika, katika mapokezi ya mwenge hapa katika ukurasa wa 27 imeeleza tarehe 29/04/2015 Mhe. Rais wa Zanzibar alikuwa mgeni rasmi katika mapokezi ya mwenge. Katika ujumbe wa mwenge wa mwaka huu wamesema " *Tumia haki yako ya kidemokrasia, jiandikishe na kupiga kura katika uchaguzi wa mwaka 2015"*. Huu ni ujumbe mzuri Mhe. Spika, na mimi naomba niwashauri wenzangu wajitokeze kweli kupiga kura katika kujiandikisha kwa mwaka huu 2015.

Pia hapa naomba niipongeze Mikoa yote kwa michango mizuri ya mwenge ambayo imepokelewa na wale waliochangia. Kwa sababu Mhe. Spika, michango ya mwenge inayotolewa na wafadhili mbali mbali au watu binafsi michango hii inarudi tena kwa wananchi na inarudi katika shughuli mbali mbali za maendeleo.

Ukiangalia katika Mkoa Mjini wa Magharibi imeshiriki katika hizi mbio za mwenge, jumla ya miradi 24 imechangiwa katika fedha hizi za mwenge na miradi yenyewe ikiwemo Sekta ya Elimu,  Sekta ya Afya, Wajasiriamali, Watu wa *Zapha+, Sober House* na Miradi hiyo 24 katika Mkoa wa Mjini Magharibi jumla ya milioni kama ishirini zimetumika kwa ajili ya miradi hiyo.

Kwa hivyo pesa za mwenge zinaisaidia Serikali kwa shughuli mbali mbali za maendeleo na si kama watu wanavyodhani vyenginevyo, mwenge labda hauna faida yoyote, mwenge una faida kwa sababu pesa zinazokusanywa zinawarudia wananchi wenyewe katika shughuli mbali mbali za maendeleo.

Mhe. Spika, nitakwenda na mimi katika Idara ya Ushirika. Mhe. Mwanaidi alisema hapa suala zima la jengo la Ofisi ya Idara ya Ushirika ambalo linahitaji ukarabati. Na mimi naomba nishauri katika hili wizara ijitahidi kuwawekea mazingira mazuri hawa Idara ya Ushirika ili waweze kufanya kazi zao kwa uadilifu ili waweze kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Nitazungumzia suala zima la mashine hii ya *DNA* wenzangu wamezungumza sana, na wamezungumza kwa sababu matukio haya ya uzalishaji ni mengi, takwimu hapa zimejieleza, watoto ambao wanadhalilishwa, wanaobakwa na ukiangalia ushahidi unapotezwa bure bure hivi, sababu itakuwa pengine ushahidi hauonekani labda pengine kuna sababu mbali mbali. Lakini *DNA* Mhe. Spika, ikiwepo na hasa itawasaidia na wale wengine ambao uwezo wao wa kujieleza ni mdogo. Kwa sababu kipimo hiki kikipimwa ina maana matukio yote yataonekana kuna watu humu wagonjwa wa akili, kuna watu wana ulemavu wa uziwi, lakini *DNA* hii anashindwa kujieleza mtoto pengine ishara atakazozionesha lakini ushahidi hautoshelezi, lakini kuwepo kwa chombo hiki Mhe. Spika, kitasaidia kuleta ule ukweli ndani nani muhalifu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa mimi naiomba tu serikali kupitia wizara hii kwa kweli suala hili walitilie mkazo kabisa kama tulivyotia mkazo kwenye kufuatiliwa meli, na huu ndio uhai wa vijana wetu, kwa sababu watoto wakifanyiwa ukatili kama huu wa kijinsia tunawaharibu mpaka saikolojia yao, hata maisha yao ya baadae inakuwa hayana mwelekeo mzuri.

Mhe. Spika, na suala zima la ajira ya watoto hapa napenda niishukuru wizara suala hili limepungua kiasi kikubwa, na kwa sababu siku za nyuma ilikuwa linavuma sana watoto wadogo wanapita mitaani wanaokota chupa, wanaokota vyuma chakavu kwa biashara mbali mbali, kokoto lakini wizara imejitahidi kwa suala hili hata hivi sasa linapungua kidogo kidogo.

Pia naomba wasiridhike na hali hiyo, wajitahidi kwa sababu hawa ni watoto wetu wanataka wajengewe *future* nzuri baadae hawa watakuja kuwa walimu wazuri. Watakuja kuwa madaktari wazuri, kwa hiyo naomba wasiridhike na mabadiliko hayo lakini waendelee na jitihada hizi ili watokomeze kabisa suala hili zima la ajira kwa watoto.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba tu nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada zake kubwa, utendaji wake wa kazi kwa kuleta maendeleo katika nchi hii pamoja na watendaji wake wote, na nawatakia kila la kheri na naunga mkono asilimia mia moja hotuba hii. (*Makofi*)

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi kidogo ya kuweza kuchangia mawili matatu katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto Mhe. Zainab Omar Mohammed.

Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa utendaji wake mahiri kabisa, na kwa kweli Mhe. Waziri ni mmoja kati ya mawaziri ambao wamekuwa wakifanya kazi kwa uadilifu, kwa ushirikiano mkubwa na haya ninayoyasema kwa uhakika kwa sababu mimi nimewahi kuwa Mjumbe wa Kamati hii katika kipindi kile cha miaka miwili na nusu cha kwanza.

Kwa hivyo, namfahamu vizuri sana Mhe. Zainab. Mhe. Spika, lakini mbali na yeye vile vile Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake ni watu wazuri wanastahili kupewa pongezi.

Mhe. Spika, kwa kweli nichukue fursa hii pia kumpongeza Mhe. Haroun kwa sababu yeye ni waziri mwenza, na amekuwa akitoa ushirikiano mkubwa sana katika wizara hii na hasa suala zima la uwezeshaji, na ukizingatia kwamba yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uwezeshaji.

Kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kumuwezesha na kumsaidia Mhe. Waziri katika kuendeleza na kuimarisha masuala mazima ya uwezeshaji ya wananchi.

Yote haya Mhe. Spika, ni kazi nzuri ambayo anaifanya Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein, kazi ambayo kwa kweli aliyoifanya katika kipindi hiki cha miaka mitano ni kazi nzuri, na kwa kweli sote tumeridhika na utendaji wake, na tuna imani kubwa kwamba katika kipindi kinachokuja ataendeleza yote ambayo ameyaanzisha na yale ambayo yanastahiki kuanzishwa.

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Uendeshaji na Uratibu wa Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mheshimiwa niipongeze sana wizara katika kuandaa mafunzo ya ujasiriamali katika maeneo tofauti ya vijana wanaohitimu hususan katika vijana waliosoma vyuo vikuu.

Mheshimiwa hili ni jambo zuri sana hasa ukizingatia kwamba vijana wetu ambao huwa wanamaliza vyuo vikuu huwa hawana ajira, hivyo wanastahiki kusaidiwa ili kuweza kujiendeleza katika maisha yao.

Mhe. Spika, juzi wakati nikiangalia televisheni ya *TBC* nilipata fursa ya kuangalia kipindi kimoja ambacho vijana wa Vyuo Vikuu vya Tanzania Bara

wamewezeshwa na kuweza kujiajiri katika masuala ya kilimo. Sasa niiombe wizara kufanya kazi ya ziada ili kuwawezesha vijana wetu na hasa kupata mafunzo katika vijana wale ambao nimeona katika mikoa mbali mbali Tanzania Bara ambao wameweza kujiajiri kwa kupitia masuala haya ya mikopo.

Kwa hivyo, nichukue fursa hii kuiomba wizara ili kuweza kuwezesha vijana wetu ambao wanamaliza katika vyuo vikuu vyetu hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, pia vijana wetu ambao huwa wanajishughulisha katika masuala ya biashara ndogo ndogo. Mheshimiwa kwa kweli vijana wetu wanastahili kupewa msukumo na uwezeshaji katika kujiendeleza na biashara ndogo ndogo ambazo wanazianzisha katika kujikwamua na maisha yao. Kwa hiyo, niiombe wizara kuwasaidia vijana katika masuala haya ya kuwawezesha kuendeleza na biashara ndogo ndogo ili waweze kujisaidia katika maisha yao.

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Ushirika. Mheshimiwa mashirikiano kwa kweli ambayo yanahitajika katika kujiendeleza vijana au wananchi ambao wanashiriki katika masuala mbali mbali ya ushirika. Kwa kweli ipo haja kuweza kusaidia vikundi mbali mbali ili kuweza kujiendeleza, kwa sababu wananchi wengi huwa wanajikusanya kwa pamoja ili kuweza kujisaidia na kuendeleza mambo mbali mbali ya kiuchumi yakiwemo masuala ya kilimo, masuala ya ufugaji na masuala ya wale vijana ambao huwa wanachonga chonga, na masuala mengine mbali mbali.

Kwa hivyo, nimefurahi sana kuona kwamba wizara inafanya bidii kubwa katika kuvisaidia vikundi hivi vya ushirika ili kujiendeleza katika kazi zao mbali mbali.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije katika suala zima la kuwasaidia wazee katika hifadhi. Mimi kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana na kumshukuru sana Rais Dkt. Ali Mohammed Shein katika kuwawezesha wazee na kuweza kuimarisha zaidi huduma za wazee na hasa katika lile suala zima la kuwawezesha wazee wale ambao wamezidi miaka 70.

Mhe. Spika, wazee wetu ambao wamelikomboa Taifa hili na kuiletea sifa kubwa sana nchi yetu ambao sasa hivi wamekuwa hawana uwezo wa kujiendesha maisha yao, hivyo wanahitaji kupewa huduma ya ziada na kuwawezesha zaidi. Lakini tendo ambalo amelichukua Mhe. Rais ni tendo la kupigiwa mfano na kupewa pongezi kubwa sana.

Mimi kwa kweli kila unapopita mitaani Mhe. Spika pongezi kubwa amekuwa akipewa Mhe. Rais na haya yote ni katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu wazee wetu hawa ambao leo huko nyuma walikuwa ni

wafanyakazi ambao wametulea sisi mpaka tumefika umri huu, wamefanya kazi kubwa sana kuliendeleza Taifa letu kiuchumi, kibiashara na mambo mbali mbali.

Kwa hivyo, kuona kwamba Mhe. Waziri amewaangalia na kuwawezesha wazee wetu hawa, kwa kweli ni faraja kubwa sana, kwa sababu Mhe. Spika, mimi nina imani Mwenyezi Mungu atujaalie sote tutafika katika umri wa wazee, ingawa wewe tayari unaunyemelea nyemelea Mhe. Spika lakini uzee huu basi utapata faida na baraka za Mhe. Rais.

Kwa hivyo, usijali Mhe. Spika ni wajibu wetu kumpongeza Mhe. Rais na sote ambao tunaounyemelea uzee huo Mhe. Haroun pale najua na yeye katika wanaounyemelea nyemelea. Kwa hivyo, ni wajibu wetu sote kuangalia na kumpongeza Mhe. Rais kwa juhudi zake ambazo amechukua kwa wazee wetu.

Mhe. Spika, kwa kweli nije katika masuala ya vijana. Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amefanya mambo makubwa sana katika kuwasaidia vijana. Na nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na wizara yake kwa ujumla kwa kazi kubwa wanayoifanya kuwasaidia vijana. Wamefanya mambo makubwa kuwasaidia vijana katika mambo mbali mbali na haya yote ni matunda ambayo yanatokana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu Chama cha Mapinduzi ilani yake inaelekeza kuwaimarisha na kuwaendeleza vijana.

Kwa hivyo, haya yote ambayo yanafanyika ni matunda makubwa ambayo yanatokana na ilani hiyo na utekelezaji wake ambao unatokana na Mhe. Rais katika kuelekeza mawaziri wake, ili kuweza kuwasaidia vijana wetu hawa ambao kwa kweli ndio Taifa la kesho. Kwa hivyo, niipongeze sana Serikali hii ya SMZ katika kuwasaidia vijana kwa kujikwamua na mambo mbali mbali.

Mhe. Spika, lakini vijana wetu ambao leo hii wale ambao wamemaliza masomo katika vyuo mbali mbali, wamemaliza masomo katika skuli mbali mbali wanahitaji kuwezeshwa katika nyanja mbali mbali zikiwemo za uvuvi, za uwezeshaji katika masuala mbali mbali. Na nimshukuru sana kwa sababu Mhe. Haroun Ali Suleiman amefanya kazi kubwa wakati wizara hii ilipokuwa mikononi mwake. Na nina imani kubwa kwamba atamsaidia sana Mhe. Waziri ili kuwawezesha vijana na hili linatokana na kazi kubwa ya Mhe. Rais ambayo ameifanya katika kuwasaidia vijana wetu.

Kwa hivyo, nina imani ili wizara hii ifanye kazi ya ziada, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha yale ambayo yanazungumzwa kuwezesha wizara hii basi aipe kipaumbele ili kuweza kufanikisha kazi ambazo zinaweza kusaidia vijana wetu kujikwamua kimaisha, kujikwamua katika kujiendeleza kiuchumi katika maisha yao.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilikuwa sina mengi kwa sababu nimechupia nilikuwa sijajipanga, lakini nimechukua fursa hii kuchangia kidogo ili na mimi niweze kuchangia wizara hii ambayo inasimamiwa na Mhe. Zainab Omar.

Baada ya machache hayo naiunga mkono asilimia mia moja hotuba hii. Mheshimiwa nakushukuru sana.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Mhe. Spika, na mimi awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kutujaalia kuwepo jioni hii katika kutekeleza majukumu yetu ya kuisimamia serikali pamoja na kuwasemea wananchi wetu kwa niaba yao.

La pili nikushukuru kunipa nafasi hii angalau na mimi kwa muhtasari nitoe mchango wangu katika hotuba ya Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri ambao ulitupa ufafanuzi wa kutosha katika kukipitia kitabu hiki.

Mhe. Spika, kiujumla wake niwapongeze watendaji wote wa Wizara ya Uwezeshaji kwa umahiri wao, mashirikiano yao na juhudi zao katika kuendeleza jukumu zima ambalo wamepewa na Taifa hili, jukumu ambalo ni kubwa kwa sababu wana jukumu la ustawi wa jamii, vijana, wanawake na watoto. Ina maana kwamba wizara hii imebeba majukumu mengi ya kuwastawisha watu na makundi mbali mbali katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Kwa hivyo, nasema kwamba nawapongeza sana watendaji kwa mashirikiano yao katika kuwawezesha watu wa makundi haya ambayo nimeyataja hapa.

Mhe. Spika, mimi nianze na mchango wangu katika ukurasa wa 15, hizi nambari hazisomeki vyema kiasi fulani kwa sababu zimekozeshwa rangi ambayo haionekani kwa upeo. Lakini hii nahisi ni ukurasa wa 15, ukurasa huu nataka nisome utekelezaji wa malengo ya Idara ya Uwezeshaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka 2014/2015. Mimi niende katika kifungu cha 33 hapa naomba ninukuu.

“Mhe. Spika, utekelezaji wa malengo kwa Idara hii ulikuwa kama ifuatavyo:-

- Jumla ya vijana 71 (Unguja 50 na Pemba 21) walipatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kujiajiri katika shughuli za ujasiriamali”.

Mhe. Spika, hili ni lengo zuri lakini ukilinganisha na idadi ya vijana ambao tunao katika visiwa hivi vya Unguja na Pemba naona kwamba idadi ya vijana 71 ni idadi ndogo sana, ni idadi ndogo, na kwa kweli nimuombe Mhe. Waziri suala hili

aliangalie kwa kina hasa katika kipindi kijacho. Kwa sababu wajasiriamali kwa kweli ni watu muhimu sana, na vijana hasa ndio wanaotaka wawezeshwe kwa sababu wana nguvu, wana uwezo wa kutembea hapa na pale, wana uwezo wa kufanya kazi mbali mbali.

Kwa hivyo, idadi ya vijana 71 kwa Unguja na Pemba ni idadi ndogo, kwa kweli inahitaji iwepo idadi kubwa ambayo itawawezesha vijana kupata taaluma ya ujasiriamali.

Mhe. Spika, niende katika nukta ya tatu inasema kwamba, jumla ya wajasiriamali wadogo wadogo 38, kati yao 32 wanawake na 6 wanaume, wamewezeshwa kushiriki katika maonesho ya JUAKALI yaliyofanyika nchini Rwanda.

Mhe. Spika, hili ni jambo zuri, ni jambo zuri kwa nini? Kwa sababu vijana kutembea kwenda katika sehemu nyengine ya ujasiriamali wanapata kujifunza, na pia wanapata kuiga yale mazuri ambayo yamefanywa na wenzao ili na wao waje kuyafanya hapa kwao, au kwa njia nyengine pia vijana hawa wanaweza kuigwa na wenzao wa nchi nyengine yale mazuri ambayo wanayafanya hapa ili kurithi nchi nyengine ambayo wamekutana na vijana hawa.

Mhe. Spika, suala hili la vijana kwenda katika maonesho ni jambo zuri na naiomba wizara suala hili kila ikifika kipindi cha maonesho katika nchi tofauti wawapeleke vijana wetu ili kupata taaluma ya kuweza kujiajiri, kwa sababu kama tunavyosema kwamba ajira si ya serikali tu, kujiajiri vijana katika ujasiriamali, kujiajiri vijana katika shughuli zao mbali mbali ni jambo zuri ambalo litawakomboa katika kupambana na maisha magumu ambayo yapo.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu katika ukurasa wa 16 nukta ya pili. Katika juhudi za kuwawezesha wananchi kiuchumi, wizara imeanzisha Kituo cha Kukuza Wajasiriamali Mbweni, Unguja. Kituo hicho tayari kimeanza kazi kikiwa na jumla ya wajasiriamali 385. Ni jambo zuri kwa sababu hapa watatoka vijana wakiwa na ujuzi wa kile ambacho wanajifunza, na hapa inaonesha kwamba watapata maelekezo, watapata uzoefu ili waweze kufanya majukumu yao kwa ufanisi wa hali ya juu, lakini nilikuwa na swali nimuulize Mhe. Waziri kituo hiki kiko Mbweni Unguja sijui ana mpango gani wa kisiwa cha Pemba kuanzisha kituo hiki cha taaluma ya wajasiriamali.

Je, wapo hawajaingizwa hapa tu au hawajaanzishwa, kama hakijaanzishwa kituo cha kukuza wajasiriamali pale kisiwani Pemba, namuomba Mhe.Waziri alipe kipaumbele kwa sababu pale Pemba wapo wajasiriamali wengi ambao pia nao wanahitaji taaluma hii ya kuweza kufanya shughuli zao kwa ufanisi.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 17 nukta ya kwanza inasema kwamba "Wizara kwa mashirikiano na Chuo cha Barefoot kilichopo Tilonia nchini India, imekamilisha ukarabati wa jengo kwa ajili ya uanzishwaji wa kituo cha kuwafunza wanawake utengenezaji wa vifaa vya umeme wa jua. Kituo hicho kilichopo Kibokwa Mkoa wa Kaskazini Unguja kinatarajiwa kuzinduliwa rasmi mwezi wa Julai, 2015".

Mhe. Spika, hili ni jambo zuri, nasema kwamba wizara kuanzisha chuo hiki kwa ajili ya wanawake kujifunza masuala ya umeme wa jua ni jambo zuri, lakini hapa niseme tu kwamba, kituo hiki kitakuwa na wanawake wangapi kwa wakati mmoja? hiyo (a).

(b) mafunzo haya yatachukua kwa muda wa siku ngapi, miezi mingapi au miaka mingapi.

(c) je, kituo hiki kilichoko Kibokwa watu wa Micheweni, Chambani, Mkoani, watafaidika vipi kujiunga na chuo hiki?

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu kwa sababu na mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati hii ya Uwezeshaji, sitaki nizungumze kwa urefu sana natia tia nyalio tu ili kukuza na mimi katika *hansard* masuala haya, niende katika ukurasa wa 25. Mheshimiwa naomba kunukuu kifungu cha 57.

Kifungu cha 57 kinasema kwamba:

"Mhe. Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto itaanza kutoa pencheni jamii kwa wazee wote wenye umri wa kuanzia miaka 70 Unguja na Pemba. Hatua hii inachangia juhudi za serikali katika mpango wake wa kupunguza umasikini kwa wananchi wa Zanzibar".

Mhe. Spika, dhana hii kwa serikali ni dhana nzuri sana, ni dhana ya kupigiwa mfano ikitekelezwa. Naomba kwa sababu wazee wanatusikia, wazee wa miaka 70 wapo wanasikiliza taarifa hii na tumesema kwamba mwaka 2015/2016 ina maana ni bajeti inayokuja, nimuulize Mhe. Waziri amejipanga vipi kuwatambua wazee kiuhalisia Wazanzibari, wazee hawa amejipanga vipi kuwatambua na vipi watapewa haki hii bila ya upendeleo.

Wazee wengi katika miaka iliyopita wazee wa miaka 70 wengi wao hawana vyeti vya kuzaliwa, pencheni hii isijekuwa na vikwazo vikubwa kwao itakuja kuwa ile dhana na dhamira ya wizara baada ya kuwa njema inaweza kuwa mbaya.

Mhe. Spika, naomba ieleweke kwamba, tukitaja wazee tusifikirie tu wazee tuwaangalie ujana wao walikuwa vipi, wazee hawa ndio waliotufikisha sisi hapa. Uchumi wa Zanzibar tunaoringia hivi sasa basi asasi yake, misingi yake inatokana wazee hawa. Kwa sababu wazee hawa Mhe. Spika, ndio waliopanda mikarafuu ambalo ndio zao kubwa la uchumi la Zanzibar kwa miaka mingi, ndio waliopanda minazi. Minazi ambayo na karafuu kwetu sisi Zanzibar ndio nafuu, wazee hawa ndio waliojenga majumba ambayo tunaishi sisi watoto wao, wazee hawa ndio waliokuwa wachukuzi katika mabandari yetu kutulea sisi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hawa kuwapa pencheni ni haki yao, wao ndio walioikuza Zanzibar hii mpaka ikafikia leo kuwepo hapa. Kwa hivyo, Mheshimiwa dhana ya kuwapa posho au pencheni wazee wa Kizanzibari ni dhana nzuri, ni dhana ya kupigiwa mfano.

Naomba suala hili lipewe umakini wa aina yake tusiwachukulie tu kwamba wazee, hapana, sio wazee tu, historia yao katika kuleta uchumi na kuipamba nchi hii ni wao. Tulikuwa na vyanzo vingi na mambo mengi ya kimaendeleo na tunaendelea kuwa nayo wameyaanzisha wao kwa nguvu zao, kwa jembe na panga na shoka walizokuwa wakizitumia kwa ajili ya kuilea Zanzibar yetu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri mimi, wewe na mwengine yeyote aliyemo katika Baraza, aliyeko nje ya Baraza anafaidika kwa nguvu za wazee waliotangulia. Kwa hivyo, hawa hatuwapi pencheni kama tu ni masihara tunawapa pencheni kama ni haki yao.

Kwa hivyo, umri wa miaka 70 tumeanzia lakini pendekezo langu tutakapofikia na utaratibu mzuri huko mbele basi tupunguze kutoka 70 mpaka miaka 60 au 65. Kwa sababu kutokana na wakati wetu wa leo mzee wa miaka 60 kuanzia sasa huyo taabani, kwa sababu maisha si rafiki. Kwa hiyo, tuanze miaka 70 kwa sababu tunajifunza lakini tutakapofikia hatua za miaka ya mbele kidogo basi tuanze na wazee wa miaka 60 au 65.

Mhe. Spika, kwa kweli suala hili ni suala mama, ni suala ambalo tutapata fadhila na faida kubwa kwa serikali yetu tutakapolikamilisha hili.

Mhe. Spika, jengine nitakalolizungumza ni kuhusiana na suala zima la jengo la ofisi ya wizara Pemba. Wizara hii Pemba haina jengo, kuna jengo la kukodiwa kila mwaka, jengo ambalo pia halikidhi haja hata kukiwa na mikutano au na baadhi ya mambo utakwenda kuwakuta wafanyakazi pamoja na watendaji wao wengine wamepanga viti katika maeneo ya kujibana sana kwa kweli.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kwa hali yoyote atueleze mpango gani waliojipanga katika kuimarisha jengo la ofisi ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto pale Pemba.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika suala zima la udhalilishaji wa kijinsia na ukatili wa wanawake na watoto. Mhe. Spika, suala hili ni baya na ni baya sana halifai, na litaendelea kuwa halifai.

Suala hili kila kipindi cha bajeti tunalipigia kelele kwamba ukatili unaendelea, unyanyasaji unaendelea. Sasa umefika wakati serikali ikiwa kuna sheria ambazo zinakwaza zibadilishwe, zirekebishwe ili sheria hizi ziendane na wakati; wale wote ambao wanakamatwa na hatia za udhalilishaji, wale wote ambao wanakamatwa na hatia za ukatili basi sheria iwakamate na iwatie hatiani. Kesi kwenda danadana, ushahidi haujapatikana, ushahidi haujakamilika, aliyekamatwa ni bubu, aliyekamatwa hasemi, hauna ushahidi kamilifu.

Sheria vyovyote iwavyo iwekewe mazingira ambayo kila mwenye kosa akamatwe kwa mujibu wa kosa lake, ushahidi uwekwe katika mazingira ambayo kila aliyetendwa tendo la ukatili au kudhalilishwa kwa hali yoyote aliyo kama mlemavu wa kiungo, mlemavu wa aina yoyote basi kuwe na sheria ambayo itamlinda, akikamatwa mdhalilishaji kwa sheria itakayomlinda mlemavu au mwengine basi iwe inampa ruhusa au inatoa fursa ya kutoa ushahidi ambao utamtia hatiani huyu muhusika.

Mhe. Spika, kwa kweli nishukuru sana, nishukuru kunipatia nafasi hii angalau na mimi kutoa mchango wangu mchache. Mwisho kabisa niseme kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chambani. Mheshimiwa nakushukuru sana.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe binafsi, lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa ujumla kwa hotuba yake nzuri, mwanana, ambayo leo wamekuja kutuwasilishia hapa.

Pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa namna ya ufundi alioutumia wa aina yake leo katika kuiwasilisha hotuba hii. Namshukuru sana Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nikimaliza hapo vile vile nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa upande wa ule Mfuko wa Uwezeshaji, kwa namna ambavyo anauendeleza vizuri na hatimaye hata na sisi katika maeneo yetu kwa mfano katika Jimbo letu la Kikwajuni tukaweza kupata watu na angalau karibu mia wamewezeshwa katika Mfuko ule. Kwa taarifa ambayo Mhe. Waziri ameniambia

ni kwamba hata yale marejesho yanakwenda vizuri, ni jambo la kutia moyo na wengine ili waweze kupata.

Nikimalizia hapo mimi leo mchango wangu sio mkubwa sana, isipokuwa nakwenda moja kwa moja katika Idara hii ya kuwawezesha vijana. Mhe. Spika, naomba uniruhusu ninukuu kitabu cha bajeti cha mwaka 2010/2011.

"Mhe. Spika, katika eneo ambalo linawahusu vijana kwa mwaka huu 2010/2011 idara hii ilikusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuendelea na hatua ya uundaji wa Baraza la Vijana Zanzibar
2. Kuratibu na kusimamia mbio za mwenge
3. Kuendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano kwa taasisi za vijana ndani na nje ya nchi pamoja na kuendeleza kambi kazi za vijana kwa upande wa Zanzibar
4. Kuendeleza na kuimarisha vikundi vya vijana vya uzalishaji mali kwa kutoa mafunzo ya uanzishaji na uendelezaji wa *SACCOS* na ujasiriamali, uongozi na utunzaji wa mahesabu na mambo mengine; yako mengi sana".

Mhe. Spika, nikiacha kitabu hiki nakuja katika kitabu cha mwaka 2012/2013, sekta hiyo hiyo ya vijana.

Mhe. Spika, hapa kuna malengo yanayofanana na yale, lakini tunaanza na kwamba:

"Kukuza uwezo wa kiutendaji wa Idara, kukamilisha uundaji wa Baraza la Vijana, kuratibu mbio za mwenge, kuendeleza na kuimarisha vikundi vya vijana, uzalishaji mali, kwa kutoa mafunzo na uanzishaji na uendelezaji wa *SACCOS*, ujasiriamali, uongozi na utunzaji wa mahesabu, kutayarisha mipango ya maendeleo ya vijana, kufanya mapitio ya sera ya maendeleo ya vijana, kujenga uwezo wa vijana kupitia stadi za maisha, vita dhidi ya UKIMWI na madawa ya kulevya, kuendeleza ushirikiano na uhusiano wa taasisi za vijana ndani na nje ya nchi".

Mhe. Spika, naomba unistahamilie, nakuja mwaka 2013/2014.

"Katika mwaka 2013/2014 kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana, kuratibu mpango wa mipango kwa vijana na kuhamasisha kujiunga na vyama vya ushirika na mikopo, kuratibu mbio za mwenge, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa mpango wa stadi za maisha kwa vijana walio wengi, kuratibu uanzishwaji wa Baraza la Vijana, kuimarisha ushirikiano na uhusiano na taasisi za vijana ndani na nje".

Mhe. Spika, nakuja mwaka 2014/2015.

"Kuratibu uanzishwaji wa Baraza la Vijana, kuratibu mpango wa mikopo kwa vijana na kuhamasisha kujiunga na vyama vya ushirika na mikopo, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa mpango wa elimu ya stadi za maisha kwa vijana walio nje ya skuli, kuratibu mbio za mwenge, kufanya uratibu, ufuatiliaji na uhamasishaji wa vikundi vya vijana, uimarishaji mashirikiano ya uhusiano na taasisi za vijana ndani na nje ya nchi na mambo mengine yanayoendelea".

Sasa namalizia kwa mwaka 2015/2016.

"Kuratibu uendelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana, kuratibu na kufuatilia uanzishwaji wa Baraza la Vijana, kuratibu mbio za mwenge, kuhamasisha kuandaa na kuwaunganisha vijana na fursa mbali mbali za kiuchumi zilizopo, kuratibu utekelezaji wa kitini na muongozo wa stadi za maisha kwa vijana walio nje ya skuli, kufanya ufuatiliaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii za vijana na kuimarisha ushirikiano na taasisi zinazoshughulikia masuala ya vijana ndani na nje ya nchi".

Mhe. Spika, hapa hatujawasaidia vijana.Jjioni hii nilikuwa na vijana kulikuwa kuna michezo yao nimekwenda kufungua, katika michezo ile nikabahatika kukaa na vijana. Vijana wana malalamiko yao, nashukuru serikali imewasomesha na wamefahamu, wameelekezwa wameelewa, lakini wanachotaka kukijua vijana sasa hivi pale wanapomaliza masomo yao serikali imewapangia utaratibu gani wa kuweza kujijua namna gani wataweza kuondoka katika hatua waliyonayo, ili kuweza kujiendesha kimaisha kwa mustakabali wa kujitengenezea maisha yao.

Nimefurahi sana kuona kwamba vijana wameweza kufikia kutamka bayana kwamba hatuna lazima ya kuajiriwa katika serikali, tunaelewa uwezo wa serikali yetu, lakini kuna taratibu ambazo tunaelekezwa namna gani ya kuweza kujiajiri sisi wenyewe.

Mhe. Spika, lakini wakiangalia wanapofuatilia taratibu hizi haziko bayana wakaweza kuzielewa na wao wakaweza kufahamu ni namna gani wanaweza kujiendesha na kujitatua katika matatizo ya kujiendesha kimaisha.

Naomba sana wizara inayohusika na vijana watengeneze utaratibu badala ya utaratibu huu wa mipango ambayo inataka wao iwe kila siku tutaanzisha tu, tutafanya tu. Sasa tunataka kuona ni namna gani wameweza kufanya na vijana wakaweza kuneemeka kuweza kujiona kwamba wanaondokana na wimbi la kukosa kazi na kukaa katika vijiwe, na hatimaye wakaweza kupata kazi za

kujifanyia hata katika njia ya ujasiriamali kama ambavyo Mhe. Waziri amekwisha kutueleza humu.

Tatizo la vijana wanataka kufahamishwa ni namna gani ya kuweza kuziona na kuzipata hizo nafasi ambazo zimetamkwa na wao waweze kufaidika nazo. Wengi wao wanalalamika wanasema kwamba hawajui waanzie wapi. Naomba sana kwa sababu Mhe. Waziri wizara yake ndio yenye majukumu haya, na ndio wizara yenye mamlaka haya, naomba sana vijana wapewe taaluma nini wafanye ili waweze kuondokana na wimbi hili la kuhangaika kwa ajili ya kutafuta maisha yao na mustakabali wao wa kujiendeleza kimaisha.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa najua salamu zimekwishakufahamika hizo sina haja ya kwenda ndani sana nije katika utaratibu wa kuwaenzi wazee.

Wenzangu wengi wamezungumza hapa na wengi wameunga mkono, lakini na mimi ningeliomba na sisi kama viongozi wa Baraza hili la Wawakilishi tukiwa ni Wawakilishi wa wananchi, tutengenezeni basi utaratibu na sisi wa kuwatembelea wale wazee, tusiiachie serikali tu peke yake kufanya mambo yote na kupanga mambo yote, na sisi tuunde utaratibu wa kuweza kuwatembelea wazee wetu wale, kwani tutakapokwenda kule kuwatembelea wanazidi kupata faraja kuona kwamba na wao wamekumbukwa. Hawana shida ya kitu kutoka kwetu, wanachokiomba ni ujio wetu tu, twende pale na tuweze kuonana nao, wao katika mioyo yao watakuwa wamefarijika na wamefurahika, na wataona kwamba kweli na viongozi wengine wanawajali badala ya kuwaachia viongozi wakuu tu, kwa kwenda kila siku kuangalia na kwenda kujua matatizo yao kuwatatulia.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nimalizie sasa kwa suala zima la udhalilishaji. Wengi wamekwishazungumza katika suala hili. Mimi kwa upande wangu ningeliomba sasa, kwanza nawashukuru Idara ya Mahakama kwa kazi nzuri ambayo kwa kipindi hichi wamekuwa wakifanya katika kufikia mustakbali mzuri wa kuziendesha zile kesi za udhalilishaji na hatimaye zikaweza kuwa angalau tunapata moyo kwa namna ambavyo wanavyozishughulikia kesi zile. Nawafurahia sana watu wa Idara ya Mahakama.

Lakini pia tufike pahala sasa Mhe. Spika, wale ambao wanapambana na kadhia zile kama tulivyokuwa tukiwatangaza wahalifu zamani, turejeshe utaratibu ule ili wale watakaokuwa wanatajwa na wakatolewa katika vyombo vya habari sasa watakuwa wanaona na kuona haya na kushinda kufanya mambo ambayo yanalitia aibu Taifa letu.

Mhe. Spika, juzi nilipokuwa nachangia hapa katika Afisi ya Rais nilisema kwamba mimi nakuwa nasononeshwa sana kuona kwamba maisha yote kuna Jumuiya

zinakuwa zinaanzishwa zikiwemo Jumuiya za kina mama, mambo mengine chungu nzima kima mama kupewa sifa na kila kitu mbona sisi kina baba hatupewi sifa. Sasa lakini niliangalia na nikaenda ndani zaidi nikagundua kwamba moja kati ya kero na kadhia ambayo akina baba sisi tunafanya miongoni mwetu ni hili suala la kwenda kuwaharibu watoto wadogo ambao bado hawawezi kukidhi haja ya yule mzee ambaye anakwenda kumfuata mtoto ule.

Mhe. Spika, pamoja na kulilaani suala hili kwa nguvu zote nimefarijika sana katika Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kuona kwamba kuna muelekeo wa kuweza kupatika *DNA* kwa maelezo ambayo Mhe. Waziri alikuja kuyatoa hapa. Tunaiomba sana serikali *DNA* ije haraka, najua serikali hii ni sikivu na najua inatekeleza mambo inaposema. Sasa ile *DNA* iletwe haraka na hatimaye sasa tuweze kuona tunawashughulikia watu hawa ambao wanalitia aibu taifa letu na hususan kina baba ambao miongoni mwetu tunao utaratibu huu wa kuharibu watoto wengine ambao tumewazaa wenyewe.

Jambo la aibu, jambo la fedheha, jambo lisilopaswa kufanywa na mtu mzima ambaye kuna watu chungu nzima wanaweza kuendelea na shughuli zake, akawaacha, matokezeo yake akaenda kufuata vitoto vidogo na kuvidhalilisha na kuvifanyia mambo ambayo hayaelekei. Namshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na timu yake ya watendaji kwa shughuli hii namna walivyokuwa wameishughulikia na hatimaye serikali kuu ikasikia na mpaka sasa tukaweza kuona juhudi za kupatikanwa kwa *DNA* zipo katika hatua za mwisho.

Baada ya hapo Mhe. Spika, kwa vile wengi wamekwishasema mengi, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. Namuomba lakini Mhe. Waziri azingatie yale ambayo nimemwambia. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ninazo dakika ishirini zinataka kuchangiwa Mhe, Jaku Hashim Ayoub.

**Mhe, Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, mimi nafikiri nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Magharibi hii, na *hardly* nitatumia kama dakika tano tu. Mimi nilikuwa sitaki hata kuchangia hii. Lakini kuna mambo kidogo yamenisikitisha, na unapoona pana mashaka una haki ya kuchangia kutia mkono wako, mdomo wako au kulikimbia.

Nichukue fursa hii kumshukuru Waziri na watendaji wake kwa majukumu yao ya kikazi na niwape pole vile vile. Baada ya hapo nije katika kitabu hichi kifungu cha 52. Mhe. Spika, naomba nikinukuu:-

"Jumla ya malalamiko 132; Unguja 50 Pemba 82 ya watoto waliofanyiwa ukatili na udhalilishaji yaliripotiwa katika kitengo cha hifadhi ya mtoto cha Idara ya Ustawi wa Jamii. Kati ya hayo malalamiko 80 yanahusu kubakwa, 14 kulawitiwa,15 kukashifiwa na 23 kutoroshwa. Walalamikaji walisaidiwa kuwasilisha malalamiko yao katika vyombo vya sheria".

Mhe. Spika, hapa pana masikitiko makubwa wizara ilikuwa ieleze wazi kabisa bila ya kuficha mbali na taarifa sahihi walihukumiwa wangapi kesi zimekwenda ngapi, utaratibu gani umetumika hili ndio tunalipigia kelele siku hadi siku. Lakini kuja kutuletea hivi tu leo tunapitisha bajeti hii, wananchi wanasikiliza nini kilichofanyika. Ni kitu cha kusikitisha hapana taarifa sahihi haya ni maandishi tu au sijui ndio bajeti yetu ya mwisho tena. Lakini kwa hapa wizara ieleze wangapi wamekamatwa, hatua zimechukuliwa vipi, wangapi wamefikishwa mahakamani, wangapi kesi zao zimeachiwa huru na wangapi wamepewa dhamana. Hichi kitendo tutaendelea kupiga kelele siku hadi makelele hivi. Mhe. Waziri kidogo ulikuwa uweke taarifa sahihi kabisa.

Nikitoka hapo Mhe. Spika, nije 53:

"Wizara imepokea na kushughulikia malalamiko 140; 95 Unguja na 45 Pemba yanayohusu malezi ya watoto kati ya 92 ni ya matunzo na 48 ni mvutano wa malezi. Wimbi hili kubwa la utelekezwaji wa watoto linasababishwa kuvunjika kwa ndoa na pia tabia ya baadhi ya akina mama".

Hii wizara baada ya haya hatua gani, hukumu gani ilikuja baada ya malalamiko haya kufika kwao Afisini au tumeandika kama wizara inayohusika na masuala haya imechukua hatua gani, nini mafanikio ya watu hawa. Kama wizara ilikuwa ieleze usimamizi wake na maelezo hatua zilizofikia, mafanikio ilikuwa ieleze, kitu kama hicho Mhe. Spika.

Baada ya hapo nije hapo hapo 54:-

"Wizara imefanya zoezi la kuvitambua vituo vya kulelea watoto na kusimamia utekelezaji wao. Jumla wa vituo 11 Unguja na 8 Pemba vitatu vimetambuliwa (Angalia kiambatanisho 5")

Nini kilichofanyika, nini kimewasaidia watoto yatima, vimetambuliwa tu kama vipo, msaada gani serikali imetoa, Kwa kuchambua tu moja, mbili, tatu na nne nini ilichokisaidia, umekwenda tu kuvitambua? Ilikuwa aeleze kipi kilichosaidia, kipi kilichofanyika.

Nije namba 55

"Wizara imeendelea kuhudumia nyumba za kulelea watoto Mazizini".

Kwanza hapa nichukue hatua za dhati kabisa kumshukuru mke wa Rais mstaafu mama Shadya Karume kuwa nyumba aliyojenga ya kisasa na ya kileo kule Chuo cha kulelea Watoto Mazizini tafauti na nyumba ilivyokuwa Forodhani, nyumba ambayo ni nzuri na ya kuridhisha na wale watoto hawajihisi kama wanyonge katika pahali pale, kitu cha kupigiwa mfano hata vile vile alianzisha mambo ya ZAYADESA kupima pia vipimo vya Ukimwi.
Mhe. Spika, nije tena hapo kifungu cha 56:

"Wizara imetoa misaada ya kijamii kwa familia 156; 93 Unguja na 63 Pemba zenye watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi ikiwemo mama waliozaa watoto mapacha watatu. Aidha inaendelea na kuhudumia wazee 91 Sebleni, Welezo 37, Dimbani 8 na wanaoshi Makundeni".

Hizi nyumba kwa kweli hali zao haziridhishi. Mhe. Spika, hii kamati kabla hujanipa uhamisho nilikuwa kamati naifanyia kazi nimeshafika Makundeni hali nimeiona nyumba kule sijui kama zimejengwa katika kipindi hichi. Lakini hali hairidhishi hata nyumba za Limbani hali kweli hairidhishi ya wazee. Pamoja na kuongezwa pesa kusaidiwa lakini hali za nyumba za wazee wetu bado haziridhishi. Serikali imejitahidi imepiga hatua tuipongeze kwa hilo, imepiga hatua lakini hali ya nyumba za wazee hairidhishi ukiangalia ile hali ya Limbani, Makundeni.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije katika kitu ambacho huku nyuma hichi kitabu kiambatanisho namba 1. Jumla ya 1.8 bilioni ukazigawa hizi pesa kwa kila kikundi Wizara ya Fedha imejitahidi kupata kwa asilimia 66, niishukuru Wizara ya Fedha kwa asilimia 66 kwa fedha zilizopatikana kwa wizara hii ni hatua kubwa kidogo.

Lakini Mhe. Spika, baada ya hapo nije kiambatanisho namba 4:

Taarifa iliyokuwa na mfuko wa JK na AK hadi Mei 2015 jumla kuu bilioni 660,715,000 marejesho ni milioni 34. Kwa maana hizi pesa zilizobaki bilioni mia sita. Mimi nafikiri imekuwa sadaka tufahamishwe tu kama imetolewa sadaka, haiwezekani pesa zirejeshwe kama hivi hebu tuangalie katika milioni 660,715,434 ndizo zilizobaki umakini uko wapi hapa kama sadaka ulikuwa tuendelezwe.

Kiambatanisho namba 2 tunaambiwa wanasaidiwa vikundi. Hapa ni kichekesho huwezi kumsaidia mtu shilingi 95 elfu hesabu tuliyoifanya hii. Mwisho kiambatanisho namba mbili jumla kuu 53. Pesa 897 bilioni kwa vikundi ukavigawa

elfu 936 kila kikundi shilingi 95,000 hesabu gani hii, tunamsaidia vipi mtu kwa shilingi 95 elfu, kweli kikundi mtaji unampa shilingi 95,000, *is not serious*!

Mhe. Spika, baada ya hapo nichukue fursa hii kumshukuru Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum kwa kuona vijana angalau kuwaachia kidogo sasa hivi kufanya biashara, na baada ya kuona ukali wa maisha.

Nakushukuru Mhe. Waziri kwa hilo na ukiangalia kipindi chetu cha Ramadhani hichi kinakuja uendelee na moyo huo huo kutokana na ajira zetu kuwa ngumu ni jambo la kukushukuru sana Mhe. Waziri. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

**Mhe. Spika:** Ninazo dakika 12 aliyetangulia kuomba ni Mhe. Amina Iddi Mabrouk, kesho hakuna nafasi na baada ya hapo waliobaki wamuandikie kwa maandishi kesho asubuhi mapema namwita Mhe. Waziri afanye majumuisho. Mhe. Amina Iddi Mabrouk.

**Mhe. Amina Iddi Mabrouk:**Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia jioni hii ya leo tukiwa wazima na afya njema.

Lakini pia nitoe shukurani zangu za dhati kwako wewe kwa kunipa fursa hii na mimi niwe mchangiaji wa bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, lakini pia nichukue nafasi hii kwa dhati kumpongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa namna wanavyofanya kazi vizuri. Lakini si hivyo, tu kwa kufanya kazi ya mashirikiano.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu hautokuwa mkubwa sana, nadhani pengine dakika hizo ulizonipa zitanitosha. Baada ya hapo Mhe. Spika, niingie moja kwa moja katika kitabu hichi cha Mhe. Waziri katika ukurasa wa 19.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mhe. Waziri kama alivyotwambia katika kitabu chake katika ukurasa wa 19 kwa kufanya ziara maalum ya ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo katika wilaya zote za Unguja na Pemba.

Hii Mhe. Spika, ni kazi nzuri, kwa sababu hapo nyuma wizara hii ilikuwa na masikitiko makubwa ya kutokurejeshwa mikopo ambayo wamewapatia wananchi. Lakini Mhe. Spika, mimi nimefarijika sana kuona kwamba bajeti hii imetuonesha kwamba wamefuatilia mikopo ambayo wamewapa wananchi na pesa kwa kiasi zimerejeshwa.

Mhe. Spika, lakini kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri ametuonesha hapa pesa ambazo zimerejeshwa pesa zote zilizorejeshwa ni milioni 362,647,005. Lakini kwa Unguja pesa zilizorejeshwa ni milioni 269,869,005 na kwa Pemba ni milioni 92,778,000.

Mhe. Spika, hii kazi waliyoifanya wizara kwa kweli ni ya matumaini. Lakini ningefurahi zaidi Mhe. Waziri akatuonesha hapa na tukafahamu na tukajua kwamba kwa asilimia gani pesa ambazo zilitolewa katika mikopo hiyo imerejeshwa. Sasa katika kitabu chake hakutwambia kwamba pesa zote ambazo zilizotolewa katika mikopo kwa wananchi ni kiasi kadhaa, lakini na pesa kiasi kadhaa ndio zilizorejeshwa, ili na sisi kama ni Wawakilishi wa wananchi tukaona kwamba kwa kweli wizara imefanya kazi nzuri na kwa kiasi gani pesa ambazo zilizotolewa zimerejeshwa. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho atueleze basi pesa ngapi ambazo zilitolewa kwa wananchi na kwa asilimia mia ngapi zimerejeshwa.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niingie katika ukurasa wa 25. Niipongeze sana serikali kwa kutoa pencheni kwa wazee wetu, kwa kweli imefanya kazi ya busara na imefanya kazi nzuri sana kwa kuona umuhimu mkubwa wa kuwapa pencheni wazee ambao wametimia umri wa miaka 70.

Mhe, Spika, ni dhahiri kwamba wazee kwa asilimia kubwa wazee ambao waliokuwepo hapa Zanzibar hawana watu wa kuwashughulikia, na tegemeo lao kubwa ni kwa Serikali yao ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa hiyo, pamoja na kutoa pencheni Serikali yetu hii ya Mapinduzi lakini bado itambue kwamba wazee hawa wana mahitaji mengine na ya muhimu ya lazima ambayo Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inahitaji kuwasaidia wazee hawa. Kwa mfano mahitaji ya kijamii, huduma ya afya na nyenginezo. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri aweke utaratibu mzuri wa kuratibu namna ya kuwashughulikia serikalini ili ijue wazee hawa watapatikana wapi na afanye tathmini kila Shehia kuona kwamba wazee wako wangapi kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika ukurasa wa 24 udhalilishaji wa wanawake na watoto. Mhe. Spika, kwa kweli tumepiga kelele sana katika Baraza lako hili Tukufu na mara zote inapokuja Bajeti hii ya wanawake kina mama huwa asilimia kubwa katika kuchangia baheti hii ya Wizara ya Wanawake.

Mhe. Spika, mimi nitoe masikitiko yangu kwa kusema kwamba bado udhalilishaji wa watoto unaendelea siku hadi siku hapa nchini kwetu, na inaonekana ufumbuzi hasa haujapatikana kwa sababu sheria tayari imeshatungwa na tuliotunga sisi hapa Mhe. Spika, lakini bado matukio haya yanaendelea siku hadi siku. Sasa mimi

niseme kwamba pengine sheria hii iliyotungwa pengine adhabu zake ni ndogo, kwa hiyo wale wanaofanya matendo haya wamekuwa hawaogopi na ndio maana kila siku wanafanya matukio haya.

Jengine inawezekana hata ufuatiliaji wa sheria hizi ambazo tumezitunga wenyewe. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri hiyo sheria ambayo tuliyoitunga sisi wenyewe basi ifuatilie kwa ukamilifu kuona kwamba wale watoto wetu ambao tumewazaa wenyewe kuona kwamba wanafanyiwa matendo yale basi sheria iweze kutumika kama tulivyoitunga.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika benki hizi za Wanawake. Ni dhahiri kwamba kila siku tunasemea kuhusu kuanzishwa Benki ya wanawake hapa kwetu Zanzibar na sijui kwa nini, mimi nasema kwamba leo ni vizuri Waziri wa Fedha angekuwepo akatusikia michango yetu jinsi gani tunavyosikitika na tunawaonea choyo wenzetu wa Tanzania Bara kwamba Benki ya Wanawake wameianzisha muda mrefu, na sisi nimuombe Mhe. Waziri kwa sababu wako mawaziri wenziwe, basi hapa nina hakika salamu hizo watamfikishia Waziri wa Fedha, kwamba ajitahidi afanye kadiri iwezekanavyo na sisi hapa Wanawake wa Zanzibar tuweze kufaidika na Benki hii ya wanawake ili tuweze kupata mikopo hii iweze kutusaidia kuendesha mambo yetu.

Baada ya hayo kama nilivyosema mchango wangu hautokuwa mkubwa sana, niliona kwamba nichangie bajeti hii kama mwanamke na muda umeshakaribia niseme kwamba Mhe. Waziri atakapokuja kunijibu hoja zangu ambazo nimetaka ufafanuzi basi niseme naunga mkono kwa asilimia mia moja bajeti hii. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Mhe. Amina Iddi Mabrouk tunakushukuru kwa mchango wako huo na kuunga mkono hoja. Kama kuna Wajumbe waliobaki basi wampelekee kwa maandishi Mhe. Waziri ili usiku huu akajitayarishe kufanya majumuisho kesho asubuhi.Mara baada ya kipindi cha maswali tunategemea Mhe. Waziri aje atufanyie majumuisho.

Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana kwa mashirikiano ya kuendesha shughuli hizi. Ila nataka nisisitize tu kwamba mahudhurio yetu bado si mazuri. Kwa hiyo, tujitahidi kuwahi ili shughuli hii isiwe kama ile ya jana ikawa tunaiahirisha kwa sababu hatuna *qourum* ya kupitisha maamuzi. Basi niwashukuru tena baada ya hayo sasa niahirishe kikao hichi hadi kesho tarehe 5/6/2015 saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 1:45 Baraza liliahirishwa hadi*
*tarehe 05/06/2015 saa 3:00 asubuhi)*